# BUNGE LA TANZANIA



# HISTORIA YA BUNGE LA TANZANIA

## (1926 – 2024)

Toleo la Pili 2024

Ofisi ya Bunge

**Kimetayarishwa na:**
**OFISI YA BUNGE**
**10 Barabara ya Morogoro,**
**S.L.P. 941,**
**40490 Tambukareli,**
**DODOMA.**
**Nukushi: +255 26 2324218 Simu: +255 26 2322761-5**

**Barua Pepe: cna@bunge.go.tz**
**Tovuti: www.parliament.go.tz**
**Blog:** @bungetz.blogspot.com

**Toleo la Pili 2024**

**© Ofisi ya Bunge, 2024**

**ISBN 978-991 2-9820-1-7**

Mpigachapa
Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard),
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 941,
4049 Tambuka reli,
DODOMA.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kupigachapa, kutafsiri au kukitoa Kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Ofisi ya Bunge.

Bungetz1 @Bunge_tz Bunge.tanzania BungeTv

## YALIYOMO

**VIFUPISHO** ........................................................................ vi

**DIBAJI**........................................................................................vii

**SHUKURANI** ...................................................................................... ix

**SURA YA KWANZA**..............................................................................1

**BUNGE KABLA NA BAADA YA UHURU** .......................................1

Utangulizi ........................................................................................ 1

Asili ya Neno Bunge ........................................................................ 3

Chimbuko la Bunge la Tanzania ..................................................... 4

Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika ........................................ 5

Mabadiliko ya Baraza la Kutunga Sheria......................................... 6

Baraza la Taifa la Tanganyika Mwaka 1961...................................... 9

Bunge wakati wa Muungano Mwaka 1964 ..................................... 10

Asili ya Jina "Tanzania" .................................................................. 11

Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Bungeni ..................................... 11

Vitambulishi vya Hadhi Bungeni .................................................... 13

Alama za Bunge ............................................................................... 14

**SURA YA PILI** ...................................................................................19

**KATIBA, SHERIA NA KANUNI ZA BUNGE**.................................19

Utangulizi ........................................................................................ 19

Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ya Mwaka 1962 ........ 20
Katiba wakati wa Muungano Mwaka 1964 ..................... 21
Katiba ya Muda ya Mwaka 1965 ..................................... 21
Katiba ya Kudumu ya Mwaka 1977 ................................ 23
Sheria Mahususi za Uendeshaji wa Bunge ..................... 29
Kanuni za Kudumu za Bunge ........................................... 32
**SURA YA TATU ..........................................................34**
**UONGOZI WA BUNGE.................................................34**
Utangulizi ......................................................................... 34
Spika .................................................................................. 34
Naibu Spika ....................................................................... 43
Mwenyekiti wa Bunge....................................................... 51
Tume ya Bunge .................................................................. 51
Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni ..................... 52
Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ...................... 59
Katibu wa Bunge ............................................................... 62
**SURA YA NNE...............................................................69**
**SEKRETARIETI NA OFISI ZA BUNGE..........................69**
Utangulizi ..........................................................................69
Sekretarieti na Tume ya Bunge................. ...................... 69
Muundo wa Sekretarieti ya Bunge .................................. 70

Ofisi za Bunge ........................................................................ 71
**SURA YA TANO**..............................................................................79
**KUMBI ZA BUNGE** ........................................................................79
Utangulizi ............................................................................... 79
Ukumbi wa Shule ya Agha Khan.............................................. 79
Ukumbi wa Anatoglou ............................................................ 80
Ukumbi wa Freemasons.......................................................... 81
Ukumbi wa Karimjee............................................................... 82
Ukumbi wa CCM - Dodoma..................................................... 85
Ukumbi wa Msekwa................................................................. 86
Ukumbi Mpya .......................................................................... 86
**SURA YA SITA** ...............................................................................88
**UJUMUISHAJI WA JINSIA BUNGENI** ...........................................88
Utangulizi ............................................................................... 88
Ujumuishaji wa Jinsia kabla na baada ya Uhuru ..................... 88
Wabunge Wanawake na nyadhifa zao katika vipindi tofauti.......................................................................................... 89
Mabadiliko ya Katiba na Ongezeko la Wabunge Wanawake........................................................................... 90
Wabunge Wanawake Walioshika Nafasi za Uongozi Kitaifa na Kimataifa .............................................................. 91
Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania ............................. 98

Mkakati na Mpango Kazi wa Jinsia Bungeni .................. 99

**SURA YA SABA........................................................................100**

**BUNGE NA DIPLOMASIA YA KIBUNGE ....................100**

Utangulizi ............................................................................ 100

Bunge la Afrika Mashariki ............................................... 101

Bunge la Afrika................................................................... 102

Bunge la Pamoja la Nchi za Umoja wa Ulaya, Afrika, Carribean na Pasifiki ..................................................... 102

Umoja wa Mabunge ya Nchi za Maziwa Makuu ......... 103

Jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ...................................... 104

Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola . 105

Umoja wa Mabunge Duniani ........................................... 106

**SURA YA NANE ...................................................................107**

**MATUKIO MAHUSUSI YALIYOJIRI BUNGENI .......107**

Utangulizi ............................................................................ 107

Hotuba za Marais ................................................................ 107

Hotuba za Wageni Mashuhuri ......................................... 121

Hoja Binafsi, Kamati Teule, Kamati Maalum na Kamati Ndogo za Bunge ............................................................... 125

**SURA YA TISA ......................................................................132**

**MAFANIKIO ...........................................................................132**

Utangulizi ........................................................................ 132
Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo .................. 132
Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu ........... 132
Mabadiliko ya Mfumo na Mzunguko wa Bajeti ........... 133
Kamati ya Bajeti na Ofisi (Idara) ya Bajeti ..................... 133
Uboreshaji wa Miundombinu ........................................ 134
Bunge Mtandao na Mifumo ya Kieletroniki .................. 135
Studio ya Televisheni ya Bunge ..................................... 136
Miongozo ya Utoaji wa Huduma za Bunge .................. 136
Kituo cha Afya............................................................... 136
**MAREJELEO.......................................................................138**
**KIAMBATISHO I: Jedwali la Wabunge Wanawake kuanzia 1954 – 1985..........................................................147**
**KIAMBATISHO II: Ufafanuzi wa baadhi ya Maneno yanayotumika kwenye Shughuli za Bunge....................152**

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| ASP | - | Afro-Shiraz Party |
| BTg | - | Bunge la Tanganyika |
| BTz | - | Bunge la Tanzania |
| CCM | - | Chama Cha Mapinduzi |
| CHADEMA | - | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| CUF | - | Civic United Front |
| JMT | - | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| LAPF | - | Local Authorities Pension Fund |
| LEGCO | - | Legislative Council |
| PMO | - | Prime Minister's Office |
| SMZ | - | Serikali ya Mapinduzi Zanzibar |
| TAMISEMI | - | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANU | - | Tanganyika African National Union |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| URT | - | United Republic of Tanzania |
| IPU | - | Inter-Parliamentary Union |
| CPA | - | Common-wealth Parliamentary Association |

# DIBAJI



Kitabu hiki kinaelezea mambo yaliyotokea katika Historia ya Bunge, Maendeleo yake, Safu za Uongozi na Mafanikio tangu mwaka 1926 hadi mwaka 2024. Kitabu kina jumla ya Sura Tisa zinazoelezea kwa undani masuala mbalimbali katika historia ya Bunge la Tanzania.

Bunge la Tanzania ambalo kwa asilimia kubwa linafuata utaratibu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola, chimbuko lake linaanzia wakati wa ukoloni wa Mwingereza baada ya utawala huo kuanzisha Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika mwaka 1926. Tangu mwaka huo hadi sasa, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limepitia hatua mbalimbali kutoka Baraza la Kutunga Sheria, Baraza la Taifa, Bunge la Tanganyika na hatimaye Bunge la Tanzania. Katika hatua hizo kumekuwa na mabadiliko kadhaa ya Muundo, Uongozi, Aina za Wabunge, Sifa za kuwa Mbunge na Kamati za Bunge.

Dhamira ya mabadiliko hayo ni kuwa na Bunge lenye kuwakilisha na kuwajibika kwa Wananchi, huku Dhima yake kuu ikiwa ni kuendelea kuwa sauti ya watu kwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika Kutunga Sheria, Kusimamia Serikali, Kuridhia Mikataba, Kuchambua na Kupitisha Bajeti ya Serikali.

Ni matumaini yangu kuwa kitabu hiki kitatoa ufahamu wa kutosha kwa Bunge, Watafiti, Wahadhiri, Wakufunzi, Walimu, Wanafunzi na Wadau mbalimbali kuhusu masuala ya kibunge. Aidha, kwa lengo la kutunza historia na kumbukumbu ya Taasisi hii na Taifa kwa ujumla, kitabu kitakuwa rejea muhimu kwa kuwa kinaelezea pia mabadiliko na mafanikio ya Bunge letu kwa kipindi cha miaka 95 ya utekelezaji wa majukumu yake kuanzia mwaka 1926 hadi mwaka 2021.

Dkt. Tulia Ackson

**SPIKA**

## SHUKURANI



Uandishi wa kitabu kama hiki hukamilika kutokana na michango ya watu na taasisi mbalimbali. Ni kwa muktadha huo, napenda kutambua na kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe Dkt. Tulia Ackson Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa heshima kubwa Viongozi Wastaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Taasisi za Serikali, Maspika na Watumishi Wastaafu pamoja na wadau mbalimbali kwa kushirikiana na Sekretarieti niliyoiteua.

Hivyo, napenda kuwatambua wafuatao:- Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba, Mhe. Pius Msekwa, Mhe. Anne Semamba Makinda, Mhe. Job Yustino Ndugai, Mhe. Balozi Dkt. Getrude Mongela, Mhe. Paul Kimiti, Dkt. Thomas Kashililah, Ndg. Alex Banzi, Ndg. Eliakim Mrema, Ndg. Japhet Sagasii, Ndg. Ramadhan Issa Abdallah, Ndg. Abdallah Selemani Mwinyipembe, Ndg. Abdallah Mwanga, Ndg. Abdallah Tambaza, Ndg. Mohamed Said na Ndg. Amiri Sudi Andanenga.

Aidha, napenda kutambua michango ya Taasisi zifuatazo:- Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Maktaba Kuu ya Taifa, Idara ya Habari Maelezo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Makumbusho ya Taifa, na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Pia, nawapongeza Watumishi wa Ofisi ya Bunge walionisadia kuandika Kitabu hiki ambao ni:- Ndg. Deogratias Egidio, Ndg. Daniel Eliufoo, Ndg. Abdallah Hancha, Ndg. Angumbwike Ng'wavi, Ndg. Joshua Chamwela, Ndg. Pili Omari, Ndg. Zainab Issa, Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Aziza Makwai, Ndg. Francisca Haule, Ndg. Mwajuma Ramadhan, Ndg. Halid Jumanne na Ndg. Deonisius Simba.

Kipekee, namshukuru Katibu wa Bunge aliyenitangulia, Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuanzisha kazi ya uandishi wa Kitabu hiki ulioanza Novemba, 2019.

Vilevile, shukurani za dhati ziwaendee watu wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kufanikisha ukamilishaji wa Kitabu hiki. Aidha, natoa shukurani zangu kwa Wahariri ambao ni Mhe. Pius Msekwa (Spika Mstaafu) na Ndg. Charles Mloka (Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Mstaafu) pamoja na Wachapishaji kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc*
**KATIBU WA BUNGE**

# SURA YA KWANZA

## BUNGE KABLA NA BAADA YA UHURU

### Utangulizi

Chanzo cha Mabunge Duniani kinatokana na dhana ya mgawanyo wa madaraka katika uendeshaji wa dola ambapo kunapaswa kuwa na Serikali, Bunge na Mahakama. Dhana hii imefafanuliwa vizuri na Mwanafalsafa wa Kifaransa Baron de Montesquieu katika Kitabu chake kiitwacho *The Spirit of the Laws* (1748). Montesquieu katika kitabu hicho ameelezea aina mbalimbali za mgawanyo wa madaraka ya utawala baina ya Bunge, Mahakama na Serikali. Dhana hiyo inafafanua kuwa madaraka yasiwe kwenye mhimili mmoja wa dola bali uwepo mfumo wa kudhibitiana kwa mihimili ya dola, yaani Bunge litunge Sheria, Serikali itekeleze Sheria iliyotungwa na Bunge, na Mahakama itafsiri sheria hizo na kutoa haki kwa kuzingatia sheria zilizopo.

Dhana hiyo inasisitiza kuwa utungaji na utekelezaji wa sheria ukifanywa na mtu mmoja au kundi moja unaweza kupunguza uhuru kwa raia, kutungwa kwa sheria kandamizi, matumizi mabaya ya rasilimali za nchi na masuala mengine yasiyofaa. Hivyo, Tanzania ikiwa ni

sehemu ya dunia, inafuata mfumo huo wa utawala unaozingatia mgawanyo wa madaraka.

Mabunge mengi duniani yapo kwa ajili ya jukumu la uwakilishi wa wananchi. Hivyo Bunge ni mkusanyiko wa wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa madhumuni ya kufanya maamuzi muhimu kwa maslahi na maendeleo ya taifa husika. Mabunge mengi hapa duniani yamegawanyika katika aina kuu mbili: aina ya kwanza ni "Unicameral" yaani Bunge lenye mamlaka moja ambapo wawakilishi wote wa wananchi (wabunge) hukaa na kufanya maamuzi pamoja bila ya ulazima wa maamuzi hayo kupitiwa tena na chombo kingine cha Uwakilishi; na aina ya pili ya Bunge hujulikana kama "Bicameral" yaani Bunge lenye Mamlaka/sehemu mbili ziitwazo Seneti (Mamlaka ya Juu) na Bunge la Kawaida (Mamlaka ya Chini). Kazi za Seneti zinajumuisha kuthibitisha au kukataa Sheria zilizopitishwa na Bunge la Kawaida. Aidha, katika nchi zingine upande wowote unaweza kupitisha au kukataa Sheria zilizotungwa na upande mwingine. Kwa kawaida Wajumbe wa Bunge la Kawaida hupatikana kwa kuchaguliwa na Wananchi, wakati wale wa Seneti hupatikana kwa kuteuliwa au kuchaguliwa kulingana na utaratibu wa nchi husika.

Kama ilivyo katika mabunge mengine, Bunge la Tanzania pia ni chombo cha kutunga Sheria na ni mojawapo ya mihimili mitatu inayounda mfumo wa Utawala kulingana na mgawanyo wa Madaraka katika dola, mihimili mingine ni Mahakama na Serikali. Kwa kuzingatia aina hizo, Bunge la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni lenye mamlaka moja (Unicameral) ambalo katika utekelezaji wa majukumu yake hujigawa katika sehemu mbili, yaani Rais (President) na Bunge lenyewe (National Assembly).

**Asili ya Neno Bunge**

Neno "Bunge" linatokana na lugha za makabila ya Tanga likiwa na maana ya mikutano ya kijadi ya kufanya maamuzi juu ya jambo fulani. Historia hiyo inathibitishwa katika kitabu kiitwacho *History of Kiswahili Poetry* A.D 1000 - 2000 kilichotungwa na Prof. Mugyabuso M. Mulokozi na Prof. Tigiti S. Y. Sengo. Utafiti uliofanywa na wasomi hao, unabainisha kwamba aliyependekeza jina la Bunge kama kisawe cha *Parliament* ni mshairi maarufu kutoka mkoa wa Tanga aliyejulikana kwa jina la Ghulam Mabondo bin Mwinyimatano ambaye pia alikuwa mtaalamu na mpenzi mkubwa wa lugha ya Kiswahili. Aidha, watafiti hao wanaeleza kwamba pendekezo la Mwinyimatano lilipokelewa na Mwinyikhatibu Mohammed aliyekuwa mshairi na mpenzi mwingine wa Kiswahili kutoka Tanga. Mwinyikhatibu alilipeleka neno hilo kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya lugha aliyejulikana kwa jina la Sheikh Kaluta Amri Abeid ambaye aliliwasilisha neno "Bunge" kwa Rais Julius Kambarage Nyerere na kuomba aridhie litumike kama kisawe cha neno *Parliament*. Mwalimu Nyerere aliridhia na neno hilo likaanza kutumika rasmi mwaka 1962.

**Chimbuko la Bunge la Tanzania**

Historia ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaanza wakati wa Utawala wa Uingereza ndani ya Tanganyika mwaka 1920 ambapo Gavana wa kwanza wa Kiingereza Horace Arche Byatt alianzisha Baraza la Kumshauri Gavana na yeye kuwa Mwenyekiti. Gavana Byatt aliitumikia nafasi yake hadi Novemba, 1924. Mnamo mwaka 1925 aliteuliwa Gavana wa Pili, Sir. Donald Cameron kushika nafasi hiyo, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake rasmi tarehe 5 Machi, 1925, nafasi ya Gavana ilishikiliwa kwa muda na John Scott. Baada ya kuingia madarakani pamoja na mambo mengine, Sir Cameron aliishauri Serikali ya Uingereza kuanzisha Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika. Serikali ya Uingereza ilikubali na hivyo Bunge la Uingereza likatunga Sheria iliyojulikana kama "*The Tanganyika (Legislative Council) Order in-Council*, 1926" tarehe 19 Machi, 1926. Sir Cameron, aliteuwa wajumbe ishirini kuunda Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika ambalo lilizinduliwa tarehe 10 Oktoba, 1926. Mkutano wa Kwanza wa Baraza hilo ulifanyika tarehe 7 Disemba, 1926, Dar es Salaam, Katibu wa Baraza hilo akiwa G. F. Sayers. Wakati Baraza la Kutunga Sheria likianzishwa Tanganyika, kwa upande wa Zanzibar kulikuwa na Baraza la Utendaji na Baraza la Kutunga Sheria la Zanzibar, 1926 (The Executive Council and Legislative Council of Zanzibar, 1926).



**Sir Horace Arche Byatt**



**Sir Donald Cameron**

**Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika**

Baraza la Kutunga Sheria lilianza na Wajumbe ishirini ambao waliteuliwa na Gavana Sir Donald Cameroon akiwa Mwenyekiti wa Baraza, kati ya hao, Wajumbe kumi na tatu walikuwa watumishi wa Serikali (Wazungu) na Wajumbe saba (watano walikuwa Wazungu na wawili walikuwa Waasia) waliowakilisha mawazo ya raia. Aidha, Baraza la Kutunga Sheria lilipewa madaraka ya kutawala na si kushauri tu, kama alivyosema Gavana Donald Cameron siku alipofungua mkutano wa kwanza wa Baraza hilo (kwa tafsiri isiyo rasmi):-

*"Baraza hili lisiruhusiwe kabisa kuwa ni mahali pa kutumiwa na Serikali kwa maoni yake tu. Napenda kusisitiza kuwa ni kwa sababu hiyo, ndiyo maana nikashauri kwamba lianzishwe Baraza ambalo litachukua sehemu ya madaraka ya kuitawala nchi hii, na si Baraza ambalo kazi yake ni kutoa mashauri tu".*

Kwa wakati huo, muswada wa sheria ulipopitishwa na Baraza ulisainiwa na Gavana na kupelekwa nchini Uingereza ili kupata idhini ya kuwa sheria.

Kwa takriban miaka ishirini Baraza la Kutunga Sheria halikuwa na Wajumbe Waafrika. Katika kipindi chote hicho, Gavana aliteuwa watu mbalimbali wasio Waafrika

kuwakilisha maoni ya Wananchi kwenye Baraza, mmoja wao akiwa Bw. Robert Mortimer Gibbons aliyeteuliwa tarehe 7 Machi, 1931 ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkuu wa Chuo cha Minaki. Waafrika wa kwanza kuwa Wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria waliteuliwa tarehe 24 Novemba, 1945, wakati wa uongozi wa Gavana William Battershill. Wajumbe walioteuliwa walikuwa Chifu Abdiel Shangali na Chifu Kidaha Makwaia.

Uteuzi wa wajumbe hao ulitangazwa katika Ilani ya Serikali (Government Notice) Namba 1046 ya tarehe 30 Novemba, 1945. Mjumbe Mwafrika wa tatu alikuwa ni Chifu Adam Sapi Mkwawa aliyeteuliwa tarehe 3 Juni, 1947; na Mjumbe wa nne alikuwa Bw. Juma Mwindadi aliyeteuliwa tarehe 1 Aprili, 1948. Wakati huo wote Gavana aliendelea kuhudhuria Mikutano ya Baraza la Kutunga Sheria akiwa Mwenyekiti wa Baraza. Aidha, kulikuwa na Baraza la kumshauri Gavana ambapo waliteuliwa wajumbe wazawa (miongoni mwa wananchi) wafuatao: Chifu Kidaha Makwaia aliyeteuliwa tarehe 16 Aprili, 1951 na Chifu Adam Sapi Mkwawa aliyeteuliwa tarehe 25 Mei, 1954.

**Mabadiliko ya Baraza la Kutunga Sheria**

Kulikuwa na Mabadiliko makubwa manne katika Baraza la Kutunga Sheria kati ya mwaka 1945 hadi mwaka 1960.

**Mabadiliko ya Kwanza Mwaka 1945**

Mabadiliko ya kwanza makubwa yalihusu kuingia kwa Waafrika kwenye Baraza la Kutunga Sheria ambalo awali

lilijumuisha Wazungu na Waasia pekee kwa takribani miaka ishirini.

**Mabadiliko ya Pili Mwaka 1953**

Mwaka 1953 yalifanyika mabadiliko ya pili katika Baraza ambapo Gavana alikoma kuwa Mwenyekiti na nafasi yake ilichukuliwa na Spika. Wakati huo Gavana aliendelea na majukumu ya kumwakilisha Malkia kama Mkuu wa Baraza la Kutunga Sheria na alihudhuria Baraza endapo alikuwa na jambo la kuhutubia. Spika wa Kwanza wa Baraza la Kutunga Sheria, alikuwa Brigedia William E. H. Scupham aliyeapishwa tarehe 01 Novemba, 1953 na kuanza kazi rasmi tarehe 17 Novemba, 1953. Wajumbe wake waliendelea kuwa wanaume mpaka miaka miwili baadaye ambapo Baraza lilipata wajumbe watatu Wanawake ambao ni: Bibi Elifuraha Mkamangi Marealle, Bibi K.F Walker na Bibi S. Keeka; waliochaguliwa na kuapishwa, tarehe 19 Aprili, 1955.

**Mabadiliko ya Tatu Mwaka 1958**

Mabadiliko ya tatu ya Baraza yalifanyika mwaka 1958, ambapo Baraza lilipata Wajumbe kupitia uchaguzi ulioshirikisha vyama vitatu vya siasa: *Tanganyika African National Union* (TANU), *United Tanganyika Party* (UTP) na *African National Congress* (ANC). Baada ya uchaguzi kufanyika chama cha TANU pekee ndicho kilichopata Wajumbe wawakilishi kwenye Baraza hilo. Katika uchaguzi huo kulikuwa na mjumbe wa Baraza, Herman Sarwatt aliyeshinda nafasi yake kupitia kiti cha ujumbe wa jimbo la

Mbulu akiwa mgombea binafsi. Awali mjumbe huyu, aligombea ubunge kupitia tiketi ya TANU na kushinda kwenye kura za maoni lakini hakupata nafasi ya kugombea kupitia chama hicho.

**Mabadiliko ya Nne Mwaka 1960**

Mabadiliko ya nne ya Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika yalitokea tarehe 30 Juni, 1960 ambapo Baraza lilivunjwa rasmi na kufuatiwa na Uchaguzi Mkuu wa pili tarehe 30 Agosti, 1960. Uchaguzi huo ulikuwa ni sehemu ya maandalizi ya Uhuru wa Tanganyika. Aidha, tarehe 1 Mei, 1961 Baraza la Kutunga Sheria lilibadilika na kuwa Baraza la Taifa la Tanganyika *(*Tanganyika National Assembly*)* kwa Sheria iliyojulikana kama *The Tanganyika (Constitution) Order – in – Council,* 1961.



*Mwalimu Nyerere akiapishwa kuwa Mjumbe katika Baraza la Kutunga Sheria Mwaka 1960*

**Baraza la Taifa la Tanganyika Mwaka 1961**

Mchakato wa uhuru wa Tanganyika ulipitia hatua mbalimbali hivyo Bunge nalo lilibadilika ili kuendana na hatua hizo. Mwezi Septemba, 1960 Tanganyika ilipata madaraka ya ndani ambapo Mwalimu Julius Nyerere alikuwa Waziri Mkuu na hivyo kuongoza Shughuli za Serikali Bungeni, ingawa nchi iliendelea kuwa chini ya utawala wa Uingereza hadi tarehe 9 Desemba, 1961 ilipopata Uhuru kamili.

Katika kipindi hiki Baraza la Taifa la Tanganyika liliendelea kuundwa na Malkia wa Uingereza aliyewakilishwa na Gavana Jenerali. Wajumbe wa Baraza hilo waligawanyika katika makundi mawili: wajumbe wa kuchaguliwa na wajumbe wa kuteuliwa na Gavana Jenerali baada ya kushauriana na Waziri Mkuu. Sheria zilizotungwa na Baraza hilo ziliridhiwa na Gavana kwa niaba ya Malkia.

**Bunge la Jamhuri ya Tanganyika Mwaka 1962**

Tanganyika ilikuwa Jamhuri mwaka 1962 baada ya uchaguzi wa Rais ambaye alikuwa Kiongozi Mkuu wa nchi akisaidiwa na Makamu wa Rais. Katika hatua hiyo, Sheria zote zilizotungwa na Bunge ziliridhiwa na Rais badala ya Gavana kama ilivyokuwa awali. Aidha, Mhe. Rashid Mfaume Kawawa aliyekuwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wa Tanganyika ndiye alikuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

**Bunge wakati wa Muungano Mwaka 1964**

Mchakato wa kisheria wa kuunganisha Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ili kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulianzishwa kwa Hati ya Muungano ya mwaka 1964 iliyojulikana kama *The Articles of Union Between the Republic of Tanganyika and the People's Republic of Zanzibar*. Hati hiyo ilitiwa saini tarehe 22 Aprili, 1964 na Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika kwa upande mmoja, na Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, kwa upande mwingine. Bunge la Tanganyika na Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi na Makamisaa kutoka Zanzibar walikutana kwa dharura tarehe 25 Aprili, 1964 ambapo Rais wa Tanganyika, Mwalimu Nyerere aliwaomba waridhie Mkataba wa Muungano. Aidha, Wajumbe waliridhia Mkataba huo na kupitisha Sheria ya Muungano huo "*The Union of Tanganyika and Zanzibar Act, 1964*" kwa Hati ya dharura.

Sheria hiyo ya Muungano ilitamka kuwa, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ungeanza rasmi siku inayofuata ya tarehe 26 Aprili, 1964 ambapo kila kitu kilichokuwa cha Tanganyika kiligeuka kuwa cha Jamhuri ya Muungano, hii ikiwa ni pamoja na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Tanganyika. Bunge la Tanganyika nalo likageuka kuwa la Jamhuri ya Muungano na watumishi wake kuwa watumishi

wa Bunge hilo. Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ilitambuliwa rasmi katika Umoja wa Mataifa kwa Hati ya Muungano iliyowasilishwa tarehe 30 Aprili, 1964.

**Asili ya Jina "Tanzania"**

Baada ya Muungano lilianzishwa shindano la kutafuta jina jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kutoka ndani na nje ya nchi. Baadhi ya majina yaliyopendekezwa yalikuwa ni *Tangbar*, *Tanzani* na *Tanzania* ambapo jina la *Tanzania* lililobuniwa na Mohammed Iqbal Dar, Mtanganyika mwenye asili ya ki-Asia lilikubaliwa na kushinda na hivyo kuunganishwa kwenye jina la "Jamhuri ya Muungano" na kuwa "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".

Jina "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" lilianza kutumika rasmi tarehe 10 Desemba, 1964, baada ya Sheria ya Bunge iliyoitwa *The United Republic (Declaration of Name) Act, 1964* kusainiwa na Rais. Hatimaye, jina la nchi lilitangazwa kuwa "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" badala ya jina la awali la "Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar". Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa alijulishwa na kutambulishwa rasmi mabadiliko ya jina hilo jipya tarehe 18 Desemba, 1964.

**Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Bungeni**

Wakati wa Utawala wa Mwingereza nchini Tanganyika, lugha iliyotumika kwenye mijadala ya Baraza la Kutunga Sheria ilikuwa ni Kiingereza. Utaratibu huo uliendelea hadi mwaka 1945, walipoteuliwa Waafrika: Chifu A. Shangali na

Chifu K. Makwaia, kuwa Wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria ambao walianzisha vuguvugu la matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala ya Baraza hilo. Vuguvugu hilo liliendelea hadi mwaka 1950 katika Kikao cha Ishirini na Tano cha Baraza hilo ambapo Chifu Shangali aliwasilisha rasmi hoja ya kutaka kutafsiri hati zote za Baraza kwa lugha ya Kiswahili. Hoja hiyo ilipingwa vikali na Wajumbe wengi waliokuwa Wazungu kwa sababu mbalimbali ikiwemo ya kutojitosheleza kwa lugha ya Kiswahili kisarufi na kimsamiati.

Hoja ya matumizi ya lugha ya Kiswahili iliendelea kuungwa mkono hata baada ya kuanzishwa kwa Chama cha TANU mwaka 1954 ambapo miongoni mwa masuala mengine iliamuliwa Kiswahili kitumike kama lugha ya pili kwenye Baraza la Kutunga Sheria. Aidha, katika Mkutano Mkuu wa TANU wa mwaka 1958 iliazimiwa kuwa Kiswahili kiwe lugha rasmi ya Tanganyika baada ya uhuru. Ili kuthibitisha kwamba Kiswahili ni lugha yenye kujitosheleza kisarufi na kimsamiati, Rais wa Tanganyika, Mwalimu Julius Nyerere, alihutubia Bunge kwa mara ya kwanza tarehe 10 Desemba, 1962, kwa lugha ya Kiswahili. Hotuba hiyo ilidhihirisha kuwa Kiswahili kinaweza kutumiwa kwenye mijadala ya Bunge bila kuathiri hadhi wala ufanisi wake.

Katika Kikao cha Pili cha Mkutano wa Tano wa Bunge, tarehe 12 Februari, 1963, Spika wa Bunge aliwakumbusha Wabunge kuanza rasmi kutumia lugha ya Kiswahili badala ya Kiingereza pekee katika mijadala ya Bunge kama

ilivyotangazwa tarehe 6 Septemba, 1962 na Makamu wa Rais, Rashidi Mfaume Kawawa, kwamba Kiswahili ndiyo lugha rasmi ya Taifa. Aidha, kwa kuwa Bunge lilijumuisha Waafrika, Wazungu na Waasia, mazingira hayo yalilazimisha matumizi ya lugha mbili sambamba: Kiswahili na Kiingereza ambapo lugha hizo zimeendelea kuwa lugha rasmi katika mijadala ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi sasa.

**Vitambulishi vya Hadhi Bungeni**

Kwa mujibu wa utaratibu wa kibunge, vipo vitambulishi vya hadhi vinavyopaswa kutumika kabla ya kutaja jina au cheo cha Mbunge. Tangu kuanza kwa Bunge la Jamhuri ya Tanganyika mwaka 1962 hadi sasa, kumekuwa na mabadiliko kadhaa ya vitambulishi. Kuanzia mwaka 1962, vitambulishi vya maneno Bwana, Bibi au Bi vilitumika kabla ya kumtaja Spika au Mbunge yeyote. Maneno Bwana, Bibi au Bi yametafsiriwa kutoka katika maneno ya lugha ya Kiingereza *Mister* au *Mistress (Mr./Mrs.* na *Miss).*


Matumizi ya vitambulishi hivyo yaliendelea hadi mwaka 1974 vilipobadilishwa na kuwa "Ndugu". Mabadiliko hayo yalilenga kuondoa matumizi ya neno "Bwana" lililoashiria dhana ya Ubwana na Utwana ambayo ilikinzana na itikadi ya wakati huo ya Ujamaa na Kujitegemea. Mwaka 1987 ilitolewa hoja Bungeni kwamba neno "Mheshimiwa" litumike badala ya neno "Ndugu". Hoja hiyo ilijengwa kutokana na utaratibu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola hususan Bunge la Uingereza ambalo hutumia kitambulishi

cha neno *Honorable* likiwa na maana "Mheshimiwa". Hoja hiyo iliungwa mkono na kukubalika na hivyo kuanza kutumika rasmi na kuendelea hadi sasa.

**Alama za Bunge**

Kama ilivyo katika mihimili mingine ya dola, Bunge pia lina alama mahususi za utambulisho wake. Alama hizo ni kama ifuatavyo:-

**Siwa**



Siwa ni rungu lililonakishiwa kwa dhahabu linalotumika kama kielelezo cha mamlaka ya Bunge, ambalo hubebwa na Mpambe wa Bunge. Awali, Baraza la Kutunga Sheria chini ya uenyekiti wa Gavana halikuwa na alama yoyote ya kuonesha mamlaka. Kwa mujibu wa utamaduni wa mabunge ya nchi za jumuiya ya madola, mamlaka ya Spika hudhihirishwa kwa kutumia Siwa (Mace), ambapo Siwa ya kwanza ya Tanganyika ililetwa na Serikali ya Uingereza na ilikabidhiwa kwa Spika na Gavana wa Tanganyika, Sir Edward Twining tarehe 13 Oktoba, 1954. Wakati akiikabidhi Siwa hiyo kwa Spika alisema (tafsiri isiyo rasmi):-

> *"Nakukabidhi wewe Bwana Spika Mesi hii ya alama ya Cheo, ambayo ni alama ya mamlaka ya Kifalme, kwa idhini ya Mtukufu Malkia wetu, na kukuagiza wewe na watakaoshika kazi yako kuwa walinzi wa haki ya Mesi hii"*



Baada ya Uhuru, Bunge liliendelea kutumia Siwa iliyoletwa na Serikali ya Uingereza iliyokuwa na alama ya Taji la Malkia, kama alama na mamlaka ya Spika. Hata hivyo, muonekano huo ulibadilishwa kwa kuondoa alama ya Taji la Malkia na kuwekwa alama ya Mwenge wa Uhuru na meno ya tembo. Aidha, Siwa hiyo yenye uzito wa wastani wa kilo nane na urefu wa takriban futi tano imenakshiwa kwa madini ya dhahabu.

Kwa kawaida Spika au mwakilishi wake anapoingia au kutoka ukumbini hutanguliwa na Mpambe wa Bunge akiwa amebeba Siwa, ambayo huwekwa mezani wakati Spika amekalia kiti chake. Aidha, Siwa inapokuwa ndani ya droo (*draw*) humaanisha Bunge linakutana kama Kamati ya Bunge Zima wakati wa kupitisha muswada wa sheria na maazimio, au kamati ya matumizi wakati wa kupitisha bajeti za wizara na bajeti ya Serikali au kujadili mpango wa maendeleo.

**Bendera ya Bunge**



Utaratibu wa kuwa na Bendera ya Bunge ulianza mwaka 1992, ikiwa ni sehemu ya kuendana na mfumo wa vyama vingi vya Siasa. Bendera ya Bunge ilibuniwa na Kamati ya Uongozi ya Bunge. Kwa mujibu wa Spika mstaafu Msekwa, Kamati hiyo ilizingatia msingi kwamba Bunge ni

miongoni mwa mihimili ya dola na hivyo, dhana hiyo ilipaswa kudhihirishwa katika bendera ya Bunge. Ili kutekeleza hilo, Kamati iliamua kwamba bendera ya Bunge iwe na kitambaa cha rangi ya buluu, ikiashiria bahari iliyopo katikati ya Tanzania Bara na Zanzibar na ikinakshiwa na bendera ya nchi na Siwa kama alama ya Bunge.

Aidha, Bendera ya Bunge ilianza kutumika rasmi mwaka 2004 baada ya Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Na. 3 ya Mwaka 1988 kufanyiwa Marekebisho mwaka 2004, ili kuwezesha matumizi sahihi ya Bendera ya Bunge kwenye Ofisi za Bunge na Wabunge, Viongozi wa Bunge na kupererushwa kwenye magari ya Wabunge.

**Nembo ya Bunge**

Nembo ya Bunge ilianzishwa kwa ajili ya kuutambulisha Mhimili wa Bunge. Nembo hii ilipatikana kwa kushindanisha wabunifu mbalimbali na baadaye kupata ithibati na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kabla ya kuanza kutumika mwaka 2004. Nembo ya Bunge inatumika katika nyaraka zote zinazoandaliwa na kuchapwa na Ofisi ya Bunge. Kabla ya mwaka 2004 nyaraka zote zilizozalishwa na Bunge zilitumia Nembo ya Taifa.

### Vazi la Spika kuanzia Mwaka 1994



Mara baada ya kustaafu kwa Chifu Adam Sapi Mkwawa mwaka 1994, Spika aliyefuata alikuwa Pius Msekwa ambaye hakuwa Chifu, hivyo hakuwa na vazi kama wenzake waliotangulia. Katika mazingira hayo iliamualiwa kuwa lipatikane vazi rasmi litakalotumiwa na Spika. Hivyo, iliundwa Kamati Maalum ya Bunge kwa ajili ya kubuni na kupendekeza vazi rasmi la Spika. Baada ya Kamati kukamilisha kazi yake, mapendekezo ya ubunifu yalipelekwa Uingereza kwa ajili ya kutengeneza vazi hilo. Vazi hilo lililoanza kutumika mwaka 1994, limenakshiwa kwa rangi za bendera ya Taifa na alama mbalimbali zinazowakilisha rasilimali za nchi kama vile madini na mazao.

### Kiti cha Spika



Kiti cha Spika ni miongoni mwa alama za Bunge. Kiti hicho hutumiwa na Spika, Naibu Spika au Mwenyekiti wa Bunge wakati wa kuongoza vikao vya Bunge. Kiti hicho kina nakshi tofauti ikilinganishwa na viti wanavyokalia Wabunge wengine. Tangu Uhuru wa Tanganyika, Bunge limekuwa na aina sita za viti, kikiwemo kilichotolewa zawadi na Bunge la Uingereza (House of Commons) kwa Bunge la Tanganyika. Kiti hicho kiliboreshwa kwa kuwekwa nembo


ya Taifa la Tanganyika na baadaye nembo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# KATIBA, SHERIA NA KANUNI ZA BUNGE

## Utangulizi

Bunge ni zao la Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 62 ya Katiba ya Kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katiba hii pamoja na Katiba za awali zimefanyiwa mabadiliko mara kadhaa ambayo baadhi yake yamekuwa na matokeo ya moja kwa moja kwa Bunge katika muundo, majukumu, aina za Wabunge, sifa za kuwa Mbunge na maeneo mengine yanayohusu Bunge na Wabunge. Aidha, katika utekelezaji wa shughuli zake Bunge kwa nyakati tofauti lilitunga Sheria na Kanuni kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

## Katiba ya Tanganyika ya Mwaka 1961




Katiba hii iliyodumu kwa mwaka mmoja iliandikwa chini ya usimamizi wa Malkia wa Uingereza na ilikuwa ya maridhiano na makubaliano kati yake na Watanganyika kwa lengo la kuwawezesha kupata Uhuru. Makubaliano hayo yalifikiwa katika Mkutano wa Katiba uliofanyika Karimjee Hall, Dar es Salaam, kuanzia tarehe 27 hadi 29 Machi, 1961. Kabla ya hapo, kulikuwa na Serikali ya Madaraka ya ndani iliyoongozwa na

Mwalimu Julius Nyerere akiwa Waziri Mkuu chini ya usimamizi wa Gavana kwa niaba ya Malkia, kuanzia Septemba, mwaka 1960. Uhuru kamili wa Tanganyika ulipatikana tarehe 9 Desemba, 1961.

Muundo wa Bunge (Baraza la Taifa) kwa mujibu wa Ibara ya 14 ya Katiba ya mwaka 1961, lilikuwa na sehemu mbili ambazo ni Malkia wa Uingereza na Wabunge. Ibara ya 25 na 29 za Katiba hii zilibainisha majukumu mawili ya Bunge ambayo ni kuendesha na kusimamia shughuli zote za uchaguzi na kutunga sheria. Ibara ya 16 na 17 (1) zilitamka uwepo wa aina mbili za Wabunge kwa maana ya Wabunge wasiozidi kumi wa kuteuliwa na Gavana kwa kushauriana na Waziri Mkuu na Wabunge sabini na moja wa kuchaguliwa. Ibara ya 18 ilianisha sifa za mtu kuwa Mbunge kuwa ni raia wa Tanganyika, awe ametimiza umri wa miaka ishirini na moja, na awe na uwezo wa kuongea na kusoma Kiingereza kwa ufasaha isipokuwa kama ni mlemavu wa kuona au ana ulemavu mwingine.

**Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ya Mwaka 1962**
Katiba hii ilitungwa na Bunge, baada ya Bunge hilo kukaa kama Bunge Maalum la Katiba. Katiba hiyo ilipitishwa tarehe 23 Novemba, 1962 na kuanza kutumika tarehe 9 Desemba, 1962 ambapo pamoja na mambo mengine ilianzisha nafasi ya Makamu wa Rais. Muundo wa Bunge chini ya Katiba hii uliendelea kuwa na sehemu mbili ambazo ni Rais wa Tanganyika (badala ya Malkia) na Wabunge.

Upitishwaji wa Katiba hii ulitanguliwa na uchaguzi wa Rais wa vyama vingi uliofanyika tarehe 1 Novemba, 1962 ambapo Mwl. Julius Kambarage Nyerere, chini ya chama cha TANU alichaguliwa kuwa Rais wa Tanganyika. Vyama vingine vilivyoshiriki katika uchaguzi huo ni:- *African National Congress* (ANC) na *United Tanganyika Party* (UTP).

**Katiba wakati wa Muungano Mwaka 1964**

Baada ya Muungano, Rais alitoa Matamko mbalimbali ya kisheria (Decrees) ya kuifanya Jamhuri ya Zanzibar kuwa sehemu ya Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ya mwaka 1962. Mathalani, Rais alitoa Tamko (Decree) Na. 235 lililochapishwa katika Gazeti la Serikali, Juzuu XLV Na. 30 la tarehe 28 Aprili, 1964. Tamko hilo liliweka bayana kuwa, tangu siku ya Muungano, kila kitu kilichokuwa cha Tanganyika kiligeuka kuwa cha Jamhuri ya Muungano, ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ya mwaka 1962.

Katiba hiyo ilipewa jina la Katiba ya Muda ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (*The Interim Constitution of the United Republic of Tanganyika and Zanzibar).* Bunge la Tanganyika nalo liligeuka kuwa la Jamhuri ya Muungano pamoja na watumishi wake kuwa watumishi wa Bunge hilo.

**Katiba ya Mpito ya Mwaka 1965**



Bunge la Jamhuri ya Muungano lilitunga Katiba ya Muda ya Tanzania ya Mwaka 1965 (The Interim Constitution of the United Republic of Tanzania, 1965 ambayo ilimtaja Rais wa Zanzibar

kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, akiwa ni msaidizi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano katika masuala yote ya kiutawala kwa upande wa Zanzibar. Aidha, ilitamka kuwa Waziri Mkuu ndiye msaidizi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano katika masuala yote yanayohusu upande wa Tanzania Bara, kwa kofia ya Makamu wa Pili wa Rais; na ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa kofia ya Waziri Mkuu. Katiba hii pia ilifuta mfumo wa vyama vingi vya siasa na kubaki na vyama viwili: *Tanganyika African National Union* (TANU) kwa upande wa Tanzania Bara na *Afro-Shiraz Party* (ASP) kwa upande wa Zanzibar ambavyo tarehe 5 Februari, 1977 viliungana na kuanzisha Chama Cha Mapinduzi (CCM). Muundo wa Bunge chini ya Katiba hii uliendelea kuwa na sehemu mbili ambazo ni Rais wa Tanganyika na Wabunge; na pia Ibara ya 49 ilielezea majukumu ya Bunge kuwa ni kutunga sheria kwa masuala ya Muungano na ya Tanzania Bara.

Aidha, Toleo la 1972, Ibara ya 24 (1) iliainisha aina zifuatazo za Wabunge:- Wabunge mia moja na ishirini wa kuchaguliwa, Wabunge kumi na tano waliochaguliwa na Bunge kutoka katika taasisi na Jumuiya za Chama, Wakuu wa Mikoa kumi na nane kutoka Tanzania Bara na watano kutoka Zanzibar, Wabunge wasiozidi thelathini na mbili walioteuliwa na Rais wa Zanzibar kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, Wabunge wasiozidi ishirini kutoka Zanzibar na wasiozidi kumi kutoka Tanzania Bara walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Ibara ya 27(1) ilitamka sifa mbili za mtu kuwa Mbunge ambazo ni:- kutimiza umri wa miaka ishirini na moja na kuwa mwanachama wa TANU au ASP.

Toleo la mwaka 1973 na 1976, Ibara ya 45 (1) na Ibara ya 24 (1) zilitaja Kamati zifuatazo:- Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Mambo ya Siasa, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali, Kamati ya Mambo ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii, Kamati ya Kanuni za Bunge na Kamati ya Mambo Mengineyo. Aidha, Bunge lilipewa mamlaka ya kuunda Kamati nyingine za namna mbalimbali kadri litakavyoona inafaa.

**Katiba ya Kudumu ya Mwaka 1977**




Baada ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi, Kamati ya watu ishirini ambayo iliandaa Katiba ya CCM ilipewa pia jukumu la kuandaa mapendekezo ya Katiba ya Kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya mapendekezo ya Kamati hiyo kukamilika yaliwasilishwa Serikalini kwa ajili ya uandishi wa Katiba yenyewe. Kwa mujibu wa Pius Msekwa ambaye alikuwa mmoja wa Wajumbe wa Kamati hiyo, Mwandishi Mkuu wa Sheria wakati huo, George Liundi ambaye alipewa jukumu la uandishi, ndiye alipendekeza Katiba hiyo iandikwe kwa lugha ya Kiswahili. Kamati hiyo ilikuwa na Wajumbe kumi (10) kutoka Tanzania Bara na Wajumbe kumi (10) kutoka Zanzibar ambao ni:-

**Kutoka Tanzania Bara**: Lawi Sijaona, Peter Kisumo, Ngombale-Mwiru, Peter Siyovelwa, Pius Msekwa, Jackson Kaaya, Basheik Mikidadi, Beatrice Muhango, Nicodemus Banduka na David Mwakawago.

**Kutoka Zanzibar**: Thabit Kombo, Hassan Nasoro Moyo, Abdallah Natepe, Seif Bakari, Hamis Hemed, Rajab Heri, Ali Mzee, Asia Amour, Juma Salum na Hamdan Muhidin.




*Wajumbe walioshiriki kuandika Katiba ya Mwaka 1977*

Baada ya Kamati kukamilisha rasimu ya mapendekezo ya Katiba, Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar aliteua Wajumbe wa Bunge Maalum la Kutunga Katiba mpya (Constituent Assembly) ambao walikuwa ni Wabunge wale wale wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bunge hilo lilikutana Dar es Salaam tarehe 25 Aprili, 1977 na kupitisha Katiba katika muda wa saa nne. Katiba hii ilipitishwa ndani ya muda mfupi kwa kuwa wakati huo majukumu yote yalikuwa yakijadiliwa na kuamuliwa ndani ya Vikao vya CCM na Bunge lilikuwa na

kazi ya kurasimisha kwa lengo la kukidhi matakwa ya kisheria.

Mambo ya msingi yaliyokuwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ni pamoja na kutamka kuwa: Bunge litakuwa na sehemu mbili, yaani Rais na Wabunge, Chama Cha Mapinduzi kuwa na mamlaka ya mwisho, haki ya kupiga kura kwa kila mwanachi mwenye sifa, na kuunganisha nyadhifa za Serikali na Chama. Aidha, kutokana na chama kupewa mamlaka ya mwisho ya kuamua, Serikali ilibaki na jukumu la kutekeleza maamuzi ya chama na Bunge kutunga Sheria ili kuwezesha utekelezaji huo. Mfumo wa chama kushika hatamu uliendelea hadi mwaka 1992 ambapo mfumo wa vyama vingi vya siasa ulirejeshwa.

Aidha, masuala mengine yaliyohusiana na Bunge katika Katiba hiyo ni kwamba:- Ibara ya 50 ililipa Bunge majukumu ya kutunga sheria juu ya mambo yote ya Muungano. Ibara ya 54 (1) ilielekeza kuwa Bunge ni Kamati ya Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM ambayo kazi yake ilikuwa ni kusimamia kwa ujumla utekelezaji wa siasa ya chama unaofanywa na Serikali pamoja na mashirika ya umma.

Ibara ya 23 (1) ilitaja aina za Wabunge kuwa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Wabunge mia moja na sita waliowakilisha Wilaya za Uchaguzi, Wabunge wa Taifa kumi na tano waliochaguliwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 29, Wabunge wa Taifa ishirini na tano waliochaguliwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya Ibara

ya 30, Wakuu wa Mikoa, Wabunge wasiozidi thelathini na mbili waliochaguliwa na Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Wabunge wasiozidi ishirini kutoka Zanzibar walioteuliwa na Rais wa Zanzibar na Wabunge wasiozidi kumi walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ibara ya 26 (1) ilibainisha sifa za kuwa Mbunge ambazo ni raia wa Jamhuri ya Muungano aliyetimiza umri wa miaka ishirini na moja, mwanachama anayezingatia masharti ya Katiba ya chama, mtu aliyetosheka na asiye na tamaa, aliyependa kueneza matunda ya uhuru kwa wananchi wote kwa manufaa yao na maendeleo ya taifa kwa ujumla, na ambaye hakuzuiliwa kugombea uchaguzi kwa mujibu wa katiba hiyo. Vilevile, Ibara ya 47 (1) iliendelea kuzitambua Kamati za Bunge zilizokuwepo kwenye Katiba ya Muda ya mwaka 1965.

**Mabadiliko ya Katiba ya Kudumu ya Mwaka 1977**

Katiba ya mwaka 1977 imefanyiwa mabadiliko mara kumi na nne hadi sasa. Kati ya mabadiliko hayo, yaliyohusiana na Bunge moja kwa moja ni:-

**Mabadiliko ya Tatu, mwaka 1980**

Mabadiliko hayo yalilenga kubadilisha idadi ya Wabunge wanaowakilisha wilaya za uchaguzi ili idadi yao iendane na idadi ya wilaya mpya za uchaguzi. Hii ni kwa sababu kila wilaya ilikuwa ni jimbo la uchaguzi, hivyo idadi ya wilaya ilipoongezeka na idadi ya Wabunge iliongezeka.

**Mabadiliko ya Tano, Mwaka 1984**

Mabadiliko haya yalilenga kuongeza idadi ya Wabunge wanawake na Kamati za Bunge. Ibara ya 66 ilitaja aina za Wabunge kuwa ni waliochaguliwa kuwakilisha wilaya za uchaguzi za Mbunge mmoja, Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha wilaya za uchaguzi za Wabunge wengi, Wabunge wanawake kumi na tano waliochaguliwa na Bunge kutokana na mapendekezo ya Jumuiya ya Wanawake wa Tanzania, miongoni mwao angalau watano kutoka Tanzania Bara na watano kutoka Zanzibar. Wengine ni Wabunge watano waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi kutoka miongoni mwa wajumbe wake, Wabunge wa taifa kumi na tano waliochaguliwa na Bunge kutokana na mapendekezo ya Jumuiya za chama, Wabunge kumi na tano walioteuliwa na Rais, miongoni mwao, angalau watano kutoka Tanzania Bara na watano kutoka Zanzibar na Wakuu wa mikoa.

Aidha, Ibara hii ilikusudia kuongeza idadi ya Wabunge wanawake kumi na tano waliochaguliwa na Bunge kutoka miongoni mwa watu waliopendekezwa na Jumuiya ya Wanawake wa Tanzania. Toleo hili la Katiba liliendelea kuzitambua Kamati zilizotajwa katika matoleo yaliyopita isipokuwa Ibara ya 96(1) iliongeza Kamati nne ambazo ni Kamati ya Uongozi, Kamati ya Mambo ya Katiba na Sheria, Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, na Kamati ya Mashirika ya Umma.

**Mabadiliko ya Sita, Mwaka 1990**

Mabadiliko haya yalianzisha mfumo mpya wa uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Aidha, mabadiliko haya yaliliondoa Bunge na CCM kwenye shughuli zote zilizohusiana na masuala ya uchaguzi, ambapo kabla ya mabadiliko haya uchaguzi ulisimamiwa na CCM na kuratibiwa na Bunge.

**Mabadiliko ya Nane na Tisa, Mwaka 1992**

Mabadiliko ya Nane yalirejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa na kubadilisha utaratibu wa kuongeza idadi ya Wabunge wanawake kwa kuondoa idadi ya awali ya wanawake kumi na tano na kuweka asilimia kumi na tano ya Wabunge wote. Mabadiliko hayo pia yalimtambua Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Mbunge kutokana na wadhifa wake.

Aidha, mabadiliko ya tisa yaliweka utaratibu wa Bunge kumuondoa Waziri Mkuu madarakani kwa kura ya kutokuwa na imani naye. Hatua hii ililenga kulipa Bunge mamlaka zaidi ya kuisimamia Serikali.

**Mabadiliko ya Kumi na Tatu, Mwaka 2000**

Mabadiliko haya yalimpa Rais mamlaka ya kuteua watu wasiozidi kumi kuwa Wabunge. Aidha, yaliongeza idadi ya viti maalumu vya wanawake Bungeni kutoka asilimia kumi na tano hadi asilimia ishirini ya Wabunge wote.

Aidha, Ibara 67 (1) imeweka bayana kuwa moja ya sifa ya kuwa Mbunge ni kwamba, katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali.

**Mabadiliko ya Kumi na Nne, Mwaka 2005**

Mabadiliko haya yalilenga kuongeza idadi ya Wabunge wanawake na kuruhusu nafasi ya Spika kugombewa na asiye Mbunge. Ibara ya 66 (1) ilifafanua kuwa kati ya Wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi angalau wawili wawe wanawake. Aidha, ibara hiyo ilimpa Rais mamlaka ya kuteua Wabunge wasiozidi kumi, na miongoni mwao wasipungue wanawake watano. Vilevile, ibara hiyo iliongeza idadi ya Viti Maalum vya Wabunge wanawake kutoka asilimia ishirini hadi asilimia thelathini ya Wabunge wote. Mabadiliko hayo pia yalifafanua kuwa, Spika anaweza kuchaguliwa kutoka miongoni mwa watu wasio Wabunge.

**Sheria Mahususi za Uendeshaji wa Bunge**

Bunge kwa nyakati tofauti limekuwa likitunga Sheria mbalimbali kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya Sheria hizo ni:-

**Sheria ya Tanganyika (*Legislative Council*) *Order-in-Council* ya mwaka 1926**

Sheria hii ilianzisha Baraza la Kutunga Sheria kwa upande wa Tanganyika, [*Legislative Council of Tanganyika (LEGCO)*] mwaka 1926 ambayo iliainisha muundo na namna ya utendaji wa Baraza hilo.

**Sheria ya Baraza la Kutunga Sheria (Madaraka na Haki) SURA 359**

Sheria hii ya Baraza la Kutunga Sheria(Madaraka na Haki) SURA 359[The Legislative Council (Powers and Privileges) Ordinance CAP.359] iliweka kinga na haki za Baraza la Kutunga Sheria. Sheria hiyo iliendelea kutumika hadi mwaka 1988 ilipofutwa na Sheria nyingine mpya inayoitwa Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ya mwaka 1988 ambayo inatumika hadi sasa.

**Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge SURA 296**

Sheria hii ya Kinga Madaraka na Haki za Bunge SURA 296 [The Parliamentary Immunities, Powers and Priviledges Act, CAP. 296] ilitungwa kwa madhumuni ya kutekeleza matakwa ya Ibara ya 101 ya Katiba yanayohusu uhuru wa kutoa mawazo. Sheria hii imetaja masuala mbalimbali kama, haki na uhuru kamili wa majadiliano na kutoa maoni; kinga dhidi ya mashtaka kwa mambo yanayosemwa Bungeni; uhuru wa kuandaa na kuhutubia mikutano ya hadhara; na pia haki ya Bunge kutilia mkazo haki zake ambazo siyo makosa ya jinai.

**Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge ya mwaka 1997**

Kutokana na kuanza kwa uwakilishi wa vyama vingi Bungeni mwaka 1995, ambao ulisababisha mabadiliko mengine katika miundo ya uendeshaji na utendaji katika vyombo vya umma na taasisi za Serikali, Bunge lilitunga Sheria hii ya Tume ya Huduma za Bunge ya mwaka 1997(The Parliamentary Service Commission Act, 1997) kwa ajili ya kuanzisha chombo maalum cha kuimarisha

utendaji wa Bunge hususani katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Bajeti ya Bunge, maslahi ya Wabunge na utumishi katika Ofisi ya Bunge. Hivyo, Sheria hiyo ilitungwa ili kwenda sambamba na mabadiliko ya mfumo huo.

**Sheria ya Uendeshaji wa Bunge SURA 115**

Sheria hii ya Uendeshaji wa Bunge SURA 115 [The National Assembly (Adminstration) Act, CAP. 115] ilitungwa na kufuta Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge ya mwaka 1997 kwa lengo la kuweka utaratibu bora zaidi utakaoiwezesha Sekretarieti ya Bunge kutoa huduma kwa Wabunge, kuunda Tume ya Bunge pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Bunge.

**Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo SURA 96**


Sheria hii ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo SURA 96 [The Constituencies Development Catalyst Fund Act, CAP. 96] ilitungwa kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kusimamia na kuratibu miradi ya maendeleo itakayoanzishwa na wananchi wenyewe katika majimbo ya uchaguzi na hivyo kuhamasisha maendeleo ya majimbo hayo kwa Serikali kuchangia fedha moja kwa moja chini ya usimamizi wa Mbunge wa jimbo husika.

**Sheria ya Bajeti SURA 439**

Madhumuni ya kutunga Sheria ya Bajeti SURA 439 [The Budget Act, CAP. 439] ni kuweka mfumo bora wa

kiutendaji kati yaSerikali, Bunge na vyombo mbalimbali vinavyohusika katika mchakato wa Bajeti ya Serikali, kwa kuzingatia mipango, mapato na matumizi ya Serikali. Sheria hii imetambua majukumu ya Kamati ya Bunge ya Bajeti inayohusika na masuala ya Bajeti pamoja na majukumu ya Ofisi ya Bajeti ya Bunge (ambayo kwa sasa ni Idara ya Bajeti ya Bunge).

**Kanuni za Kudumu za Bunge**




Kanuni za Bunge ni mwongozo wa namna shughuli mbalimbali za Bunge zinavyopaswa kuendeshwa katika vikao vya Bunge pamoja na Kamati zake. Kihistoria, Sheria iliyoanzisha Baraza la Kutunga Sheria ya mwaka 1926 [Tanganyika (Legislative Council) Order in Council, 1926] ilimpa uwezo Gavana kwa kushauriana na Baraza hilo kutunga na kurekebisha Kanuni ili kuweka utaratibu bora wa uendeshaji wa shughuli za Baraza.

Aidha, kwa mujibu wa Katiba ya Tanganyika ya mwaka 1961, Bunge liliendelea kutunga kanuni zake zilizojulikana kama Kanuni za Bunge za mwaka 1961 zilizokuwa katika lugha ya Kiingereza. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, Bunge chini ya Katiba ya mpito ya mwaka 1965, lilitunga Kanuni mpya za mwaka 1965 kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili na kufuta Kanuni za mwaka 1961.

Katiba ya kudumu ya mwaka 1977 chini ya Ibara ya 89(1) iliendelea kutoa mamlaka kwa Bunge kutunga Kanuni, ambapo mwaka 1987 lilitunga upya Kanuni ambazo ziliendelea kufanyiwa marekebisho na kutolewa katika matoleo mbalimbali. Aidha, Kanuni hizo zilifutwa na Kanuni za Toleo la mwaka 1994 wakati nchi inaelekea kwenye uchaguzi wa mfumo wa vyama vingi vya siasa. Kanuni hizo zimeendelea kufanyiwa maboresho mbalimbali na kuchapwa upya katika matoleo tofauti ili kuweka utaratibu bora wa uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, Kanuni za Kudumu za Bunge zinazotumika kwa sasa ni Toleo la Februari mwaka 2023.

# SURA YA TATU

## UONGOZI WA BUNGE

### Utangulizi

Sura hii inaelezea dhana ya uongozi wa Bunge kama Taasisi, ambapo kwa mujibu wa Katiba, Spika wa Bunge ndiye kiongozi mkuu na pia Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Bunge, akisaidiwa na Naibu Spika. Hali kadhalika, Katibu wa Bunge ndiye kiongozi mkuu wa Sekretarieti ya Bunge, ambaye pia ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Bunge, Afisa Masuhuli na Mwenyekiti wa Menejimenti ya Bunge. Aidha, Waziri Mkuu ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ambaye anasimamia uwajibikaji wa Mawaziri Bungeni. Kwa upande mwingine, Kiongozi wa Upinzani Bungeni ndiye kiongozi wa Mawaziri Vivuli Bungeni.

### Spika

Jina Spika limetoholewa kutoka neno "*Speaker*" lenye asili ya lugha ya kiingereza. Baada ya Bunge kuanza rasmi kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zake kuanzia mwaka 1963, Spika pia aliitwa "Khatibu" ambalo ni neno lililoazimwa kutoka katika lugha ya kiarabu likimaanisha "msemaji".

Tangu kuundwa kwa Baraza la Kutunga Sheria, vikao vilikuwa vikiongozwa na Mwenyekiti ambaye alikuwa ni

Gavana. Nafasi ya Mwenyekiti ilibadilika na kuwa Spika na kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Novemba, 1953 siku ambayo **Brigedia William Erick Halstead Scupham**, raia wa Uingereza aliapishwa kuwa Spika wa kwanza na aliitumikia nafasi hiyo hadi tarehe 30 Aprili, 1958. Spika Scupham alifuatiwa na **Barclay Nihill** aliyetumikia nafasi hiyo kuanzia tarehe 1 Mei, 1958 hadi tarehe 31 Desemba, 1959. Mtiririko wa Viongozi wa Bunge katika nafasi ya Uspika baada ya uhuru wa Tanganyika hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

**Abdulkarim Yusufali Alibbai Karimjee (1959 - 1962)**



Alikuwa Spika wa kwanza mzawa mwenye asili ya ki-Asia katika Baraza la Kutunga Sheria kuanzia mwaka 1959 hadi mwaka 1962. Alishika nafasi hiyo kutoka kipindi cha ukoloni hadi mwanzoni mwa Tanganyika huru. Alizaliwa mwaka 1906 na kufariki mwaka 1977. Karimjee alitoka katika familia ya wafanyabiashara iliyokuwa na shughuli zake Tanganyika. Alianza harakati za siasa katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambapo kati ya mwaka 1952 na 1956 alishika nafasi ya Naibu Meya, na mwaka 1951, 1954 na 1957 alihudumu kama Meya wa Jiji hilo. Aidha, kumbukumbu zinaonesha kuwa akiwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam aliiomba familia yake kujenga ukumbi kwa ajili ya vikao vya Halmashauri ya Jiji hilo uliopewa jina la Karimjee. Ukumbi huo ndio uliotumika kwa ajili ya vikao vya Bunge.

**Chifu Adam Sapi Mkwawa (1962 - 1973; 1975 - 1994)**



Alikuwa Spika wa pili wa Bunge la Tanganyika na Spika wa kwanza wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye asili ya kiafrika. Alizaliwa tarehe 16 Juni, 1920, Iringa na kufariki tarehe 25 Juni, 1999. Alihitimu elimu ya Chuo Kikuu katika Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala, Uganda mwaka 1940. Chifu Mkwawa alijulikana kama Mtwa (Chifu) Sapi na alikuwa Mwafrika wa kwanza nchini kupewa cheo cha heshima cha Kapteni wa Jeshi la Wakoloni wa Uingereza la ***King's African Rifles*** (KAR). Alishika wadhifa wa Uspika katika vipindi viwili tofauti: 1962 hadi 1973; na 1975 hadi 1994 na ndiye Spika aliyeshikilia nafasi hiyo kwa muda mrefu zaidi (miaka 28). Katika kipindi cha mwaka 1973 hadi 1975 aliteuliwa kuwa Waziri wa Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma. Sehemu kubwa ya mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika, Katiba ya Mpito na Katiba ya Kudumu yalifanyika wakati wa uongozi wake.

**Chifu Erasto Andrew Mbwana Mang'enya (1973 - 1975)**



Alikuwa Spika wa tatu wa Bunge la Tanganyika na Spika wa pili wa Bunge la Tanzania kuanzia mwaka 1973 hadi mwaka 1975. Alizaliwa tarehe 17 Aprili, 1915, Muheza, Tanga. Alijulikana kama Mtema (Chifu) wa Wabondei kutoka Milima ya Usambara Kaskazini

- Mashariki mwa Tanzania. Alitunukiwa Shahada kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala, Uganda. Aliingia Bungeni mwaka 1960 ambapo mwaka 1962 aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Nishati na Ujenzi. Mwaka 1963 hadi mwaka 1964 alihamishiwa Wizara ya Mambo ya Nje, na alipelekwa New York, Marekani kama Balozi wa Kudumu wa Tanganyika kwenye Umoja wa Mataifa. Mwaka 1964 hadi mwaka 1965 alikuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii na Utamaduni wa Taifa. Aidha, mwaka 1965 alikuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi ya Tanzania (*Ombudsman*), na mwaka 1970 aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la kusikiliza Rufaa juu ya Majengo yaliyotaifishwa kutokana na Azimio la Arusha mwaka 1967.

**Pius Msekwa (1994 - 2005)**



Alikuwa Spika wa nne wa Bunge la Tanzania na Spika wa kwanza katika Bunge la vyama vingi vya siasa kuanzia mwaka 1994 hadi mwaka 2005. Alizaliwa tarehe 9 Juni, 1935 Ukerewe, Mwanza. Alikuwa Mbunge wa Jimbo la Ukerewe kuanzia mwaka 1990 hadi mwaka 2000. Ana Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Siasa aliyohitimu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1974, Shahada ya Sanaa katika Historia kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda, mwaka 1960 na Shahada ya Sheria kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Katibu wa Bunge (1962 - 1969), Katibu wa Chama cha TANU (1967 - 1970),

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (1970), Mwenyekiti wa Tume ya Ukaguzi wa Mfumo wa Mahakama (1974), Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (1977), Kamishna wa Mikoa ya Kilimanjaro na Tabora (1981 - 1984), Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (1984 - 1989), Naibu Spika (1991- 1994). Pamoja na nafasi za uongozi alizotumikia, kupitia nafasi yake ya Spika wa Bunge, aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA) kati ya mwaka 1996 hadi mwaka 1999. Kwa sasa ni Katibu wa Baraza la Viongozi wastaafu wa Chama Cha Mapinduzi na mwandishi wa vitabu. Chini ya uongozi wake Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge ya mwaka 1997 ilitungwa.

**Samuel John Sitta (2005 - 2010)**



Alikuwa Spika wa tano wa Bunge la Tanzania, aliyeongoza Bunge la Tisa kwa kauli mbiu ya "Kasi na Viwango" kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2010. Alizaliwa tarehe 18 Desemba, 1942, Urambo, Tabora na alifariki tarehe 7 Novemba, 2016. Alitunukiwa Shahada ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mwaka 1971 na Stashahada ya Usimamizi wa Biashara aliyohitimu kutoka Chuo Kikuu cha IMEDE, Uswisi mwaka 1976. Aliingia Bungeni mwaka 1975 na kutumikia hadi mwaka 1995. Alirudi tena Bungeni mwaka 2005 kupitia jimbo la Urambo Mashariki, Tabora na kuliwakilisha hadi mwaka 2015. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Mkurugenzi wa Utawala

wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) (1969 - 1975), Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) (1995 - 2005), Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki (2010 - 2015), Waziri wa Uchukuzi mwaka 2015 na Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2014). Chini ya uongozi wake Sheria ya uendeshaji Bunge ya Mwaka 2008 na Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ya Mwaka 2009 zilitungwa. Aidha, alisimamia marekebisho makubwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge mwaka 2007.

**Anne Semamba Makinda (2010 - 2015)**



Alikuwa Spika wa sita na mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo na aliyeongoza Bunge la Kumi kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2015. Alizaliwa tarehe 15 Julai, 1949 katika mkoa wa Iringa (Njombe). Ana Stashahada ya Juu ya Uhasibu kutoka Chuo cha Maendeleo Mzumbe (Chuo Kikuu cha Mzumbe) aliyohitimu mwaka 1975. Alikuwa Mbunge katika Bunge la Tanzania kwa miaka arobaini tangu mwaka 1975 hadi mwaka 2015 kupitia aina mbalimbali za ubunge ikiwemo uwakilishi wa vijana na jimbo la Njombe Kusini. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Uratibu na Muungano (1983 - 1990), Waziri wa Maendeleo ya Jamii Wanawake na Watoto (1990 -1995), Mwenyekiti wa Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Utalii (2000 - 2005),

Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanawake Tanzania (2000 - 2010) na Naibu Spika (2005 - 2010) akiwa pia Mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo.

Katika nyanja za kimataifa alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Kibunge la Nchi za Jumiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC Parliamentary Forum) (2000 - 2010). Akiwa Naibu Spika na Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Kibunge la SADC (2008 - 2010) aliongoza ushawishi wa ongezeko la nafasi za uwakilishi wa wabunge wanawake hadi kufikia asilimia 30 katika nchi za Botswana, Malawi, Msumbiji na Zambia. Akiwa Spika amekuwa Rais wa SADC PF (2014 – 2015) na Mwenyekiti wa CPA Kanda ya Afrika mwaka 2014. Vilevile, amewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na Mwenyekiti wa Bodi mbalimbali. Alisimamia mabadiliko ya mfumo wa bajeti (budget cycle) kwa maana ya Aprili hadi Juni badala ya Juni hadi Agosti kama ilivyokuwa awali ili kutoa nafasi kwa Wabunge kujadili, kuchangia na kufanya maridhiano kwenye maeneo yenye kipaumbele.

**Job Yustino Ndugai (2015 – 2022)**



Alikuwa ni Spika wa saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyeongoza Bunge la Kumi na Moja kuanzia mwaka 2015 hadi 2020; na Spika wa Bunge la Kumi na Mbili kuanzia Novemba 2020-2022. Alizaliwa tarehe 2 Januari, 1960 Kongwa, Dodoma. Aliingia Bungeni mwaka 2000 akiwa Mbunge wa jimbo la Kongwa. Ana Shahada ya Uzamili ya

Utawala wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha *Eastern and Southern African Management Institute* (ESAMI), aliyohitimu mwaka 2008, Shahada ya Uzamili ya Sayansi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway mwaka 1996, Stashahada ya Sayansi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway mwaka 1995, na Shahada ya Sayansi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 1993. Akiwa Bungeni ameshika nyadhifa mbalimbali zikiwemo:- Mwenyekiti wa Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira (2005 – 2010), Mwakilishi wa Afrika Mashariki kwenye Kamati ya Utendaji ya CPA (2010 - 2015), Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na Mazingira ya ACP/EU (2010 - 2015) na Mwenyekiti wa Maspika wa CPA Kanda ya Afrika (2019). Chini ya uongozi wake ameanzisha Bunge Mtandao, na utaratibu wa kuwagawia majoho Maspika wastaafu kama kumbukumbu ya utendaji wao katika Bunge. Amesimamia uanzishwaji wa Shule ya Sekondari ya Bunge ya Wasichana ya Mfano ya Kidato cha Tano na Sita inayozingatia mahitaji ya msingi ya jinsia iliyopo Kikombo, jijini Dodoma. Aidha, katika wakati wa uongozi wake miongoni mwa Sheria zilizotungwa na Bunge ni pamoja na Sheria ya Makao Makuu, Dodoma ya mwaka 2018, Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi ya mwaka 2017. Vile vile, alichagiza kuandikwa kwa Kitabu hiki cha Historia ya Bunge la Tanzania.

**Dkt. Tulia Ackson (2022 hadi Sasa)**



Ni Spika wa nane wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndiye Spika wa Bunge la kumi na mbili kuanzia Februari mwaka 2022 hadi sasa. Alizaliwa tarehe 23 Novemba, 1976, mkoani Mbeya.

Aliingia Bungeni mwaka 2015 akiwa ni Mbunge wa kuteuliwa na Rais na kuhudumu hadi mwaka 2020; na kuanzia Novemba, 2020, alichaguliwa kuwa Mbunge wa jimbo la Mbeya Mjini. Ana Shahada ya Uzamivu ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Cape Town, Afrika Kusini aliyohitimu mwaka 2007, Shahada ya Uzamili ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 2003 na Shahada ya Sheria aliyohitimu mwaka 2001 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Miongoni mwa kazi alizowahi kufanya na nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2004 - 2015), Mjumbe wa Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014 na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali (2015). Vilevile ndiye Rais wa thelathini na moja wa Umoja wa Mabunge duniani (IPU). Nafasi hiyo anaishikilia kuanzia Oktoba mwaka 2023 hadi sasa ambapo amekuwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika na wa tatu duniani kushika nafasi hiyo.

**Naibu Spika**

Kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 85 na Ibara ya 86, Naibu Spika ni nafasi inayotokana na kuchaguliwa katika Mkutano wa kwanza wa Bunge ambapo majukumu yake ni kumsaidia Spika katika kuliongoza Bunge kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Mtiririko wa Viongozi wa Bunge katika nafasi ya Naibu Spika ni kama ifuatavyo:-

**Abdulkarim Yusufali Alibbai Karimjee (1956 - 1957)**



Alikuwa mmoja kati ya Wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria ambaye alichaguliwa kuwa Naibu Spika tarehe 25 Aprili, 1956 na kutumikia wadhifa huo hadi mwaka 1957. Wasifu wake kwa undani upo kwenye kipengele cha Maspika.

**Chifu Haroun Msabila Lugusha (1958 - 1959)**



Alikuwa Naibu Spika wa kwanza mwenye asili ya kiafrika katika Baraza la Kutunga Sheria. Alizaliwa tarehe 20 Septemba, 1920, Sikonge, Tabora na kufariki mwaka 2001. Alikuwa na elimu ya Stashahada ya Kilimo ya Chuo Kikuu cha Makerere aliyoipata mwaka 1942. Alikuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria kuanzia mwaka 1953 hadi mwaka 1959 na baadaye Mjumbe wa Tume ya Huduma

za Serikali za Mitaa (Local Government Service Commission) katika kipindi cha mwaka 1962 hadi mwaka 1964. Aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Serikali za Mitaa kuanzia mwaka 1957 hadi mwaka 1959. Mwaka 1996 hadi mwaka 2000 alikuwa Mbunge wa Sikonge, Tabora.

**Erasto Andrew Mbwana Mang'enya (1960 - 1961; 1966 - 1973)**



Aliingia kwenye Baraza la Kutunga Sheria mwaka 1960 na kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Mwaka 1962 alichaguliwa kuwa Waziri Mdogo (Naibu Waziri) wa Mawasiliano, Nishati na Ujenzi (Communications, Power and Works) katika Serikali ya Tanganyika huru na baadaye alihamishiwa katika Wizara ya Mambo ya Nje na kupelekwa New York, Marekani kama Balozi wa kudumu wa Tanganyika katika Umoja wa Mataifa mwaka 1963 na kuhudumu hadi mwaka 1964. Wasifu wake kwa undani upo kwenye kipengele cha Maspika.

**Frank Mfundo (1962 - 1964)**



Alikuwa Naibu Spika chini ya uongozi wa Spika Chifu Adamu Sapi Mkwawa, ambapo alitumikia cheo chake kwa muda wa miaka miwili kutoka mwaka 1962 hadi 1964. Alikuwa Mbunge wa Handeni na Waziri Mdogo wa Elimu miaka ya 1960.

**Herman Elias Sarwatt (1964 - 1965)**



Alichaguliwa kuwa Naibu Spika tarehe 8 Septemba, 1964 chini ya uongozi wa Spika, Chifu Adam Sapi Mkwawa, nafasi aliyoitumikia hadi 1965. Alizaliwa tarehe 9 Mei, 1919, Mbulu, Arusha kwa wakati huo. Mwaka 1958, aligombea ubunge jimbo la Mbulu kama mgombea binafsi na kushinda. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki kabla ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977.

**Chifu Stanslaus Rugaba Kasusura (1973 - 1985)**



Alikuwa Naibu Spika chini ya Maspika wawili: Chifu Erasto Mang'enya na Chifu Adam Sapi Mkwawa kuanzia mwaka 1973 hadi mwaka 1985. Alizaliwa mwaka 1918 na kufariki mwaka 1996. Alikuwa Mbunge wa Biharamulo (1965 – 1975) na Mbunge wa Tabora Vijijini (1975 – 1980). Alikuwa Chifu wa Ussuvi Mashariki, Mkoa wa Kagera kuanzia Septemba, 1952 hadi Novemba, 1962. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Mkuu wa Wilaya: Biharamulo (1962 - 1963) na Shinyanga (1964 - 1965) na Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Usagaji la Taifa (National Milling Corparation).

**Austin Kapere Shaba (1986 - 1988)**



Alikuwa Naibu Spika kuanzia mwaka 1986 hadi mwaka 1988. Alizaliwa tarehe 12 Desemba, 1925, Sumbawanga, Rukwa na kufariki mwaka 1988. Alikuwa Mbunge kuanzia mwaka 1960 hadi mwaka 1968 akiwakilisha jimbo la Mtwara na kuchaguliwa kuwa Waziri wa Afya na Nyumba. Tarehe 5 Oktoba, 1968 alilazimika kujiuzulu nafasi zote za uongozi baada ya kuwepo utatanishi kuhusu uhalali wa uraia wake ingawa baadaye alipewa uraia wa Tanzania. Mwaka 1980 alichaguliwa tena kuwa Mbunge wa Mtwara Mjini nafasi iliyompa fursa mwaka 1986 kuchaguliwa kuwa Naibu Spika nafasi aliyoitumikia hadi mwaka 1988. Alikuwa na elimu ya afya kutoka Chuo cha Afya, Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 1947. Mwaka 1948, aliajiriwa kama Msaidizi wa Afya na baadaye kufanya kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Afisa Tawala na Balozi wa Tanganyika katika Umoja wa Mataifa (1962 – 1963). Aidha, alikuwa Waziri wa Serikali za Mitaa na Ujenzi (1963 - 1968).

**Balozi George Maige Nhigula (1988 - 1990)**



Alikuwa Naibu Spika kuanzia mwaka 1988 hadi mwaka 1990. Alizaliwa tarehe 3 Aprili, 1929 Kwimba, Mkoa wa Mwanza na kufariki mwaka 2011. Alikuwa Mbunge wa Jimbo la Kwimba kuanzia mwaka 1985 hadi mwaka

1995 alipostaafu rasmi. Alikuwa na elimu ya Shahada kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda aliyoipata mwaka 1956, na Stashahada ya Diplomasia ya Chuo cha Oxford, Uingereza aliyohitimu mwaka 1962. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Katibu Mkuu Wizara ya Kazi (1965 – 1967), Balozi Cairo, Misri (1968 - 1971), Balozi London (1971 – 1974), Balozi Japan (1974 – 1978) na Balozi India (1978 – 1980).

**Pius Msekwa (1990 - 1994)**



Alitumikia nafasi mbalimbali katika masuala ya kibunge na siasa katika nyakati tofauti. Mwaka 1990 alichaguliwa kushika nafasi ya Naibu Spika ambayo aliitumikia hadi mwaka 1994 chini ya uongozi wa Spika, Chifu Adam Sapi Mkwawa. Wasifu wake kwa undani upo kwenye sehemu ya Maspika.

**Mathias Kihaule (1994 - 1995)**



Alikuwa Naibu Spika kuanzia mwaka 1994 hadi mwaka 1995. Alizaliwa tarehe 16 Julai, 1933 katika kijiji cha Lugarawa, Wilaya ya Ludewa, Iringa (Njombe) na kufariki mwaka 2012.

Alikuwa Mbunge wa jimbo la Ludewa kuanzia mwaka 1980 hadi 1990. Alikuwa na Shahada ya Uzamili na Shahada ya Kwanza katika fani ya Elimu alizohitimu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Miongoni mwa kazi alizowahi kufanya ni pamoja na:-

Mwalimu wa *Middle Schools* (1958 – 1965) na Mhadhiri wa Chuo Kikuu (1970 -1971). Aidha, aliwahi kuwa Makamu Mkuu wa Chuo cha Ualimu, Mpwapwa mwaka 1975.

**Balozi Philip Sang'ka Marmo (1995 - 2000)**



Alikuwa Naibu Spika kuanzia mwaka 1995 hadi 2000. Alizaliwa tarehe 29 Desemba, 1951 Wilaya ya Mbulu, Mkoani Arusha (Manyara). Alikuwa Mbunge wa Mbulu kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka 2010. Ana Shahada ya Uzamili ya Uandishi wa Sheria kutoka Taasisi ya Sheria na Masuala ya Kimataifa ya Bangladesh (Bangladesh Institute of Law and International Affairs) na Shahada ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Wakili wa Serikali, Mwandishi wa Sheria Mwandamizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora mwaka 2006, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Uratibu na Bunge (2008 - 2010) na Balozi wa Tanzania katika nchi za China (2011 – 2013) na Ujerumani (2013 – 2017).

**Juma Jamaldin Akukweti (2000 - 2005)**



Alikuwa Naibu Spika kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2005. Alizaliwa tarehe 20 Septemba, 1947 Tunduru, Mkoa wa Ruvuma na kufariki mwaka 2007. Aliwahi kuwa Mbunge akiwakilisha Jimbo la Tunduru kuanzia mwaka 1990 na baadaye kuteuliwa kuwa Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu mwaka 2006 hadi alipofariki. Alikuwa na Shahada ya Sayansi ya Elimu kutoka chuo Kikuu cha Dar es salaam aliyohitimu mwaka 1975.

Miongoni mwa kazi alizowahi kufanya ni pamoja na:- Mkufunzi (1975 - 1977), Mshauri wa Wanafunzi, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (1977 – 1981), Meneja wa Utawala Taasisi ya Uvuvi Tanzania (1981 - 1989), Mratibu na Meneja wa Utawala Kampuni ya kuzalisha mafuta ya kupikia Morogoro (1989 -1990)

**Anne Semamba Makinda (2005 - 2010)**



Ni mwanasiasa mkongwe kwa takribani miaka arobaini na mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Naibu Spika kuanzia mwaka 2005 hadi 2010. Wasifu wake kwa undani upo kwenye sehemu ya Maspika.

**Job Yustino Ndugai (2010 - 2015)**



Alishika nafasi mbalimbali za masuala ya Bunge tangu alivyoingia Bungeni rasmi mwaka 2000. Pamoja na nafasi zingine, alichaguliwa kuwa Naibu Spika kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2015. Wasifu wake kwa undani upo kwenye sehemu ya Maspika.

**Dkt. Tulia Ackson (2015-2022)**



Ameshika nafasi mbalimbali za masuala ya Bunge tangu alivyoingia Bungeni mwaka 2015. Pamoja na nafasi zingine alichaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la kumi na moja kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2020 na Naibu Spika wa Bunge la Kumi na mbili kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2022 chini ya uongozi wa Spika Job Yustino Ndugai. Wasifu wake kwa undani upo kwenye sehemu ya Maspika.

**Mhe. Mussa Azzan Zungu (2022 hadi sasa)**



Ni mwanasiasa mkongwe kwa takribani miaka ishirini, na ndiye Naibu Spika wa Bunge la kumi na mbili kuanzia mwaka 2022 hadi sasa. Alizaliwa tarehe 25 Mei, mwaka 1952 mkoani Dar es salaam. Amekuwa Mbunge wa jimbo la Ilala tangu alipoingia Bungeni mwaka 2005 hadi sasa.

Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni, Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Kibunge cha nchi Jumuiya ya Madola kwa Tanzania(CPA), (2005-2010), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii (2015-2018), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Januari-Novemba 2020, Mwenyekti wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama (2018-2022), Mjumbe wa Tume ya Huduma za Bunge kuanzia 2016 hadi sasa. Ana stashahada ya masuala ya Uongozi kutoka Chuo cha Ulinzi cha Taifa Dar es saam aliyohitimu mwaka 2021, astashahada ya diplomasia kutoka chuo cha Uhusiano wa Kimataifa Cairo, Misri aliyohitimu mwaka 2007, na astashahada ya Uhandisi wa vyombo vya anga kutoka Chuo cha Kijeshi cha Anga Tanzania na Canada (1979-1982).

**Mwenyekiti wa Bunge**

Mwenyekiti wa Bunge ni Mbunge anayeongoza shughuli za Bunge kwa niaba ya Spika, ambaye huchaguliwa kutoka miongoni mwa Wenyeviti au Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Kabla ya kuanza kutambulika kama

Mwenyekiti wa Bunge, hapo awali alijulikana kama Msadizi wa Spika kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 1994.

Nafasi hiyo ilianza rasmi mwaka 1995 ambapo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 1995, kulikuwa na Wenyeviti wawili waliochaguliwa kutoka miongoni mwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge hadi mabadiliko ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya mwaka 2007, yalipoongeza nafasi moja na hivyo nafasi za wenyeviti kuwa tatu. Aidha, mabadiliko hayo yaliwezesha Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kuchaguliwa katika nafasi hiyo kwa kuzingatia jinsi na pande za Muungano.

**Tume ya Bunge**

Tume ya Bunge ndicho chombo kikuu katika uongozi wa Bunge kilichoanzishwa mwaka 1997 kwa Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge ya mwaka 1997; na baadae kutungwa kwa Sheria ya Uendeshaji wa Bunge, SURA Na. 115 ya mwaka 2008. Tume hii inaongozwa na Spika wa Bunge ambaye ni Mwenyekiti na Katibu wa Bunge ambaye ni Katibu wa Tume.

Majukumu yake ni kupanga na kupendekeza kwa Serikali bajeti kwa ajili ya Mfuko wa Bunge kwa kushauriana na Katibu wa Bunge:- inaajiri, kuthibitisha, kupandisha vyeo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa maofisa wa Bunge. Aidha, Tume inapanga vigezo na masharti ya utumishi wa Bunge, kuandaa na kupendekeza Serikalini viwango vya mishahara, posho na stahili zingine kwa ajili ya Wabunge na Watumishi wa Bunge na kutekeleza majukumu yoyote kwa mujibu wa Sheria.

**Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni**

Waziri Mkuu ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni ambaye husimamia shughuli zote za Serikali na uwajibikaji wa pamoja wa Mawaziri Bungeni. Wakati wa vikao vya Bunge, Waziri Mkuu asipokuwepo Bungeni kwa kipindi kinachozidi siku moja, humteua Waziri mwingine kuwa kiongozi wa muda wa Shughuli za Serikali Bungeni. Makamu wa Rais pia aliwahi kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ya mwaka 1962. Orodha ya Viongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia uhuru wa Tanganyika ni kama ifuatavyo:-

**Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (1961 - 1962)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Kwanza wa Serikali ya Tanganyika na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia mwaka 1961 hadi mwaka 1962, alipojiuzulu.

Alizaliwa tarehe 13 Aprili, 1922 katika Kijiji cha Butiama, Mkoani Mara na kufariki tarehe 14 Oktoba, 1999. Alikuwa Mbunge wa jimbo la Dar es Salaam kati ya mwaka 1961 hadi 1962. Alikuwa Rais wa kwanza wa Tanganyika huru na hivyo kubeba hadhi ya kuitwa "Baba wa Taifa" kwa kuongoza juhudi za kutafuta uhuru na ujenzi wa Taifa.

Ni kati ya viongozi wachache wa Afrika ambao wameacha madaraka kwa hiari baada ya kutawala kwa takribani miaka ishirini na nne Kabla ya kuingia kwenye siasa alikuwa ni mwalimu kazi ambayo ilimpatia jina alilotumia maisha yake yote.

**Rashid Mfaume Kawawa (1962, 1972 - 1977)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Pili wa Serikali ya Tanganyika na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, kuanzia tarehe 22 Januari, 1962 akipokea nafasi hiyo kutoka kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Alizaliwa tarehe 27 Februari, 1926, Namtumbo, Ruvuma na kufariki mwaka 2009. Aliwahi kuwa Mbunge wa jimbo la Nachingwea (1960 - 1965), Liwale (1975 - 1985) na Kuteuliwa (1985 - 1990). Jina la Kawawa ni miongoni mwa majina yasiyoweza kusahaulika katika ukombozi wa Tanganyika ambapo uzalendo, utendaji kazi na weledi wake ulimfanya ajulikane kama "**Simba wa Vita**". Alikuwa Makamu wa Pili wa Rais na Waziri wa Ulinzi na alishiriki kuanzishwa kwa Jeshi la Wananchi (JWTZ) wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) lakini pia kujenga misingi imara ya majeshi hayo.

**Edward Moringe Sokoine (1977 - 1980 na 1983 - 1984)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge wa jimbo la Masai mwaka 1965 hadi mwaka 1975, na Monduli mwaka 1975 hadi mwaka 1984. Alizaliwa tarehe 1 Agosti, 1938, Kijiji cha Emairete Monduli Juu, Arusha na kufariki mwaka 1984. Alikuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa awamu mbili, awamu ya kwanza kuanzia mwaka 1977 hadi mwaka 1980 na awamu ya pili kuanzia mwaka 1983 hadi 1984. Uongozi wake ulikuwa wa mfano kutokana na uadilifu, utendaji kazi na upigaji vita masuala ya rushwa na ubadhilifu wa mali ya umma.

**Cleopa David Msuya (1980-1983 na 1994 - 1995)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa jimbo la Mwanga, Kilimanjaro kati ya mwaka 1980 hadi mwaka 1985. Alizaliwa tarehe 4 Januari, 1931 Mwanga, Mkoani Kilimanjaro. Alikuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa awamu mbili: awamu ya kwanza (1980 - 1983) akiwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais, na awamu ya pili (1994 - 1995) akiwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Waziri wa Fedha (1972 – 1975 na 1983 – 1985), na Waziri wa Viwanda (1975 – 1980 na 1990 – 1994).

**Dkt. Salim Ahmed Salim (1984 - 1985)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia mwaka 1984 hadi mwaka 1985 akiwa Mbunge wa kuteuliwa (1980 - 1990). Alizaliwa tarehe 23 Januari, 1942, Zanzibar. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Naibu Waziri Mkuu na wakati huo akiwa Waziri wa Ulinzi (1986 – 1989), Balozi wa Tanzania katika nchi za: Cuba, Misri, India, China, Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Rais wa Kikao cha 34 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (1979) na Rais wa Mkutano wa Kimataifa kuhusu kuiwekea vikwazo Afrika Kusini (1981). Aidha, aliwahi kuwa Rais wa Mkutano wa Kimataifa wa Paris uliojadili ubaguzi wa rangi, Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Umoja wa Mataifa ya kuondoa ukoloni na Mjumbe Maalum wa Umoja wa Afrika katika mgogoro wa Darful. Sasa, Dkt. Salim ni Mwenyekiti wa Wakfu wa Mo-Ibrahimu (Mo-Ibrahimu Foundation) ambayo inatoa Tuzo ya Utawala Bora kwa marais wastaafu barani Afrika.

**Joseph Sinde Warioba (1985 - 1990)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Sita na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge wa kuteuliwa mwaka 1983 hadi mwaka 1990 na Mbunge wa Jimbo la Bunda mkoani Mara. Alizaliwa tarehe 3

Septemba, 1940 wilayani Bunda, Mwanza (Mara). Alikuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia mwaka 1985 hadi mwaka 1990. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Mwanasheria wa Serikali (1968 -1970), Wakili wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (1970), Mwanasheria Mkuu wa Serikali (1976 - 1983), Waziri wa Sheria (1983 – 1985), Jaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Sheria za Bahari (1996 - 1999), Mwenyekiti wa Tume ya Rais Dhidi ya masuala ya Rushwa Serikalini na Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba (2012 - 2014).

**John Samwel Malecela (1990 - 1994)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Saba na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Alikuwa Mbunge wa Kuteuliwa mwaka 1972 hadi 1984, na wa jimbo la Mtera mwaka 1995 hadi mwaka 2010. Alizaliwa tarehe 10 Aprili, 1934 Mvumi, mkoani Dodoma.

Alikuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia mwaka 1990 hadi 1994. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:-Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania, Umoja wa Mataifa (1964 - 1968), Waziri wa Mambo ya Nje (1972 – 1973), Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji (1973 – 1974), Waziri wa Maliasili na Kilimo (1975), Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (1975 – 1976), Waziri wa Utamaduni, Chakula na Usalama (1975 - 1980), Mkuu wa Mkoa wa Iringa (1980 –1984), Balozi wa Tanzania katika nchi ya Ethiopia na OAU (1967 – 1969) na Uingereza (1989 - 1990) na Makamu Mwenyekiti wa CCM (1995 - 2007)

**Frederick Tluway Sumaye (1995 - 2005)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Nane wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa jimbo la Hanang, Arusha (Manyara) mwaka 1983 hadi mwaka 2005. Alizaliwa tarehe 29 Mei, 1950 Wilaya ya Hanang mkoa wa Arusha (Manyara). Alikuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia mwaka 1995 hadi 2005. Miongoni mwa nafasi alizoshika ni pamoja na:- Waziri wa Kilimo, Mifugo na Ushirika na Balozi wa Heshima katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda.

**Edward Ngoyai Lowassa (2005 - 2008)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Tisa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge wa Taifa mwaka 1985 hadi mwaka 1995 na Mbunge wa Jimbo la Monduli mwaka 1995 hadi mwaka 2015. Alizaliwa tarehe 26 Agosti, 1953 Wilaya ya Monduli, Arusha na kufariki mwaka 2024. Alikuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2008. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:-Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mahakama na Masuala ya Bunge (1990 - 1993), Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi (1993 - 1995), Waziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mazingira na Kuondoa Umasikini (1997 - 2000) na Waziri wa Maji (2000 - 2005).

**Mizengo Kayanza Peter Pinda (2008 - 2015)**



Alikuwa Waziri Mkuu wa Kumi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa jimbo la Mpanda Mashariki (2000 – 2015), Rukwa (Katavi). Alizaliwa tarehe 12 Agosti, 1948 Mpanda Vijijini, mkoani Rukwa. Alikuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia mwaka 2008 hadi mwaka 2015. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Wakili wa Serikali katika Wizara ya Katiba na Sheria, Msaidizi wa Katibu wa Baraza la Mawaziri (1996 – 2000), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (2000 – 2006) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (2006 – 2008).

**Kassim Majaliwa Majaliwa (2015 – hadi sasa)**



Ni Waziri Mkuu wa Kumi na Moja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa jimbo la Ruangwa, Lindi kuanzia mwaka 2010 hadi sasa. Alizaliwa tarehe 22 Desemba, 1960, Ruangwa mkoa wa Lindi. Amekuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia mwaka 2015. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Mkuu wa Wilaya Urambo, Tabora na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa (Elimu) (2010 – 2015).

## Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni

Kiongozi wa Upinzani Bungeni ni Mbunge anayechaguliwa na Wabunge wanaounda Kambi ya Upinzani ili kuwa Kiongozi wa Kambi hiyo na msimamizi wa Mawaziri Vivuli Bungeni. Nafasi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, ilianza mwaka 1995 baada ya uwepo wa uwakilishi wa vyama vingi Bungeni. Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 1995, kiongozi huyo alitokana na chama kilichokuwa na idadi ya Wabunge wasiopungua 30.

Baada ya mabadiliko kadhaa ya Kanuni za Kudumu za Bunge hadi kufikia Toleo la mwaka 2016, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, alitokana na Wabunge wote wa Upinzani ambao idadi yao si chini ya asilimia kumi na mbili na nusu ya Wabunge wote. Aidha, inapotokea vyama viwili au zaidi vyenye idadi sawa ya Wabunge ambao ni zaidi ya asilimia kumi na mbili na nusu, Wabunge wa Vyama vinavyohusika huchagua Kiongozi wa Kambi ya Upinzani chini ya utaratibu watakaokubaliana.

Aidha, Toleo la mwaka 2020, Kanuni ya 21 imeweka mabadiliko kuhusu Kambi ya Upinzani Bungeni ambapo kwa sasa inatambulika kama Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni. Kwa mujibu wa Kanuni ya 22 ya toleo hilo, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni anachaguliwa kama ilivyokuwa kwenye Kanuni ya 14 ya Toleo la mwaka 2016. Bunge la Kumi na Mbili halina Kiongozi wa Kambi ya Walio Wachache Bungeni kwa

kutokukidhi matakwa ya Kanuni ya 22 ya Toleo la mwaka 2020.


Orodha ya Viongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni baada ya utaratibu wa vyama vingi hadi Bunge la Kumi na Moja ni kama ifuatavyo:-

**Fatma Maghimbi (1995 – 2000)**



Alikuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika Bunge la Saba lililoanza mwaka 1995 hadi mwaka 2000 kupitia CUF. Alizaliwa tarehe 10 Desemba, 1946 Pemba. Alikuwa Mbunge wa Chakechake, Pemba (1995 - 2000). Alirejea Bungeni katika Bunge la Tisa (2005 - 2010) kupitia jimbo hilo ambapo aliteuliwa kuwa Waziri Kivuli wa Sheria, Katiba na Utawala Bora.

**Dkt. Amani W. A. Kabourou (2000 – 2003)**



Alikuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika Bunge la Nane kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2003 kupitia CHADEMA. Alizaliwa tarehe 23 Mei, 1949 Kigoma na kufariki mwaka 2018. Alikuwa Mbunge kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka 2005 akiwakilisha jimbo la Kigoma Mjini. Aidha, akiwa mwanachama wa CCM, alichaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka 2012.

**Wilfred M. Lwakatare (2003 – 2005)**



Alikuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika Bunge la Nane kuanzia mwaka 2003 hadi mwaka 2005 kupitia CUF. Alizaliwa tarehe 4 Januari, 1962, Kibeta, Bukoba Mjini. Alikuwa Mbunge wa jimbo la Bukoba Mjini kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2005. Alirejea Bungeni kupitia CHADEMA mwaka 2015 akiwakilisha jimbo hilo ambapo aliteuliwa kuwa Waziri Kivuli wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

**Hamad Rashid Mohamed (2005 – 2010)**



Alikuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika Bunge la Tisa kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2010 kupitia CUF. Alizaliwa tarehe 1 Machi, 1950 Zanzibar. Ni miongoni mwa wanasiasa wakongwe aliyeingia Bungeni toka miaka ya 1970 kupitia aina mbalimbali za ubunge. Mwaka 2001 hadi mwaka 2005 alikuwa Mbunge wa kuteuliwa. Aidha, alirejea Bungeni akiwakilisha jimbo la Wete, Zanzibar kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2015, kupitia CUF. Aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Zanzibar akiwa pia ni kiongozi wa chama cha *Alliance for Democratic Change*.

**Freeman Aikael Mbowe (2010 - 2020)**



Alikuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika Bunge la Kumi kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2015; na Bunge la Kumi Moja kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2020 kupitia CHADEMA. Alizaliwa 14 Septemba, 1961 Hai, Moshi. Alikuwa Mbunge akiwakilisha jimbo la Hai kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2005. Alirejea Bungeni mwaka 2010 akiwakilisha tena jimbo hilo hadi mwaka 2020.

**Katibu wa Bunge**

Kwa mujibu Ibara ya 87 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katibu wa Bunge ndiye Mtendaji Mkuu wa Bunge, ambaye huteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye madaraka ya juu katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, Sheria ya Utawala wa Bunge ya mwaka 2008, inatoa nafasi kwa Tume ya Utumishi wa Bunge kupendekeza majina matatu kutoka miongoni mwa Watumishi wa Bunge kwa Rais ili aweze kuteua Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge husaidiwa na Sekretarieti ya Bunge kutekeleza majukumu yake. Orodha ya Makatibu wa Bunge tangu uhuru hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

**Geoffrey William Young Hucks (1960 - 1962)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge mwaka 1960 na kuhudumu hadi mwaka 1962. Alizaliwa tarehe 30 Disemba, 1906, Potters Bar, Middlesex, Uingereza na alifariki mwaka 2002. Alikuwa


Mtumishi katika Serikali ya Kikoloni, Tanganyika. Aliongoza kipindi cha mpito kutoka Baraza la Kutunga Sheria hadi Baraza la Taifa baada ya uhuru wa Tanganyika. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kamishina wa Jimbo la Nyanda za Juu Kusini na Msimamizi wa Kwanza wa Uchaguzi Mkuu wa Tanganyika mwaka 1962.

**Pius Msekwa (1962 - 1970)**



Katibu wa Kwanza wa Bunge mwenye asili ya kiafrika ambaye aliteuliwa mwaka 1962 na kuhudumu hadi mwaka 1970. Kabla ya kushika nafasi hiyo, alifanya kazi kama Katibu Msaidizi wa Bunge chini ya uongozi wa Geoffrey Hucks. Wasifu wake kwa undani upo kwenye sehemu ya Maspika.

**Yassin Osman (1970 - 1974)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge mwaka 1970 na kuhudumu hadi mwaka 1974. Alizaliwa tarehe 13 Agosti, 1937 na kufariki mwaka 1977. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Karani (1957 - 1960), Afisa Wilaya Msaidizi (1961), Afisa Wilaya (1961 - 1962), Katibu Msaidizi wa Bunge (1962 -1970) na Balozi wa Tanzania nchini Uingereza (1974 – 1977).

**Jaji William Maina (1974 - 1979)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge mwaka 1974 na kutumikia nafasi hiyo hadi mwaka 1979. Alizaliwa tarehe 6 Mei, 1936 Kilema, Moshi. Ana Shahada ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 1969. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Jaji wa Mahakama Kuu (1979 – 1996), Kamishina wa Maadili (1979 – 2005) na Kamishina wa Tume ya Kurekebisha Sheria (2005 – 2008).

**Jaji Elias Kazimoto (1979 - 1985)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge mwaka 1979 na kuhudumu hadi mwaka 1985. Alizaliwa tarehe 9 Oktoba, 1942 Ulanga, Morogoro na kufariki mwaka 2020. Ana Shahada ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 1969. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Hakimu (1968), Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi (1979 - 1986) na Jaji wa Mahakama Kuu (1986 – 1998).

**Mahmoud Mwindadi (1985 - 1992)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge mwaka 1986 na kuhudumu hadi mwaka 1992. Alizaliwa tarehe 14 Februari, 1934. Ana Astashahada ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Miongoni mwa kazi

alizowahi kufanya ni pamoja na:- Katibu ngazi ya II kuanzia (1954 – 1962), Afisa Msaidizi wa Miundo ya Utumishi (1963 - 1965), Afisa Utawala (1965 – 1978), Afisa Mkuu wa Utawala na Rasilimali Watu (1978 -1979), Katibu Msaidizi Mwandamizi wa Bunge (1979 - 1983) na Katibu Msaidizi Mkuu wa Bunge (1982 – 1986).

**George Mlawa (1992 - 2000)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge mwaka 1992 na kuhudumu hadi mwaka 2000. Alizaliwa tarehe 10 Septemba, 1947. Ana Shahada ya Sheria na alihitimu kozi ya Ushauri wa Sheria (Legal Advisors) kutoka Advanced Legal Studies University ya London, Uingereza aliyohitimu mwaka 1985. Miongoni mwa kazi alizowahi kufanya ni pamoja na:- Mwanasheria wa Serikali (1974 - 1986), Katibu Msaidizi wa Baraza la Mawaziri, sehemu ya Katiba na Masuala ya Bunge (1986 - 1991), Naibu Katibu wa Tume ya Rais kuhusu Chama Kimoja au Vyama Vingi (1991 - 1992) na Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi (1992 - 1993). Alikuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2005.

**Jaji Kipenka Mussa (2000 - 2004)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge mwaka 2000 na kutumikia nafasi hiyo hadi mwaka 2004. Alizaliwa tarehe 28 Disemba, 1954. Ana Shahada ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 1981.

Miongoni mwa kazi alizowahi kufanya ni pamoja na:- Afisa Msaidizi Ustawi wa Jamii, Wizara ya Kazi (1976 - 1981), Mwanasheria wa Serikali katika ngazi mbalimbali (1981 - 1997), Mkurugenzi wa Haki za Binadamu, Wizara ya Katiba na Sheria (1997 - 2000), Jaji wa Mahakama Kuu (2004 - 2012) na Jaji wa Mahakama ya Rufaa (2012 - 2019).

**Damian Foka (2004 - 2008)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge mwaka 2004 na kuhudumu hadi mwaka 2008. Alizaliwa tarehe 29 Aprili, 1948 Kondoa mkoa wa Dodoma. Ana Shahada ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda aliyohitimu mwaka 1973. Miongoni mwa kazi alizowahi kufanya ni pamoja na:- Afisa Mipango, Wizara ya Uchumi na Mipango (1973 - 1974), Mchumi, Ofisi ya Mkoa wa Mwanza (1974 - 1977), Afisa Mipango katika Halmashauri mbalimbali (1977 – 1986) , Msaidizi wa Rais katika Ofisi ya Rais (1986 - 2000) na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (2000 - 2004).

**Dkt. Thomas Kashililah (2009 - 2017)**



Aliteuliwa rasmi kuwa Katibu wa Bunge mwaka 2009 baada ya kukaimu nafasi hiyo kuanzia mwaka 2008, na alihudumu hadi mwaka 2017. Alizaliwa tarehe 4 Machi, 1962 Lushoto mkoa wa Tanga. Ana Shahada ya Uzamivu ya Usimamizi wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Newport tawi la Afrika Kusini aliyohitimu mwaka 2005,

Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Newport tawi la Afrika Kusini aliyohitimu mwaka 2001 na Shahada ya Uchumi wa Viwanda kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 1987. Miongoni mwa kazi alizotumikia katika ni pamoja na:- Afisa Uchumi Tume ya Mipango (1987 - 1988) na Afisa wa Bunge katika ngazi mbalimbali (1988 - 2008). Aidha, aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo (2017 - 2019).

**Stephen Kagaigai (2017 – 2021)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge mwaka 2017, nafasi aliyohudumu hadi Mei, 2021. Alizaliwa tarehe 8 Mei, 1963 Ngara mkoa wa Kagera. Ana Shahada ya Uzamili ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 2004 na Shahada ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 1992. Miongoni mwa kazi alizowahi kufanya ni pamoja na:- Afisa wa Sheria katika Ofisi ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma, Wakili wa Serikali katika ngazi mbalimbali, Mratibu wa Utawala wa Utumishi wa Umma katika Ofisi ya Rais Ikulu, Msaidizi wa Katibu wa Baraza la Mawaziri (Cabinet undersecretary) na Kaimu Karani wa Baraza la Mawaziri.

**Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* (Kuanzia 2021 hadi sasa)**



Aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge Mei, 2021. Alizaliwa tarehe 9 Februari, 1973 Mkoa wa Dar es Salaam. Ana Shahada ya Uzamili ya Uongozi na Ulinzi wa Taifa kutoka Chuo cha Taifa cha Ulinzi, Dar es Salaam aliyohitimu mwaka 2019; Shahada ya Uzamili ya Sheria aliyohitimu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2009; na Shahada ya Sheria aliyohitimu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1999.

Miongoni mwa nafasi alizowahi kuzitumikia ni pamoja na:- Mkurugenzi wa Idara ya Shughuli za Bunge (2015 – Mei, 2021); Naibu Mshauri Mkuu wa Bunge, Mambo ya Sheria (2009 - 2015); Kiongozi wa Sekretarieti kwenye Kamati Maalum ya Ukaguzi wa Akaunti wa Tegeta (ESCROW) (2014); Mjumbe wa Sekretarieti kwenye Tume ya Mabadiliko ya Katiba (2012 - 2014); Kiongozi wa Sekretarieti kwenye Kamati Kamati Teule ya Bunge ya Kuchunguza Uhalali wa Utaratibu wa Wizara Kuchangisha Fedha kwa ajili ya kupitisha Bajeti Bungeni (JAIRO) (2011); Mjumbe wa Sekretarieti kwenye Kamati Teule ya Kuchunguza Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura (RICHMOND) (2008); na Mwanasheria Mwandamizi wa Bunge (2006 - 2009). Aidha, aliajiriwa Ofisi ya Bunge mwaka 2000 kama Mwanasheria wa Bunge.

# SURA YA NNE

## SEKRETARIETI NA OFISI ZA BUNGE

**Utangulizi**

Sura hii inahusu Sekretarieti ambayo ni Watumishi wa Ofisi ya Bunge wanaohudumia Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, kwa mujibu wa Ibara ya 88 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Sekretarieti ya Bunge imepitia hatua mbalimbali tangu kuundwa kwake mwaka 1962 ikianza na Watumishi watano ambao ni: Katibu wa Bunge, Katibu wa Bunge Msaidizi, Katibu Muhtasi, Dereva na Tarishi (Mhudumu). Hadi Mei, 2024, Sekretarieti ya Bunge ina Watumishi mia tatu na kumi; miongoni mwao wanaume ni mia moja thelathini na sita na wanawake ni mia moja sabini na nne.

Kwa upande wa Ofisi za Bunge, Sekretarieti imetumia majengo mbalimbali kama ofisi katika kutekeleza majukumu yake kwa vipindi tofauti vya historia ya Bunge. Makao Makuu ya Ofisi za Bunge yapo Dodoma na ofisi ndogo zingine zipo Dar es Salaam na Zanzibar.

**Sekretarieti na Tume ya Bunge**

Tangu Baraza la Kutunga Sheria hadi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watumishi wengi walikuwa ni wa kuazimwa kutoka Serikalini. Utaratibu wa kuazima uliendelea hadi mwaka 1998 ambapo baadhi ya watumishi walianza kuajiriwa kupitia Ofisi ya Rais,

Menejimenti ya Utumishi wa Umma baada ya kuundwa kwa Tume ya Bunge mwaka 1997.

Kuundwa kwa Tume hiyo kulianza, Januari 1996, baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki na Huduma za Bunge, kupewa jukumu la kujadili na kupendekeza Muundo mpya wa Bunge ili kuimarisha utendaji katika mfumo wa vyama vingi vya siasa kwa mujibu wa Waraka wa Spika wa Kumb. Na. BG/C/30/VOL.II/98. Taarifa ya Kamati hiyo ilisomwa Bungeni Aprili, 1996 ambapo ilipendekeza Bunge kuwa Taasisi inayojitegemea kwa kuzingatia Ibara ya 4(1) na Ibara ya 63(2) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, pendekezo lingine lilikuwa kuanzishwa kwa Muundo wa Bunge unaoakisi madaraka kamili katika utekelezaji wa majukumu yake; na kuwa na Tume ya Utumishi wa Bunge itakayoshughulikia masuala mbalimbali ya kibunge ikiwemo kusimamia Ajira, na Maslahi ya Wabunge na Watumishi. Kutokana na mapendekezo hayo Serikali iliwasilisha Muswada wa Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge wa mwaka 1997 uliopitishwa kuwa Sheria iliyoanza kutumika tarehe 1 Julai, 1997.

**Muundo wa Sekretarieti ya Bunge**

Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge ya mwaka 1997, iliipa Tume jukumu la kuandaa Muundo utakaofaa kwa ajili ya uendeshaji bora wa majukumu ya Bunge kwa kuzingatia mfumo wa vyama vingi vya siasa. Muundo uliopendekezwa ulikuwa na Ofisi Binafsi, Idara tano na Vitengo vinne kama ifuatavyo:- Ofisi ya Spika, Idara ya Shughuli za Bunge, Idara

ya Kamati za Bunge, Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, Idara ya Maktaba na Utafiti, Idara ya Utawala na Utumishi, Kitengo cha Uhasibu, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Kitengo cha Ulinzi na Usalama, na Kitengo cha Habari na Elimu kwa Umma. Aidha muundo huo ulipitishwa Aprili mwaka 1998.

Mwaka 2008, Bunge lilipitisha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge

ambayo ilifuta Sheria ya Tume ya Utumishi wa Bunge ya mwaka 1997, kwa lengo la kuweka utaratibu bora wa kuwezesha Sekretarieti kutimiza majukumu yake. Baada ya Sheria ya mwaka 2008 na mabadiliko kadhaa, Muundo wa Bunge wa mwaka 2018 unajumuisha Idara, Ofisi Binafsi na Vitengo vifuatavyo:- Ofisi Binafsi ya Spika, Ofisi Binafsi ya Naibu Spika, Ofisi Binafsi ya Katibu wa Bunge, Ofisi Binafsi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Idara ya Shughuli za Bunge, Idara ya Kamati za Bunge, Idara ya Maktaba na Utafiti, Idara ya Bajeti, Idara ya Sheria, Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge, Kitengo cha Uhasibu, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Kitengo cha Menejimenti ya Usimamizi, Ununuzi na Ugavi,

Kitengo cha Mawasiliano na Mahusiano ya Kimataifa, Kitengo cha TEHAMA na Kitengo cha Ulinzi na Usalama.

### Ofisi za Bunge

**Dar es Salaam:** Baada ya Uhuru wa Tanganyika, Sekretarieti ya Bunge ilikuwa ikitumia nyumba ya Serikali kama Ofisi, iliyokuwa eneo ambalo hivi sasa kimejengwa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Dar es Salaam. Baada ya

kuhama kwenye Ofisi hiyo, Sekretarieti ilikuwa ikitumia jengo lililokuwa *Park Road* (Barabara ya Luthuli), kwa sasa jengo hilo linatumiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sekretarieti ilianza kuwa na Ofisi zake mahususi mwaka 1960, baada ya Marion Lady Chesam, (aliyewahi kuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria kupitia jimbo la Iringa), kutoa zawadi ya nyumba yake iliyopo Mtaa wa Shaaban Robert ili itumike kama Ofisi ya Bunge. Jengo hilo ndilo linalotumika hadi sasa kama Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam.



*Jengo la Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam*

**Dodoma**: Baada ya Tamko la Rais la mwaka 1973 la kuhamishia Makao Makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma, mwaka 1974; Mikutano midogo ya Bunge ilianza kufanyika Dodoma na Mkutano wa Bajeti uliendelea kufanyika katika ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam. Kutokana na mabadiliko hayo, Sekretarieti ilipewa ofisi katika jengo la Makao Makuu ya CCM, Dodoma lililopo

Mtaa wa Kuu (Barabara ya Nyerere) ili kuratibu mikutano iliyofanyika Dodoma kwa urahisi. Ofisi za Bunge zilizokuwepo katika jengo hilo ni:- Ofisi ya Katibu wa Bunge, Utawala, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Uhasibu na Ofisi ya Uchaguzi.

Aidha, kutokana na uchache wa ofisi na kuongezeka kwa watumishi, mwaka 1984 Ofisi ya Bunge ilipanga katika Jengo la Christian Council of Tanzania (CCT) na kuhamishia Idara zake ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli zake, isipokuwa Idara ya *Hansard* ambayo iliendelea kubaki katika Jengo la CCM kurahisisha kuchukua kumbukumbu za vikao, kwa Mikutano iliyoendelea kufanyika katika jengo hilo.




*Jengo la CCT*

Ofisi za Bunge ziliendelea kuwepo katika Jengo la CCT kwa takriban miaka saba hadi mwaka 1991 zilipohamia katika jengo la Mji Mlezi (Mkapa House) lililokuwa likimilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma.




*Jengo la Mkapa (Mkapa House)*

Mwaka 1996, sehemu ya Sekretarieti ya Bunge ilihamia kwenye ofisi zilizokuwa katika kituo cha Uwekezaji cha Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali za Mitaa (LAPF) eneo la Makole. Mwaka 1997, Sekretarieti yote ya Bunge ilikua imehamia katika moja ya jengo la kituo hicho ambalo lilifanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji. Aidha, mwaka 1998 Serikali ilikinunua kituo hicho na kukikabidhi kwa Ofisi ya Bunge.



*Jengo Kuu la Utawala*

Aidha, ongezeko la Wabunge na Watumishi, lilisababisha Ofisi ya Bunge kuhitaji maeneo zaidi kwa ajili ya kujenga Ofisi na Kumbi za Mikutano ya Bunge. Kati ya mwaka 2003 na 2004, Ofisi ya Bunge ilinunua jengo la Kampuni ya magari ya Tanganyika (Tanganyika Motors Company) kwa ajili ya matumizi ya ofisi, na eneo lingine lilinunuliwa ili kujenga ukumbi mpya wa Bunge. Ukarabati wa jengo la Tanganyika Motors (Utawala Annex) umewezesha kupatikana kwa kumbi za Kamati za Bunge, kituo cha Afya na ofisi za Watumishi zilizoanza kutumika mwaka 2017. Aidha mwaka 2018 Bunge liliongeza eneo la Ofisi zake katika jengo kuu la utawala kwa kuongeza eneo jipya la ofisi na kumbi za mikutano kwenye sakafu ya tano.



*Jengo la Utawala Annex*

**Zanzibar:** Wazo la kuwa na Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar lilitokana na Mkutano Maalumu wa tarehe 5 Februari, 1977 uliofanyika uwanja wa Amani, Zanzibar wakati wa kuunganisha vyama vya TANU na ASP na kuzaliwa CCM. Kwa kuwa Wabunge wote wa Tanzania Bara walihudhuria tukio hilo, na hapakuwepo na Ofisi ya Sekretarieti kuratibu uwepo wao, ndipo ulipoonekana umuhimu wa kuanzishwa Ofisi Ndogo ya Bunge, Zanzibar.

Mwaka 1978, Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar walikubaliana kuhusu kuanzishwa kwa Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar. Wakati mchakato wa kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ukiendelea, Bunge

lilipatiwa ofisi ya muda na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwenye jengo la Mahakama Kuu eneo la Shangani.

Mwaka 1984, yalifanyika maadhimisho ya miaka 20 ya Muungano, ambapo ofisi mbalimbali za Serikali zilijenga mabanda ya maonesho Mwanakwerekwe ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano. Baada ya maadhimisho hayo yalitolewa maelekezo na Serikali ya Jamhuri kwamba, Banda la Ofisi ya Waziri Mkuu lililotumika katika maonesho hayo liboreshwe ili kuwa Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar lilioanza kutumika mwaka 1997.

Mwaka 2004, Tume ya Utumishi wa Bunge iliamua kufanya tathmini ya majengo yake yote ikiwa ni pamoja na jengo la Mwanakwerekwe, Zanzibar ambalo ilibainika litahitaji maboresho ambayo yangetumia gharama kubwa. Hivyo, Wajumbe walitoa pendekezo la kutafutwa kiwanja ili kujenga jengo jipya litakalokidhi mahitaji ya Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Bunge katika eneo la Tunguu Kusini Unguja ambapo jiwe la msingi la ujenzi liliwekwa tarehe 25 Aprili, 2004 na aliyekuwa Spika, Pius Msekwa. Ujenzi wa ofisi hiyo ulikamilika na kufunguliwa rasmi tarehe 27 Aprili, 2007 na aliyekuwa Rais wa SMZ na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Aman Abeid Karume.



*Jengo la Ofisi Ndogo ya Bunge, Zanzibar*

## SURA YA TANO

## KUMBI ZA BUNGE

### Utangulizi

Tangu kuanzishwa kwa Baraza la Kutunga Sheria mpaka kuitwa Bunge la Tanzania, baada ya Uhuru na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Bunge limetumia takribani Kumbi kumi kwa ajili ya mikutano yake. Baadhi ya Kumbi hizo ni:- Ukumbi wa Shule ya Agha Khan (Shule ya Sekondari Tambaza), Anatoglou, Freemansons Hall, Karimjee, CCM - Dodoma, Msekwa na sasa Ukumbi Mpya wa Bunge. Aidha, wakati Bunge lilipojulikana kama Baraza la Kutunga Sheria, liliwahi kukutana Arusha mwezi Desemba, 1929 katika Mkutano wa Bajeti. Vile vile, Bunge liliwahi kukutana Mwanza mwezi Oktoba, 1967 mara baada ya Mkutano Mkuu wa TANU. Aidha, Bunge limewahi kukutana Zanzibar, kisiwani Unguja mwaka 1977 na kisiwani Pemba mwaka 1978.

### Ukumbi wa Shule ya Agha Khan

Ukumbi huu ambao ulikuwa wa kwanza kutumiwa na Wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria, kwa sasa ni sehemu ya majengo ya Shule ya Sekondari ya Tambaza iliyopo barabara ya Umoja wa Mataifa, jijini Dar es Salaam. Aidha, ukumbi huu ulitumiwa hadi mwanzoni mwa miaka ya 1950.




*Jengo la Ukumbi wa Shule ya Agha Khan (Tambaza)*

**Ukumbi wa Anatoglou**

Ukumbi huu ulitumiwa na Baraza la Kutunga Sheria kuendesha Mikutano yake kati ya mwaka 1952 hadi mwaka 1955. Jengo hilo lilipewa jina la Anatoglou, ambaye alikuwa ni mlowezi wa Kigiriki aliyegharamia ujenzi wa ukumbi huo. Aidha, jengo hilo lilizinduliwa rasmi na Gavana Sir Edward Twining tarehe 8 Desemba, 1952.



*Jengo la Ukumbi wa Anatoglou*

**Ukumbi wa Freemasons**

Ukumbi huu ulitumiwa na Baraza la Kutunga Sheria kati ya mwaka mwaka 1952 hadi mwaka 1955 pale ambapo ukumbi wa Anatoglou ulikuwa na shughuli zingine.




*Jengo la Ukumbi wa Freemasons*


**Ukumbi wa Karimjee**

Ukumbi huu ulianza kutumiwa na Baraza la Kutunga Sheria tarehe 19 Aprili, 1955. Ukumbi huu ulijengwa na familia ya Karimjee na kutolewa zawadi kwa halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Abdulkarim Yusufali Karimjee akiwa Meya wa jiji la Dar es Salaam aliona uhitaji wa kuwa na ukumbi mahususi wa kuendeshea vikao vya Halmashauri, hivyo, alimwomba baba yake Mzee Yusufali Karimjee kujenga ukumbi kwa ajili ya Halmashauri. Ombi lake lilikubaliwa na hatimaye ukumbi ulijengwa na kuzinduliwa rasmi na Gavana Edward Twining tarehe 16 Aprili, 1955.



*Jengo la Ukumbi wa Karimjee*

Waraka wa kukabidhi jengo la Karimjee kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam



KNOW ALL MEN BY THESE PRESENTS THAT

WHEREAS the Karimjee Family came to the shores of Azania one hundred and thirty years ago as traders and merchant adventurers from India, and being well received and kindly treated, founded and established their house in Zanzibar and on the Azania Coast Lands; and

WHEREAS the House of Karimjee, by the Grace of God, prospered and took great part in the enterprise of developing these lands and opening the way for trade, commerce and agriculture, and being desirous of ensuring that a measure of the fruits of their industry and endeavour shall be devoted to the well being of the people of the country in which their House is established and which they have come to love in loyalty as their own;

NOW THEREFOR the members of the House of Karimjee, having caused this building to be erected as a token of their deep and loyal affection for this Territory and its peoples, do hereby give, donate and convey the said building, which shall be known as KARIMJEE HALL, to the Municipal Council of Dar es Salaam and dedicate it in perpetuity for the use benefit and enjoyment of all people of all races and creeds who dwell within the Municipality of Dar es Salaam.

Given under the hand of

YUSUFALI ALIBHAI KARIMJEE JIVANJEE

TAYABALI HASANALI ALIBHAI KARIMJEE

ABDULLA MOHAMEDALI ALIBHAI KARIMJEE

ABDULKARIM YUSUFALI ALIBHAI KARIMJEE

On behalf of the members of the House of Karimjee.

This sixteenth day of April, 1955 at Dar es Salaam.

Waraka wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kukubali kupokea zawadi ya jengo la Karimjee:-



PORTUS PACIS

MUNICIPAL COUNCIL OF DAR ES SALAAM

At a Special Meeting of the Municipal Council of Dar es Salaam held in the Council Chamber at the Karimjee Hall in the Municipality of Dar es Salaam on the 16th April, 1955

IT WAS RESOLVED

That this Council does hereby accept the gift of the Karimjee Hall, so generously offered by the Karimjee Family, for the use benefit and enjoyment of the people of Dar es Salaam and places on record its gratitude to the said Family for their munificence and public spirit in presenting such a magnificent gift.

In witness whereof the Common Seal of the Municipal Council of Dar es Salaam was hereunto affixed in the presence of :—

MAYOR

TOWN CLERK

## Ukumbi wa CCM - Dodoma

Ukumbi huu ulianza kutumiwa na Bunge mwaka 1974 baada ya Tamko la Rais Namba 230, la tarehe 1 Aprili, 1973 la kuhamisha Makao Makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Ukumbi huu ulitumika kwa Mikutano midogo ya Bunge isipokuwa Mkutano wa Bajeti ambao uliendelea kufanyika katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam. Ukumbi huo kwa sasa unatumiwa na *National Microfinance Bank* (NMB), Tawi la Dodoma.




*Jengo la CCM, Dodoma*

**Ukumbi wa Msekwa**

Ukumbi huu ulianza kutumika mwaka 1996 baada ya Bunge kuhamia rasmi Dodoma likiwa katika mfumo wa vyama vingi vya siasa. Jengo hili lilipo eneo la Makole lilikuwa linamilikiwa na Mfuko wa LAPF, na lilijengwa kama kituo cha Uwekezaji cha Mfuko huo. Kwa kuwa jengo hilo halikujengwa mahususi kwa ajili ya Mikutano ya Bunge, ililazimu yafanyike marekebisho kadhaa ili kukidhi mahitaji ya shughuli za kibunge.



*Jengo la Ukumbi wa Msekwa*

**Ukumbi Mpya**

Ukumbi huu uliojengwa rasmi kwa ajili ya shughuli za kibunge ulianza kutumika tarehe 12 Juni, 2006 baada ya kuzinduliwa rasmi na Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Pamoja na mambo mengine, kutokuwepo kwa jengo mahususi kwa ajili ya Mikutano ya Bunge na ongezeko la Wabunge, vilichagiza ujenzi wa ukumbi huo. Ukumbi huo wenye uwezo wa kutumiwa na takriban

Wabunge mia nne na mbili na Wageni mia mbili, ulianza kujengwa mwaka 2004 na kukamilika mwaka 2006.



*Jengo la Ukumbi Mpya wa Bunge*



*Ukumbi Mpya wa Bunge unavyoonekana kwa ndani*

# SURA YA SITA

## UJUMUISHAJI WA JINSIA BUNGENI

### Utangulizi

Sura hii inahusu namna Bunge lilivyozingatia masuala ya jinsia wakati likitekeleza majukumu yake. Ujumuishaji (gender mainstreaming) wa masuala ya jinsia bungeni, unaenda sambamba na historia ya Bunge la Tanzania ambapo, uwakilishi bungeni umezingatia mahitaji ya kimkakati ya wanawake na wanaume. Ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika ufuatiliaji na tathmini za shughuli za kitaifa ni moja ya mikakati ya kufikia usawa wa kijinsia duniani uliowekewa msisitizo na Mkataba wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake, uliosainiwa katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1979. Aidha, Tanzania imeridhia mkataba huo, na kuzingatia mikataba mingine ya kimataifa na kikanda inayohusu jinsia kwa kuandaa Sera, Mipango na Mikakati. Mwaka 2018, Bunge lilizindua Mkakati na Mpango Kazi wa Jinsia wenye lengo la kujumuisha masuala ya jinsia katika utekelezaji wa majukumu yake.

### Ujumuishaji wa Jinsia kabla na baada ya Uhuru

Tangu kuanza kwa Bunge la Tanzania mwaka 1926, hakukuwa na uwakilishi wa Wabunge wanawake hadi mwaka 1955 ndipo kwa mara ya kwanza waliingia Wabunge

wanawake watatu wa kuteuliwa ambao ni Bi. Elifuraha Mkamangi Mareale, Bi. K. F Walker na Bi. S. Keeka. Baada ya uhuru, idadi ya Wabunge Wanawake imekuwa ikiongezeka sambamba na kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi katika kila kipindi cha uhai wa Bunge kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

**Wabunge Wanawake na nyadhifa zao katika vipindi tofauti**

| Mwaka | Wabunge Wote | Wabunge Wanawake | Mawaziri | Naibu Waziri | Spika | Naibu Spika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1955 - 1960 | 82 | 4 | - | - | - | - |
| 1961 - 1962 | 81 | 7 | - | - | - | - |
| 1963 - 1965 | 98 | 6 | - | - | - | - |
| 1965 - 1970 | 190 | 4 | - | 1 | - | - |
| 1970 - 1975 | 202 | 4 | - | 1 | - | - |
| 1975 - 1980 | 227 | 13 | 2 | - | - | - |
| 1980 - 1985 | 226 | 12 | 2 | - | - | - |
| 1985 - 1990 | 239 | 24 | 5 | - | - | - |
| 1990 - 1995 | 233 | 22 | 5 | - | - | - |
| 1995 - 2000 | 268 | 41 | 6 | - | - | - |
| 2000 - 2005 | 289 | 62 | 4 | 5 | - | - |
| 2005 - 2010 | 318 | 94 | 6 | 6 | - | 1 |
| 2010 - 2015 | 350 | 122 | 8 | 4 | 1 | - |
| 2015 - 2020 | 393 | 145 | 4 | 7 | - | 1 |
| 2020 - 2025 | 393 | 147 | 7 | 5 | 1 | - |

*Chanzo: Kitabu cha Orodha za Wabunge na Taarifa Rasmi za Bunge kuanzia 1955 hadii 2024*

## Mabadiliko ya Katiba na Ongezeko la Wabunge Wanawake

### Katiba ya Mwaka 1977, Toleo la Mwaka 1984

Katiba za awali zilizotungwa kabla ya Katiba ya Kudumu ya mwaka 1977 hazikutaja idadi mahususi ya Wabunge Wanawake. Kwa mara ya kwanza katika mabadiliko ya Tano ya Katiba ya mwaka 1977, Toleo la mwaka 1984, Ibara ya 66 (1) (c), ilitaja idadi ya ya Wabunge Wanawake kumi na tano waliochaguliwa na Bunge kutoka miongoni mwa watu waliopendekezwa na jumuiya ya wanawake wa Tanzania, miongoni mwao angalau watano wakiwa wanatoka Tanzania Bara na watano wakiwa wanatoka Tanzania Zanzibar.

### Katiba ya Mwaka 1977, Toleo la Mwaka 1995

Mabadiliko yaliyofanyika katika Ibara ya 66(1) yaliongeza aina za Wabunge Wanawake kwa kuanzisha utaratibu wa viti maalum vya Wabunge Wanawake kufikia asilimia kumi na tano ya Wabunge wote badala ya idadi ya Wabunge kumi na tano. Aidha, Wabunge hao walichaguliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni kwa kuzingatia uwiano wa uwakilishi baina ya vyama hivyo.

### Katiba ya Mwaka 1977, Toleo la Mwaka 2000

Mabadiliko yaliyofanyika katika Ibara ya 66 (1) yaliongeza idadi ya viti maalum vya Wanawake Bungeni hadi kufikia asilimia ishirini kutoka asilimia kumi na tano ya awali

ambao walichaguliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni kwa kuzingatia uwiano wa uwakilishi baina ya vyama hivyo.

**Katiba ya Mwaka 1977, Toleo la Mwaka 2005**

Mabadiliko yaliyofanyika katika Ibara ya 66(1) yaliongeza idadi ya Wabunge Wanawake kupitia Viti Maalum hadi kufikia asilimia thelathini kutoka ishirini ya awali ambapo Wabunge hao walichaguliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni kwa kuzingatia uwiano wa kura. Aidha, mabadiliko ya Ibara ya 66 (1) (e) yaliongeza sharti katika Wabunge wa kuteuliwa na Rais kwa kuteua angalau Wanawake watano na Ibara ya 66 (1) (c) iliongeza sharti la kuongeza angalau Wabunge Wanawake wawili miongoni mwa Wabunge watano wanaochaguliwa kutoka Baraza la Wawakilishi.

**Tanbihi:** Jedwali lililopo mwisho wa Kitabu hiki linaonesha hali ya uwakilishi wa Wabunge Wanawake kuanzia mwaka 1954 hadi mwaka 1985 kabla ya mabadiliko mbalimbali ya Katiba ya Hamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Toleo la 1984.

**Wabunge Wanawake Walioshika Nafasi za Uongozi Kitaifa na Kimataifa**

Kuongezeka kwa nafasi za uwakilishi wa Wabunge Wanawake kumeleta mafanikio makubwa ndani na nje ya nchi, kwani baadhi yao wameweza kushika nafasi mbalimbali za uongozi kama vile Rais, Makamu wa Rais, Spika, Naibu Spika, Mawaziri na Manaibu Waziri.

Aidha, kutokana na utendaji wao wamefanikiwa kupata nafasi za uongozi katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Kutokana na nafasi zao, wamekuwa mfano kwa Wanawake wengine nchini katika kuongeza idadi ya uwakilishi wa Wanawake. Wafuatao ni baadhi ya Wabunge Wanawake waliofanikiwa kupata nyadhifa za ngazi za juu za uongozi kitaifa na kimataifa:-

**Samia Suluhu Hassan**



Ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 19 Machi, 2021; na nafasi ya Makamu wa Rais kuanzia mwaka 2015 hadi Machi, 2021. Ameshika nafasi ya u-Rais baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 37(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Alizaliwa tarehe 27 Januari, 1960 katika kijiji cha Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar. Ana shahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Southern New Hampshire kilichopo Marekani.

Mwaka 2000 alijiunga rasmi na siasa na kupata nafasi ya kuwa Mjumbe Maalum katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na aliteuliwa kuwa Waziri wa Ajira, Jinsia na Watoto. Mwaka 2005 alichaguliwa tena kuwa Mbunge na Waziri katika Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji katika

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ). Mwaka 2010 alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Makunduchi, Zanzibar na hivyo kuingia kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano, na aliteuliwa kuwa Waziri wa Muungano na Mazingira. Aidha, mwaka 2014, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba. Vile vile, amewahi kushika nafasi zifuatazo:- Mchapishaji SMZ (1977), Afisa wa Mipango SMZ (1987 - 1988), Meneja wa Mradi wa Shirika la Chakula Duniani (WFP), Zanzibar (1985 - 1997) na Mkurugenzi Mtendaji wa Mwamvuli wa AZAKI (1998 - 1999).

**Anne Semamba Makinda**



Ni mwanasiasa mkongwe kwa takribani miaka arobaini na mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Spika mwaka 2010 hadi mwaka 2015 na Naibu Spika kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2010. Wasifu wake kwa undani upo kwenye sehemu Maspika.

**Dkt. Tulia Ackson**



Alikuwa Mbunge wa Kuteuliwa na Naibu Spika wa Bunge la Kumi na Moja (2015 - 2020) na Bunge la kumi na mbili (2020- Januari, 2022); Vilevile, ndiye Mbunge wa jimbo la Mbeya Mjini kuanzia 2020 na Spika wa Bunge la Kumi na Mbili kuanzia Februari, 2022 hadi sasa. Aidha, ni mwanamke wa pili kushika nafasi ya Naibu Spika na Spika katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Vilevile ndiye Rais wa Umoja wa Mabunge duniani (IPU) kuanzia mwaka 2023 hadi sasa. Wasifu wake kwa undani upo kwenye sehemu ya Maspika.

**Balozi Dkt. Asha-Rose Migiro**



Aliingia Bungeni mwaka 2000 kupitia nafasi ya viti maalum. Alizaliwa tarehe 9 Julai, 1956 mkoa wa Ruvuma. Kupitia nafasi yake ya ubunge katika vipindi tofauti alishika nafasi mbalimbali za uwaziri kama: Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (2000 – 2005), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (2006 - 2007) akiwa mwanamke wa kwanza kuongoza wizara hiyo, na Waziri ya Katiba na Sheria (2013-2015).

Katika kipindi chake cha pili cha ubunge, Dkt. Migiro aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa nafasi aliyoitumikia kuanzia mwaka 2007 hadi 2012 akiwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika kushika wadhifa huo Mwaka 2016 aliteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Uingereza, nafasi anayoitumikia hadi sasa.

**Balozi Dkt. Getrude Mongela**



Aliingia Bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 1980 kama Mbunge wa Taifa, na baadaye kuchaguliwa kupitia Jimbo la Ukerewe mwaka 2000 hadi 2005. Alizaliwa tarehe 13 Septemba, 1945 Kanda ya Ziwa.

Miongoni mwa nyadhifa alizowahi kushika ni pamoja na:- Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (1982 - 1985), Waziri wa Ardhi, Utalii na Maliasili (1985 - 1987), Waziri Asiye na Wizara Maalumu (1987 - 1990).

Aidha, alishika nafasi mbalimbali katika nyanja za kimataifa kama:- Balozi wa Tanzania nchini India, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki (1975 - 1977), Mjumbe wa Umoja wa Afrika wa Kamati ya Wanawake ya Amani na Maendeleo jijini Addis Ababa, Kiongozi wa Mkutano wa Dunia wa kuhakiki na kutathmini mafanikio ya karne ya Umoja wa Mataifa kuhusu wanawake, na Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Katibu Mkuu wa Mkutano wa Nne wa Dunia wa Wanawake wa Beijing, China (1995). Mwaka 2004 Dkt. Mongela, alikuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika (Pan African Parliament) na mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo aliyotumikia hadi mwaka 2009.

**Anna Magret Abdallah**



Alikuwa Mbunge kuanzia mwaka 1975 hadi mwaka 2015 kupitia aina mbalimbali za ubunge. Alizaliwa tarehe 26 Juni, 1940. Alihitimu Shahada ya Sosholojia kutoka Chuo Kikuu cha Missouri, Marekani mwaka 1963. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na: Waziri wa Afya; Ujenzi; Kilimo na Maendeleo ya Mifugo; Serikali za Mitaa; Maendeleo ya Jamii na Ushirika na Masoko. Aidha, aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya

Wanawake Tanzania (UWT), Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wabunge Wanawake Tanzania na Mkuu wa Mikoa ya Dodoma na Morogoro.

**Bibi Titi Mohamed**



Alikuwa Mbunge wa Rufiji tangu wakati wa Baraza la Kutunga Sheria kuanzia mwaka 1960 hadi mwaka 1965. Alizaliwa Juni, 1926, Dar es Salaam na kufariki tarehe 5 Novemba, 2000. Alikuwa ni miongoni mwa wanawake wa mwanzo kujiunga na harakati mbalimbali za kupigania uhuru wa Tanganyika kuanzia miaka ya 1950. Mwanzoni mwa harakati zake za kisiasa alifanikiwa kulishawishi kundi kubwa la wanawake kujiunga pamoja ili kuunga mkono harakati za Tanganyika kujikomboa. Mwaka 1955, alichaguliwa kuongoza Tawi la Wanawake la chama cha TANU ambapo alitekeleza vema jukumu la kuwashawishi wanawake kuunga mkono harakati za ukombozi na sera za chama.

Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na:- Waziri Mdogo (Naibu Waziri) katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Utamaduni na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanganyika na Tanzania (1962 – 1967). Katika chapisho la Chama cha Mapinduzi la mwaka 1991 wakati wa kuadhimisha miaka 30 ya Uhuru alitajwa kama "Shujaa wa kike katika harakati za ukombozi". Kutokana na mchango wake kwa Taifa barabara mojawapo maarufu ya Jiji la Dar es Salaam imeitwa kwa jina lake.

## Lucy Selina Lameck Somi



Alikuwa Mbunge wa Kuteuliwa katika Bunge la Tanganyika (1960 – 1965); Mbunge wa Kuchaguliwa (1965 - 1975); na (1980 - 1993) kutoka mkoa wa Kilimanjaro.

Alizaliwa mwaka 1934 mkoani Kilimanjaro na alifariki 21 Machi, 1993. Alihitimu elimu ya uuguzi na ukunga mkoani Tanga, mwaka 1955; Stashahada ya Utawala na Siasa kutoka chuo cha Ruskin, Oxford mwaka 1959; na masomo ya Uhusiano wa Kimataifa kutoka chuo cha Western Michigan mwaka 1961.

Alikuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya u-Waziri Mdogo (Naibu Waziri), akiwa Waziri Mdogo wa Masuala ya Ushirika na Maendeleo ya Jamii (1962 – 1965); na Naibu Waziri wa Afya (1966 - 1972). Miongoni mwa nafasi nyingine aliyowahi kushika ni pamoja na Katibu Muhtasi (1955 - 1957), katika Chama cha Ushirika cha Kilimanjaro (Kilimanjaro Native Cooperative Union).

Kutokana na harakati zake za kupambana na ukoloni, ubaguzi wa rangi na michango yake kisiasa, Novemba, 2020 alipewa heshima ya kupewa jina la mtaa huko Berlin nchini Ujerumani unaoitwa Lucy Lameck strasse. Jina hilo limebadilishwa kutoka Wissmann strasse ambaye alikuwa gavana wa koloni la Ujerumani Afrika Mashariki kati ya mwaka 1895 na 1896.

**Thabita Siwale**



Aliingia Bungeni kwa kuteuliwa na Rais mwaka 1975 na kuendelea na nafasi hiyo kwa aina mbalimbali za ubunge hadi mwaka 2000.

Alizaliwa mwaka 1939 katika kitongoji cha Bagamoyo, Tukuyu, mkoani Mbeya. Alihitimu Shahada ya *Home Economics* aliyoipata Nairobi, Kenya.


Alikuwa Mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya uwaziri nchini, ambapo alikuwa Waziri wa Nyumba, Ardhi na Maendeleo Mijini (1975 - 1980); (1982 - 1984) na Waziri wa Elimu ya Taifa (1980 - 1982). Aidha, alikuwa Mkuu wa shule za sekondari za wasichana za Bwiru, Mwanza na Korogwe, Tanga.

**Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania**

Umoja wa Wabunge Wanawake (Tanzania Women Parliamentarians Group - TWPG) ulianzishwa mwaka 1993, kwa lengo la kuwaunganisha na kuwajengea uwezo Wabunge Wanawake bila kujali itikadi zao za vyama, ili kujadili masuala mbalimbali yanayowahusu na kutekeleza ipasavyo majukumu yao ya kibunge ndani na nje ya Bunge. Umoja huu unahamasisha ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika nyanja za siasa, uchumi, jamii na

utamaduni na kuongeza nafasi za uwakilishi wa wanawake katika ngazi za maamuzi, utungaji wa sheria, sera na mipango mbalimbali ya Serikali. Kutokana na juhudi za kuhamasisha ujumuishaji, baadhi ya Wabunge wanaume wameunga mkono jitihada hizo kwa kuwa vinara wa maasula ya jinsia bungeni.

**Mkakati na Mpango Kazi wa Jinsia Bungeni**



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PARLIAMENT OF TANZANIA

GENDER STRATEGY AND ACTION PLAN FOR THE NATIONAL ASSEMBLY

OFFICE OF THE NATIONAL ASSEMBLY,
P.O.BOX 941,
DODOMA

JUNE, 2018

Mkakati na Mpango Kazi wa Jinsia Bungeni, ulizinduliwa mwaka 2018 ukiwa na lengo la kujumuisha masuala ya jinsia bungeni, kwa kuzingatia mahitaji yote ya kimkakati ya Wanawake na Wanaume katika miundo, mifumo na shughuli zote za uendeshaji wa Bunge. Mkakati na Mpango Kazi pia umelenga kuongeza uwakilishi wa Wabunge wa jinsia zote pamoja na wenye mahitaji maalumu ya kimkakati kama vile Wabunge wenye ulemavu na Wabunge vijana. Hata hivyo, kabla ya kuwepo kwa Mkakati na Mpango Kazi huu, Bunge la Tanzania lilishakuwa na Wabunge wenye ulemavu na Wabunge Vijana tangu mwaka 2000.

# SURA YA SABA

# BUNGE NA DIPLOMASIA YA KIBUNGE

## Utangulizi

Mabunge mbalimbali duniani kupitia Diplomasia ya Kibunge hushirikiana ili kubadilishana uzoefu na uelewa katika taratibu za uendeshaji wa Mabunge, pamoja na kujadili masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Aidha, Mabunge yamekuwa yakishirikiana kupitia mikutano, semina, warsha, makongamano na ziara zinazoandaliwa na Mabunge, Vyama vyao vya Kikanda na Kimataifa. Bunge la Tanzania limekuwa likishirikiana na Mabunge, Vyama vya Kibunge vya Kikanda na Kimataifa kutokana na Mikataba ya Kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia. Wawakilishi katika vyama hivyo huchaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kuzingatia jinsia, pande za muungano na uwakilishi wa vyama.

Ushiriki wa Bunge na Wabunge kwenye Diplomasia ya Kibunge na Vyama hivi, umeongeza ushawishi wa masuala ambayo ni ajenda ulimwenguni na kuchochea kasi ya kuridhia mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Tanzania pale ambapo Mikataba hiyo inaonekana kuwa na tija kiuchumi, kisiasa na kijamii, na hivyo kuwa na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kikatiba.

Bunge la Tanzania ni mwanachama wa Mabunge na Vyama vya Kibunge vya Kikanda na Kimataifa vifuatavyo:-

**Bunge la Afrika Mashariki**

Bunge la Afrika Mashariki (East Africa Legislative Assembly) lilianzishwa mwaka 2001, ikiwa ni chombo kimojawapo cha Taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa Ibara ya 9 ya Mkataba ulioanzisha tena Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1999. Bunge la Afrika Mashariki linafanya kazi na kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Mkataba ulioanzisha Jumuiya hiyo. Aidha, Ibara ya 48 ya Mkataba huo imeweka utaratibu wa kuchaguliwa kwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kutoka katika kila nchi mwanachama wa Jumuiya. Kama ilivyo katika nchi zote wanachama, Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kutoka Tanzania pia, hawatokani na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, bali hutokana na wananchi wenye sifa ambao hupigiwa kura kila baada ya miaka mitano na Wabunge wa Bunge la Tanzania, ambacho ndicho chombo mahususi kilichopewa jukumu hilo. Makao makuu ya Bunge hilo yapo Arusha, Tanzania. Spika wa kwanza wa Bunge la Afrika Mashariki alikuwa mtanzania Ndg. Abdulrahman Kinana kuanzia mwaka 2001 hadi mwaka 2006.

**Bunge la Afrika**

Bunge la Afrika (Pan African Parliament) lilianzishwa mwaka 2004 likiwa ni moja kati ya Taasisi kumi za Umoja wa Afrika. Bunge hili liliundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 17 cha Mkataba wa Umoja wa Afrika, (Constitutive Act of the African Union) uliosainiwa tarehe 11 Julai, 2000 na nchi 53 za Umoja huo. Malengo makuu ya kuanzishwa kwake ni kurahisisha uhimizaji wa utekelezaji bora wa sera, kanuni na taratibu zilizowekwa na Umoja wa Afrika, na kuhamasisha nchi kudumisha haki za binadamu, utawala bora na uwajibikaji. Makao makuu ya Bunge hilo yapo Midrand, Afrika Kusini. Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika alikuwa mtanzania Balozi Dkt. Getrude Mongela kuanzia mwaka 2004 hadi mwaka 2009.

**Bunge la Pamoja la Nchi za Umoja wa Ulaya, Afrika, Carribean na Pasifiki**

Bunge la Pamoja la Nchi za Umoja wa Ulaya, Afrika, Carribean na Pasifiki (ACP/EU Joint Assembly) lilianzishwa ili kuwakutanisha Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Ulaya na wenzao wa Afrika, Carribean na Pacific. Chimbuko la Bunge hili ni mkataba wa Cotonou ambao ulisainiwa mwaka 2000 Cotonou, Benin na ulianza kutumika rasmi mwaka 2003 ambapo pia Bunge la Tanzania lilijiunga. Bunge hili hufanya mikutano miwili kwa

mwaka ambapo mkutano mmoja hufanyikia makao makuu ya EU huko Brussels na mkutano wa pili kwenye mojawapo ya nchi za ACP. Kazi za Bunge la EU/ACP ni:- Kuwezesha michakato ya kidemokrasia kwa njia za mazungumzo na mashauriano, kuongeza uelewa miongoni mwa watu wa pande hizi mbili kuhusu masuala ya maendeleo na changamoto zake, kujadili masuala yanayohusu maendeleo kwenye muktadha wa ushirikiano baina ya nchi za EU na ACP, kuridhia Maazimio na kuwasilisha mapendekezo kwenye Baraza la Mawaziri la kila nchi mwanachama kwa lengo la kutekeleza malengo ya Mkataba.

**Umoja wa Mabunge ya Nchi za Maziwa Makuu**

Chimbuko la Umoja Umoja wa Mabunge ya Nchi za Maziwa Makuu (International Conference on Great Lakes Region) ni Azimio la Dar es Salaam kuhusu Amani, Usalama na Maendeleo katika Ukanda wa Maziwa Makuu lililosainiwa na Wakuu wa Nchi 11 za Ukanda wa Maziwa Makuu mwezi Novemba, 2004 Jijini Dar es Salaam. Azimio hili lilifuatiwa na utiaji saini wa Mkataba wa Usalama, Utengamano na Maendeleo katika Eneo la Maziwa Makuu uliosainiwa na Wakuu wa Nchi huko Nairobi, Kenya tarehe 15 Desemba, 2006. Hivyo, katika kuunga mkono azma ya viongozi wa nchi hizo, tarehe 4 Desemba, 2008 huko Kigali, Rwanda, Mabunge ya Nchi Wanachama yalianzisha Jukwaa la Kibunge kuhusu Mkutano wa Kimataifa wa eneo la

Maziwa Makuu. Makao Makuu ya Umoja huu yapo Kinshasa, Congo.

**Jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

Jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC - Parliamentary Forum) lilianzishwa mwaka 1997 Jijini Blantyre, Malawi kufuatia Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa SADC kuafiki uwepo wake kama moja ya Taasisi za SADC kwa mujibu wa Ibara ya 9(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa SADC. Bunge la Jamhuri la Tanzania ni mwanachama wa Jukwaa hili tangu mwaka 1997, lilipoanzishwa. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Jukwaa hili ni kuharakisha mtangamano wa nchi hizo na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Mkataba wa SADC.

Aidha, Jukwaa hili limekuwa fursa kwa Wabunge wa nchi wanachama kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya Demokrasia, Haki za Binadamu, Utawala Bora, UKIMWI na Maendeleo Endelevu. Makao Makuu ya Jukwaa hili yapo Windhoek, Namibia. Anne Makinda akiwa Spika aliwahi kuwa Rais wa Jukwaa la Kibunge la nchi za SADC kuanzia mwaka 2014 hadi mwaka 2015.

**Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola**

**Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (Commonwealth Parliamentary Association - CPA)** kilianzishwa mwaka 1911, kwa lengo la kuunganisha, kukuza na kuendeleza maadili na utamaduni wa Jumuiya ya Madola ambazo ni nchi zote zilizotawaliwa na Mwingereza. Awali uanachama kwenye umoja huu uliyahusu Mabunge ya nchi zilizokuwa kwenye himaya ya utawala wa Uingereza pekee. Hata hivyo, Mabunge ya nchi ambazo hazikutawaliwa na Uingereza yalikubaliwa kuwa Wanachama wa CPA ilimradi yanaafiki na kuzingatia malengo ya kuanzishwa kwa Umoja huu. Makao Makuu ya CPA ngazi ya Kimataifa yapo Jijini London, Uingereza.

Aidha, CPA imegawanyika kwenye Kanda Kumi (10), ambazo hujiendesha kwa kuzingatia Taratibu, Kanuni na Sheria kama zilivyoainishwa kwenye Katiba za Kanda husika pamoja na Katiba ya CPA. Bunge la Tanzania lilijiunga rasmi na CPA mwanzoni mwa miaka ya 1980. Bunge la Tanzania limekuwa likishiriki kwenye Mikutano ya CPA Kimataifa na ile ya Kanda ya Afrika, na katika vipindi tofauti limekuwa mwenyeji wa Mikutano hiyo, Kimataifa mwaka 2009, na Kikanda mwaka 2014 na 2019. Awali, makao makuu ya CPA (Kanda ya Afrika) yalikuwa Zimbabwe hadi mwaka 2003 nchi hiyo ilipojitoa

uanachama kwenye Jumuiya hiyo. Baada ya nchi hiyo kujitoa, makao makuu ya CPA (Kanda ya Afrika) yakahamia Tanzania mwaka 2003, ambapo Katibu wa Bunge la Tanzania ndiye Katibu wa CPA - Kanda ya Afrika. Katibu wa kwanza Mwafrika wa CPA ngazi ya Kimataifa alikuwa mtanzania Dkt. William F. Shija kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka 2014.

**Umoja wa Mabunge Duniani**

Umoja wa Mabunge Duniani (Inter-Parliamentary Union) hujumuisha Mabunge ya nchi huru Wanachama wa Umoja wa Mataifa na ulianzishwa mwaka 1889. Bunge la Tanzania lilijiunga rasmi na Umoja huu mwaka 1984. Malengo makuu ya Umoja huu ni:- kurahisisha mawasiliano, kuratibu na kubadilishana uzoefu miongoni mwa Mabunge na Wabunge na kujadili masuala yenye maslahi kidunia na kuyatolea mapendekezo ya hatua za ufumbuzi. Malengo mengine ni kusaidia juhudi za kuleta amani duniani kwa kusisitiza kuheshimu haki za binadamu, na kusaidia Mabunge kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu yake kupitia mikutano, semina, warsha na makongamano. Makao Makuu ya IPU yapo Geneva, Switzerland. Aidha, Rais wa sasa wa IPU ni Dkt. Tulia Ackson akiwa ni thelathini na moja na mwanamke wa kwanza kutoka Afrika na wa tatu duniani kushika wadhifa huo.

# SURA YA NANE

## MATUKIO MAHUSUSI YALIYOJIRI BUNGENI

**Utangulizi**

Sura hii inahusu baadhi ya matukio mahususi yaliyowahi kutokea Bungeni tangu uhuru hadi sasa. Miongoni mwa matukio hayo ni:- Hotuba za Marais na Wageni Mashuhuri Bungeni, Hoja Binafsi, Kamati Teule na Kamati Maalum za Bunge.

**Hotuba za Marais**

Tangu Tanzania ipate uhuru kumekuwa na awamu tano za uongozi wa nchi zilizoongozwa na marais wafuatao:- Mwalimu Julius Kambarage Nyerere - Awamu ya Kwanza (1962 - 1985); Ali Hassan Mwinyi – Awamu ya Pili (1985 - 1995); Benjamin William Mkapa - Awamu ya Tatu (1995 - 2005); Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete – Awamu ya Nne (2005 - 2015); Dkt. John Pombe Joseph Magufuli – Awamu ya Tano (2015 – Machi, 2021); na Samia Suluhu Hassan – Awamu ya Sita (Machi, 2021 hadi sasa).

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 65(1) na (2), maisha ya Bunge ni muda wa miaka mitano kuanzia kipindi ambacho Bunge jipya limeitishwa, baada ya Uchaguzi Mkuu mpaka tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge husika ili kupisha uchaguzi mwingine.

Kwa mujibu wa Ibara ya 90 na Ibara ya 91 za Katiba, Rais anayo mamlaka ya kuliitisha, kulihutubia na kulivunja Bunge. Zifuatazo ni baadhi ya nukuu za hotuba za Marais walipolihutubia Bunge :-

**Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (1962 – 1985)**



Alikuwa Rais wa Awamu ya Kwanza ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1962 - 1985). Alizaliwa tarehe 13 Aprili, 1922 katika kijiji cha Butiama, Mkoani Mara na kufariki tarehe 14 Oktoba, 1999. Wasifu wake kwa undani upo kwenye kipengele cha Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

**25 Aprili, 1964**

Rais wa Awamu ya Kwanza Mwalimu Nyerere alilihutubia Bunge tarehe 25 Aprili, 1964, Dar es Salaam, lengo likiwa kuwaomba Wabunge wathibitishe Mkataba wa Muungano kati ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, ili kuzifanya nchi hizo mbili kuwa nchi moja.

*" Paliamenti hii ndiyo Baraza Kuu la Wananchi wa Tanganyika"*

*"Nimewaiteni katika kikao hiki cha haraka ili kuwaomba mthibitishe Mkataba wa Muungano kati ya Jamhuri yetu na Jamhuri ya Unguja. Paliamenti hii ndiyo Baraza Kuu la Wananchi wa Tanganyika. Hapana jambo lolote kubwa linalohusu Katiba, au Mikataba au Sheria za nchi hii ambalo laweza kupitishwa*

*na mtu au kundi lolote ila Baraza hili. Mambo yote ya aina hiyo hayana budi yafikishwe katika Baraza hili na ni juu yenu kuyakubali au kuyakataa. Leo naleta mbele yenu Mkataba wa Muungano kati ya Tanganyika na Unguja kuzifanya ziwe nchi moja."*

**12 Oktoba, 1965**

Mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1965, Mwalimu Nyerere alitoa hotuba ya kufungua Bunge jipya, ambapo alimpongeza Bwana Spika (Khatibu) kwa kazi kubwa ya kusimamia uchaguzi huo.

*"Liko kundi jingine la watenda kazi ninalotaka kulishukuru sana. Mzigo mkubwa wa uchaguzi huu ulikuwa mabegani mwako, Bwana Spika (Khatibu), na watenda kazi wa ofisi yako, hasa makarani wawili wa Bunge hili. Labda litakuwa jambo jema ikiwa Wabunge waheshimiwa mtafikiri kidogo jinsi azimio la Bunge ambalo pengine hupitishwa kwa muda mfupi tu, linavyohitaji kazi kubwa sana kutimizwa. Uamuzi wa kufanya uchaguzi unahitaji kazi kubwa sana kutimizwa…."*

Vile vile, aliwakumbusha Wabunge wajibu wao kwa wapiga kura, kwa kusema: -

*"Kazi ya Mbunge imegawanyika sehemu tatu. Kwanza, ni kiunganisho kati ya watu na Serikali; pili kufikiria sheria mpya; na tatu, kuisahihisha Serikali ili itie juhudi zake zote kutimiza haja za watu… Kwa kweli moja katika kazi kubwa za*

*mjumbe wa Bunge ni kukutana na watu na kujua mawazo yao. Ikiwa mjumbe atafanya kazi yake barabara katika wilaya atasaidia sana kuwa kiunganisho baina ya watu na Serikali. Atachukua mawazo ya watu kuyapeleka Serikalini na atachukua mawazo ya Serikali kuyapeleka kwa watu. Ataweza kuwaeleza watu Serikali inajitahidi kufanya kitu gani, na jinsi gani wao wenyewe wanavyoweza kufaidika na mipango ambayo Serikali inafanya kuinua hali ya maisha ya watu. Vilevile ataweza kuieleza Serikali fikara mpya kutoka kwa watu, au jinsi watu wanavyoweza kusaidiwa, au kuieleza Serikali shida za watu".*

Pia, Mwalimu Nyerere aliwaasa Wabunge kutowashambulia Watumishi wa Serikali, kwa kusema:-

*"Na jambo moja la maana kabisa ni hili. Wabunge wasizoee kuwashambulia watumishi wa Serikali katika Bunge hili. Ikiwa mbunge anaamini ya kwamba mtumishi wa Serikali amekosa, na ya kwamba kumetokea maonevu fulani, basi Mbunge amwulize Waziri anayehusika. Na hapo basi itakuwa kazi yake kupeleleza jambo lile, na kama kushauri hatua zichukuliwe mtumishi yule aadhibiwe kisheria".*

**22 Julai, 1980**

Aidha, aliwapongeza Wabunge kwa wajibu wao kwa Taifa na kwa wapiga kura, kwa kusema: -

*"Ndugu Spika, katika mapambano ya miaka mitano iliyopita Wabunge wa Bunge hili wamesaidia sana, na wamedhihirisha*

*kwamba wamestahili imani waliyopewa na wananchi. Wakati mwingine wamekuwa wakiikosoa Serikali, na huo ni wajibu wao; wakati mwingine wamedai Serikali mambo yasiyowezekana; na huo ni ubinadamu. Lakini wakati wote wamefanya Serikali iwe macho, na wameeleza shida za wananchi waliowachagua. Na Wabunge wengi vilevile wamefanya kazi kubwa katika majimbo yao ya uchaguzi, wakisaidia kuendeleza juhudi za wananchi katika maendeleo, na wakati huo huo wakiangalia utekelezaji wa Sera mbalimbali za Chama na Serikali katika majimbo yao".*

**Ali Hassan Mwinyi (1985 – 1995)**



Alikuwa Rais wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1985 hadi mwaka 1995. Alizaliwa tarehe Mei 8, 1925 Kivule, mkoani Pwani na kufariki mwaka 2024. Aliwahi kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (1984 - 1985); Waziri wa Maliasili na Utalii (1982 – 1984; Balozi wa Tanzania Nchini Misri (1977 – 1982); Waziri wa Mambo ya Ndani (1975 – 1977); na Waziri wa Afya (1972 - 1975).

**7 Novemba, 1985**

Rais Ali Hassan Mwinyi, katika hotuba hii, alilipongeza na kulishukuru Bunge kwa kutimiza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa kusema:-

*"Ndugu Spika, Bunge lililopita lilianza kazi zake katika hali ngumu ya uchumi. Wabunge waliotoa mchango mkubwa*

*katika kujadili na kupitisha mipango ya maendeleo na bajeti za Serikali kila mwaka katika kipindi hiki kigumu. Nina hakika Serikali ilifaidika sana kwa mchango wao... Bunge lilipitisha marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano mwaka jana kwa madhumuni ya kuimarisha madaraka ya Umma na ya Bunge, kuimarisha uwakilishi wa Bungeni, kuimarisha Muungano na kufafanua madaraka ya Rais."*

Vile vile, alizungumzia utashi wa Serikali kulisaidia Bunge ili liweze kutekeleza wajibu wake ikiwa ni pamoja na kuliundia Sekretarieti itakayosaidia utekelezaji wa majukumu ya Bunge kwa kusema:-

> *"Bunge ndicho chombo ambacho kwa niaba ya Wananchi husimamia na kuishauri Serikali"*

*"….Kwanza kabisa Bunge ndicho chombo ambacho kwa niaba ya wananchi, husimamia na kuishauri Serikali katika kutekeleza majukumu yake… Ili kulisaidia Bunge katika majukumu haya Serikali itahakikisha kuwa Bunge hili linakuwa na Sekretarieti ya kulisaidia hasa katika kuzihudumia Kamati zake mbalimbali kwa kuzifanyia utafiti unaohitajika. Kuundwa kwa Sekretarieti hii kutakuwa ni utekelezaji wa mojawapo ya marekebisho ya Katiba yaliyofanywa mwaka 1984 na Bunge lililopita. Sekretarieti hiyo itawawezesha Wabunge kudhibiti vizuri utekelezaji katika Serikali na Mashirika ya Umma…"*

**28 Julai, 1995**

Rais Mwinyi alilihutubia na kulivunja Bunge ili nchi iweze kujiandaa na Uchaguzi Mkuu wa awamu nyingine ya uongozi wa nchi, pale nchi yetu ilipoamua kurejesha mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Katika hotuba hiyo alisema:-

> *"Mheshimiwa Spika, kipindi hiki cha awamu ya pili kimeshuhudia mabadiliko makubwa ya kisiasa, hasa baada ya kutoa ruhusa ya kuanzisha vyama vya siasa. Bunge hili Tukufu limepitisha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992, iliyoanza kutumika tarehe 1 Julai, 1992. Tangu wakati huo vyama 13 vya siasa vimesajiliwa rasmi. Vyama hivi vimeendelea kuimarika siku hadi siku kutokana na mazingira huru yaliyowekwa na Serikali. Sasa hivi vyama hivyo vinajiandaa kwa Uchaguzi Mkuu hapo ifikapo mwezi Oktoba".*

**Benjamin William Mkapa (1995 – 2005)**



Alikuwa Rais wa Awamu ya Tatu kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka 2005. Alizaliwa tarehe 12 Novemba, 1938 na kufariki tarehe 24 Julai, 2020. Aliwahi kuwa Waziri wa Sayansi na Elimu ya Juu (1992 - 1995); Waziri wa Habari na Utangazaji (1990 - 1992); Balozi wa Tanzania nchini Marekani (1983 - 1984); Balozi wa Tanzania nchini Canada (1982 - 1983); Waziri wa Habari na Utamaduni (1980 - 1982); Waziri wa Mambo ya

Nje (1977 – 1980 na 1984 – 1990); na Balozi wa Tanzania nchini Nigeria (1976 - 1977).

**4 Novemba, 1998**

Rais Mkapa alilihutubia Bunge, pamoja na masuala mengine aliyoyaelezea ya kijamii, kiuchumi, kiusalama, amani na uhusiano wa kimataifa, alizungumzia pia hali ya kisiasa kwa kuelezea umuhimu wa Wabunge wa Upinzani ndani ya Bunge:-

> *"Mheshimiwa Spika, kila sarafu ina pande mbili. Kazi na manufaa ya kuwepo kwa Wabunge wa Vyama vya Upinzani ndani ya Bunge ni kila mara kuonyesha upande wa pili wa hoja za Serikali na kuhakikisha Serikali haisinzii. Wabunge wa Vyama vya Upinzani kwa ujumla wamejitahidi kufanya kazi hiyo, na nawashukuru sana…..upo ushirikiano wa Wabunge wa Chama Tawala na wale wa Vyama vya Upinzani. Sijawahi kusikia mmeshikana mashati, kutukanana au kutwangana ngumi ndani au nje ya ukumbi huu kama inavyotokea katika baadhi ya nchi nyingine. Wala hakuna mtindo wa kudumu wa kususia vikao".*

**20 Novemba, 2000**

Rais Mkapa alitilia mkazo umuhimu wa kushirikiana na upinzani ili kuboresha utendaji wa Serikali kwa kusema:-

> *"Nawapongeza Wabunge wa Vyama vya Upinzani. Chama cha Mapinduzi ni jabali kweli kweli; chama kikongwe na*


*chenye nguvu kuliko vyote nchini, si kazi nyepesi kukishinda chama hicho hivyo nanyi mnastahili pongezi za pekee. Katika Bunge hili mtakuwa wachache kuliko ilivyokuwa katika Bunge lililopita. Lakini msiwe wanyonge au wapweke. Sote lengo letu ni kujenga nchi yetu na hakuna sababu za msingi kwa nini tusishirikiane vizuri. Kama nilivyoahidi siku ya kuapishwa kwangu, hoja zenu tutazizingatia iwapo zitasaidia kuboresha utendaji wetu. Hatutazipuuza kwa vile tu zimetolewa na upande wa upinzani. Uzito wa hoja zenyewe ndio utakuwa kigezo cha ama hoja kuzingatiwa au kuachwa".*

Vilevile, alizungumzia umuhimu wa ushirikiano kati ya Bunge na Serikali kwa kusema:-

*"Mheshimiwa Spika, nimesema mengi lakini mengi bado sijayasema. Haiwezekani nikayasema yote, nilichotaka kufanya leo ni kulijulisha Bunge lako Tukufu, juu ya mweleko ambao ninakusudia Serikali nitakayoiunda iongozwe nao. Nitajitahidi kuunda Baraza la Mawaziri liliosheheni uadilifu, uwezo na uzoefu wa kutekeleza niliyoyataja hapa na yale ambayo sikuyataja. Itakuwa Serikali ya vitendo inayoongozwa na malengo yaliyo wazi na vigezo vya utekelezaji. Lakini mafanikio yake yatategemea ushirikiano tutakaoupata katika Bunge hili. Naomba ushirikiano huo."*

**12 Februari, 2004**

Rais wa Awamu ya Tatu alilieleza Bunge azma ya mapendekezo ya mabadiliko ya Katiba ambayo moja ya kusudio lake ni kuongeza idadi ya Wabunge wanawake ambapo alisema:-




*"Katika miezi ijayo, tutapendekeza mabadiliko ya Katiba ambayo kwa maoni yetu yatasaidia kuimarisha demokrasia katika nchi yetu…tutazidi kuongeza nafasi na uwakilishi wa wanawake katika vyombo vya maamuzi. Kwa upande wa Bunge, ninakusudia idadi yao isipungue asilimia 30 ya Wabunge kabla sijaondoka madarakani."*

**Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete (2005 – 2015)**



Alikuwa Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2015. Alizaliwa tarehe 7 Oktoba 1950, kijiji cha Msoga, mkoani Pwani. Aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (1995 - 2005); Waziri wa Fedha (1994 - 1995); Waziri wa Maji, Nishati na Madini (1990 - 1994) na Naibu wa Waziri wa Nishati na Madini (1988 - 1990).

**30 Desemba, 2005**

Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliwaomba Wabunge wawe kitu kimoja ili kuweza kutekeleza shughuli za ujenzi wa nchi, alisema:-

> *"Nawashukuru watani zetu wa Kambi ya Upinzani kwanza, kwa ujasiri wao mkubwa wa kujitokeza kushindana na Chama cha Mapinduzi, maana kushindana na CCM siyo mchezo! Uchaguzi sasa umekwisha naomba ndugu zangu tuungane, tuwe kitu kimoja, tujenge na kuendeleza nchi yetu…kama mwana-CCM nafurahia sana ushindi wetu, lakini nikiwa Rais napenda niwahakikishie wenzetu wa Upinzani kuwa sina nia wala CCM haina nia au sera ya kuua Vyama vya Upinzani. Serikali ya CCM itaendeleza kwa dhati kabisa mfumo wa Siasa ya Demokrasia ya Vyama vingi. Ushauri wangu tu kwa Vyama vya Upinzani ni kuacha kuwa wepesi wa kutafuta mchawi kila wanaposhindwa uchaguzi…."*

**16 Julai, 2010**

Dkt. Kikwete alihutubia Bunge alipokuwa anamaliza kipindi chake cha kwanza cha u-Rais ambapo alielezea umuhimu wa uanzishwaji wa Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na faida zake kwa Wabunge na wananchi:-

> *"… Bunge letu ni kielelezo cha ukomavu na ustawi wa Demokrasia yetu nchini"*

> *"Mheshimiwa Spika, kama mtakavyokumbuka, Mfuko wa Bunge tayari umeanzishwa na umelipa Bunge uhuru zaidi kwa bajeti yake.*

*Tumeendelea kuongeza bajeti ya Bunge na sasa ni mara mbili ya ile tuliyoikuta mwaka 2005. Maslahi ya Waheshimiwa Wabunge nayo tumeyaboresha, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, nao umeanzishwa ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge waweze kushughulikia matatizo madogo madogo yanayowakabili wananchi wao. Mazingira bora tuliyoyajenga yameliwezesha Bunge letu katika miaka mitano hii kufanya kazi kwa uhuru zaidi, uwazi zaidi na kwa mafanikio zaidi. "*

**7 Novemba, 2013**

Dkt. Kikwete alilihutubia Bunge kuhusu mchakato wa Katiba Mpya kwa kusema:-

*"Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bunge lako Tukufu, tunategemea kupata mambo mawili kutoka kwenu yatakayowezesha mchakato kutekelezwa vizuri katika hatua zinazofuata. Jambo la kwanza ni kutungwa kwa Sheria ya Kura ya Maoni na pili kufanyika kwa marekebisho ya nyongeza ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kuhusu Bunge Maalum ili kuboresha utekelezaji wake..."*

**Dkt. John Pombe Joseph Magufuli: 2015 hadi Machi, 2021**



Alikuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2015 hadi Machi, 2021. Alizaliwa tarehe 29 Oktoba, 1959 Chato, mkoani Mwanza (Geita) na kufariki tarehe 17 Machi, 2021. Aliwahi kuwa Waziri wa Ujenzi (2010 - 2015); Waziri

wa Mifugo na Uvuvi (2008 - 2010); Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (2005 - 2008); Waziri wa Ujenzi (2000 - 2005); na Naibu Waziri wa Ujenzi (1995 - 2000).

**20 Novemba, 2015**

Rais, Magufuli katika hotuba yake ya kufungua Bunge aliahidi Serikali kutoa fedha za Mfuko wa Bunge mapema ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zake: -

> *"Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama, kwa upande wa Bunge tutahakikisha fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zinapatikana kwa wakati ili Waheshimiwa Wabunge mkashirikiane na wananchi wetu kusukuma maendeleo ya maeneo mnakotoka".*

Rais Magufuli, aliwaasa Wabunge kuepuka vitendo vya kuliaibisha Bunge ili kulinda heshima yao na ya Bunge kwa ujumla:-

> *"... tusimame pamoja, Tanzania ni yetu sote. Tutangulize mbele maslahi ya nchi"*

> *"Ningewaomba tusimame pamoja Tanzania ni yetu sote, tutangulize mbele maslahi ya nchi na kwa mara ya kwanza Watanzania waone Bunge tofauti na siyo Bunge la kuzomea, kutoka nje, kutukanana, mipasho na kadhalika..........ni lazima sasa tujenge dhana ya kutanguliza maslahi ya Watanzania tunaowaongoza badala ya maslahi ya kuzomea, yanaaibisha Bunge hili. Bunge ni chombo muhimu sana katika mihimili ya Taifa letu".*

**Samia Suluhu Hassan: Machi 2021 hadi sasa**



Ni Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia 19 Machi, 2021. Alizaliwa tarehe 27 Januari, 1960, Makunduchi, Zanzibar. Wasifu wake kwa undani upo kwenye kipengele cha Wabunge Wanawake Walioshika Nafasi za Uongozi Kitaifa na Kimataifa.

**22 Aprili, 2021**

Rais Samia alilihutubia Bunge kwa mara ya kwanza kwa dhamira ya kueleza Dira na Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita. Katika hotuba hiyo alieleza nia yake ya Kudumisha mazuri ya Awamu zilizopita, Kuyaendeleza mema yaliyopo na Kuleta mengine mapya. Aidha, Rais aliwaomba Wabunge kuwawakilisha vema wananchi kwa kujadili masuala yenye manufaa kwa Taifa. Alisema:-

> *"…Ninyi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi na kwa maana nyingine, ninyi ni sauti ya wananchi. Hivyo, sitegemei kuona Bunge hili likijielekeza kujadili masuala ambayo hayana manufaa kwa Taifa letu."*

Vile vile, alielezea umuhimu wa ushirikiano wa Bunge na Serikali ili kurahisisha utekelezaji wa dira na mweleko wa Serikali, kwa kusema:-

*"...Mawaziri wakileta vitu visivyoeleweka, wakosolewe..."*

*"…Tukosoeni pale inapobidi. Mawaziri wakileta vitu visivyoeleweka wakosolewe lakini kwa staha. Nami naahidi kuwa Serikali itakuwa tayari, wakati wote, kupokea ushauri wenu na pia ushauri wa watu wengine wenye nia ya kuiletea maendeleo nchi yetu…"*

**Hotuba za Wageni Mashuhuri**

Tanzania imekuwa na mahusiano mazuri na mataifa mbalimbali ambapo kutokana na uhusiano huo viongozi wa mataifa hayo wamekuwa wakifanya ziara za kitaifa katika nchi yetu. Wakati wa ziara hizo, baadhi yao walipata fursa ya kutembelea na kulihutubia Bunge. Baadhi ya Wageni hao ni wafuatao:-

**Joachim Chissano - Msumbiji**



Mnamo tarehe 27 Julai, 1995, Joachim Chissano, aliyekuwa Rais wa Msumbiji alilihutubia Bunge Jijini Dar es Salaam. Katika hotuba yake alizungumzia umuhimu wa amani na utulivu katika kuleta maendeleo ya Taifa na kuishukuru Tanzania kwa mchango wake katika harakati za kutafuta uhuru wa nchi yake kwa kuwahudumia wapigania uhuru waliokuwa Tanzania, na hivyo kuiona nchi hii ni sehemu maalumu kwa watu wa Msumbiji. Sehemu ya hotuba hiyo ilisema:-

> *"... Tanzania has become a special sanctuary for the people of Mozambique"*

*"...Tanzania has become a special sanctuary for the people of Mozambique and that is why we feel so much at home..."*

Rais Chissano pia alizungumzia umuhimu wa wanasiasa kuisaidia Serikali kwa kubainisha utatuzi wa masuala mbalimbali yanayoikabili nchi ili kusaidia maendeleo ya nchi kwa faida ya wananchi wote. Aidha, kwa kuwa nchi ilikuwa inaingia katika uchaguzi aliwasihi Watanzania kufanya uchaguzi wa amani na kukubaliana na matokeo kama walivyofanya Msumbiji. Alisema:-

> *"...We therefore would like to urge all politician contenders involved in this exercise to put the people's interests above their own interests. So as to ensure their contribution for the creation of a more participatory society in which every Tanzania will continue to have a say and opportunity to give his best for the development of this country".*
>
> *"...they said that the election in Mozambique were exemplary to the whole world because, in many years the participation of the people in elections, in multi-lateral elections, was so big, more than 95 percent of the electorate went to vote...there was no fight during elections...So we would urge that in Tanzania everyone should go to this people context knowing that at the ultimate analysis the people should be the only winner".*

**Filipe Jacinto Nyusi - Msumbiji**



Rais wa Msumbiji, Filipe Jacinto Nyusi alililihutubia Bunge, Jijini Dodoma tarehe 19 Mei, 2015. Katika hotuba yake alielezea umuhimu wa Bunge la Msumbiji kuwa na ushirikiano na Bunge la Tanzania ili kufahamu utatuzi wa changamoto mbalimbali kwa ustawi wa nchi zetu mbili na Bara la Afrika kwa ujumla. Sehemu ya hotuba hiyo ilisema:-

> *"Our National Assembly has been experiencing positive and encouraging developments. But we want its performance increasingly strengthened through interaction and networking with other National Assemblies, like this one, because out of this engagement and combination of synergies, bilateral and, indeed regional responses for common challenges will emerge, for the welfare and progress of our two countries and the region"*

Pia aliwakumbusha Wabunge jukumu lao la kizalendo la kukuza na kudumisha uhusiano na urafiki uliopo ili kuepusha migogoro baina ya nchi hizi mbili.

> *"…MPs from two countries have a patriotic duty to promote and cement the prevailing historical and friendly co-existence"*

*"We are of the view that MPs from two countries have a patriotic duty to promote and cement the prevailing historical and*

*friendly coexistence between our countries, free movement of people, goods and services and particularly, entrenching cross-border development as a key factor for prevention and elimination of territorial conflicts"*

**Rais Ahmed Abdallah Mohamed Sambi – Visiwa vya Comoro**



Rais wa Visiwa vya Comoro, Ahmed Abdallah Mohamed Sambi, alilihutubia Bunge tarehe 25 Agosti, 2008, Dodoma. Katika hotuba hiyo aliishukuru Tanzania kwa kuisaidia nchi yake kukikomboa Kisiwa cha Anjouani na kusaidia kudumisha umoja wa kitaifa na mtangamano. Sehemu ya hotuba hiyo alisema:-

*"The recognition of my people and my government is immense and infinite for the sacrifices without limits made by the Tanzanian people and the government. You did not hesitate to send, which you have moreover expensive, namely your children, to be with the head of the forces of the African coalition come to release the Comorian island of Anjouan, to help my country to consolidate its national unity and to restore its territorial integrity. You can be proud of its valiant soldiers. The Comorian nation will be eternally grateful to them".*

Rais Sambi katika hotuba yake pia alimsifu Mwalimu Nyerere, mwasisi wa Taifa la Tanzania, kwa uongozi wake uliokuwa na maono na hekima na aliyesaidia nchi yake na nchi nyingi za Afrika katika harakati za kupigania uhuru, kulinda amani na kuleta maendeleo, ambaye atakumbukwa daima na kizazi cha sasa na kijacho, alisema:-

> *"... Mwalimu was of these rare men who worked the History"*

*"But I also greet in you, worthy successors of Fire President Mwalimu Julius Nyerere, Fondateur of Tanzania Moderne, worthy child of Tanzania and of Africa charisma, great wisdom and vision… Mwalimu was of these rare men who worked the History, not only of their people but of all Humanity. The ground produced very few of these great men, who by their vision, their conviction and their wisdom mark forever their passage over ground. This man will remain forever in the spirit of the generations present and to come".*

**Hoja Binafsi, Kamati Teule, Kamati Maalum na Kamati Ndogo za Bunge**

Hoja nyingi zinazojadiliwa bungeni chanzo chake ni kutoka serikalini hata hivyo Kanuni za Bunge zinaruhusu hoja binafsi kuwasilishwa bungeni, ambapo hoja hizo zinaweza kutoka kwa Mbunge mmoja mmoja au Kamati ya Bunge. Wakati mwingine hoja binafsi husababisha kuundwa kwa

Kamati Teule au Kamati Maalumu. Kwa mujibu wa Kanuni, Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalumu na kwa hoja mahususi itakayotolewa na kuafikiwa.

Kwa upande mwingine, Kamati Maalumu huundwa na Spika kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni. Aidha, Kamati yoyote ya Kudumu ya Bunge inaweza kuunda kamati ndogo kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake na itapangiwa majukumu yake na Kamati ya Kudumu inayohusika. Baadhi ya Hoja binafsi, Kamati Teule, Kamati Maalumu na Kamati Ndogo zilizowahi kuundwa ni kama ifuatavyo:-

**Hoja ya Msamaha wa Kodi ya Mafuta**

Hoja hii iliwasilishwa na Chrisant Mzindakaya, aliyekuwa Mbunge wa Kwela katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 1996 akitaka maelezo kutoka Serikalini kuhusu msamaha wa kodi ya uingizaji wa mafuta ya kupikia yenye ujazo wa tani 4,700 uliotolewa na Waziri wa Fedha kwa Makampuni matatu.

Hoja hiyo ilisababisha Bunge kuiagiza Serikali kuleta maelezo juu ya suala hilo. Kutokana na agizo hilo, Waziri wa Fedha alitoa maelezo yaliyohusisha kufuta msamaha uliokuwa umetolewa awali na kuelekeza kuwa Makampuni hayo yatozwe kodi kwa viwango vipya vilivyotangazwa na Serikali katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 1996/97.

**Hoja ya Ukaguzi Maalum ya Akaunti ya Tegeta ESCROW**

Chimbuko la Hoja hii ni Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma (*Parastatal Organizations Accounts Committee* - POAC) wakati wa uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2009, ambapo moja ya Hoja ya Ukaguzi ilikuwa ni Kampuni ya IPTL kuwa chini ya ufilisi na hivyo fedha katika Akaunti hiyo kutolewa na kulipa madeni ya IPTL wakati wa ufilisi. Mwaka 2010, wakati Kamati ikiwasilisha taarifa yake ya mwaka ilitoa pendekezo la kuzuia utoaji wa fedha katika Akaunti hiyo hadi hapo migogoro kati ya TANESCO na IPTL kutatuliwa kwa maslahi ya Taifa, Bunge lilipitisha hoja hiyo na kuwa Azimio la Bunge.

Baada ya POAC kuvunjwa mwaka 2013, Kamati ya Hesabu za Serikali iliendelea kufuatilia suala hilo ambapo Machi, 2014 ilimwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi Maalum kuhusu miamala iliyofanyika katika Akaunti hiyo pamoja na umiliki wa Kampuni ya IPTL. Hoja hii ilihitimishwa kwa Bunge kupendekeza kuwawajibisha viongozi wa Serikali waliohusika.

**Kamati Teule ya Kuchunguza Tuhuma za Rushwa**

Kamati hii iliundwa mnamo tarehe 26 Agosti, 1996 kufuatia hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya tarehe 22 Agosti, 1996 kulitaka Bunge liunde Kamati Teule kuchunguza

tuhuma za rushwa zilizotolewa na Augustine Lyatonga Mrema aliyekuwa Mbunge wa Temeke dhidi ya viongozi waandamizi watatu wa Serikali na viongozi wawili wa CCM ili watoe msamaha wa kodi kwa makampuni ya uingizaji mafuta ya kula nchini. Baada ya kukamilisha kazi yake, Kamati ilipendekeza Rais ashauriwe kuchukua hatua dhidi ya Waziri wa Fedha na Maafisa waliohusika wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu za Utumishi wa Umma.

**Kamati Teule ya Kuchunguza Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura**

Kamati hii iliundwa tarehe 13 Novemba, 2007 ili kuchunguza mchakato wa zabuni ya uzalishaji umeme wa dharura, uliofanyika mwaka 2006 na kuipa ushindi *Richmond Development Company* LLC ya Houston, Texas, Marekani. Pia, Kamati ilitakiwa kuichunguza kwa kina *Richmond Development Company* LLC ili kujua umiliki, shughuli zinazofanywa na Kampuni hiyo na kupima uwezo wao wa uzalishaji umeme. Vilevile, Kamati ilitakiwa kutathmini mkataba baina ya *Richmond Development Company* LLC na TANESCO ili kujiridhisha kuhusu uhalali wa masharti ya mkataba huo, ikilinganisha na masharti yaliyomo katika mikataba ya aina hiyo iliyoafikiwa na TANESCO/Serikali. Baada ya kukamilisha kazi yake Kamati hiyo ilitoa taarifa Bungeni iliyosababisha Waziri Mkuu kujiuzulu na hivyo kuvunjwa kwa Baraza la Mawaziri.

**Kamati Teule ya Kuchunguza Migogoro ya Matumizi ya Ardhi**

Kamati hii iliundwa tarehe 9 Novemba, 2013 baada ya hoja iliyotolewa na Profesa Peter Msolla aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji tarehe 1 Novemba, 2013, kwamba Bunge liunde Kamati Teule ya kuchunguza na kuchambua kasoro mbalimbali za kisera zinazohusu Ardhi, Kilimo, Mifugo, Maji, Wanyamapori na Uwekezaji. Aidha, Kamati hiyo itoe mapendekezo ya kupunguza na kuondoa migogoro ya ardhi ya muda mrefu kati ya Wafugaji, Wakulima, Wawekezaji, maeneo ya Hifadhi, na Watumiaji wengine wa ardhi. Baada ya kukamilisha kazi yake, Kamati ilitoa mapendekezo ya muda mfupi, wa kati na mrefu ya utatuzi wa migogoro ya ardhi, huku ikihimiza migogoro hiyo kudhibitiwa na Serikali ili isiendelee kuleta athari kwa jamii na taifa kwa ujumla. Aidha, Kamati ilipendekeza Bunge liendelee kuisimamia Serikali katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa ili kuhakikisha migogoro hiyo inakwisha kabisa.

**Kamati Maalumu ya Uvuvi wa Bahari Kuu**

Kamati hii iliundwa kupitia Waraka wa Spika, Na.05 wa tarehe 17 Novemba, 2017 ulitolewa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 5 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kamati hii iliundwa ili kuchunguza na kushauri kuhusu usimamizi na udhibiti wa rasilimali za bahari kuu. Serikali imefanyia kazi mapendekezo ya Kamati kwa kuchukua hatua madhubuti za kurekebisha Sheria na

mifumo ya usimamizi, udhibiti na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi katika bahari kuu kwa lengo la kuhakikisha Taifa linanufaika.

**Kamati Maalumu ya Almasi**

Kamati hii iliundwa kupitia Waraka wa Spika, Na.03 wa tarehe 05 Julai, 2017 kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 5 (1) ya Toleo la Januari, 2016. Kamati hii iliundwa kwa lengo la kuchunguza na kushauri juu ya mfumo wa uchimbaji, usimamizi, udhibiti wa biashara na umilikiwa Madini ya Almasi. Serikali iliyafanyia kazi mapendekezo na ushauri wa Kamati hiyo, kwa kuondoa kasoro zilizokuweko katika mifumo ya uchimbaji, usimamizi, udhibiti wa biashara na umiliki wa madini ya Almasi kwa manufaa ya Taifa.

**Kamati Ndogo ya Operesheni Tokomeza**

Kamati Ndogo ya kuchunguza matatizo yaliyosababishwa na Utekelezaji wa "Operesheni Tokomeza" iliundwa na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira; ili kuchunguza jinsi Operesheni hii iliyolenga kupambana na majangili ilivyopangwa na kutekelezwa, ili kubaini kama kulikuwa na ukiukwaji wa Sheria za nchi. Kuundwa kwa Kamati hii kulitokana na Uamuzi wa Spika alioutoa tarehe 01 Novemba, 2013, wakati Bunge likijadili jambo la dharura kwa mujibu wa Kanuni ya 47 ya Toleo la 2013, lililowasilishwa na Said Nkumba (Mbunge wa Sikonge wa wakati huo). Kamati hii iliwasilisha mapendekezo na ushauri kwa Serikali, ambao ulisababisha uwajibikaji kwa Mawaziri

Wanne waliokuwa wakiongoza Wizara za Maliasili na Utalii, Mambo ya Ndani ya Nchi, Mifugo na Uvuvi, na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Kamati Maalumu ya Tanzanite**

Kamati hii iliundwa tarehe 02 Juni, 2017 kwa lengo la kushauri kuhusu ufanisi katika Uchimbaji, Usimamizi na Udhibiti wa Biashara ya Madini ya Tanzanite nchini. Kamati iliundwa kwa mujibu wa Waraka wa Spika Namba 02 wa mwaka 2017, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 5 (1) ya Toleo la Januari, 2016. Aidha, kuundwa kwa Kamati hii Maalumu kulichangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kutoridhishwa na mchango wa sekta ya madini katika maendeleo ya taifa; matokeo ya Kamati za kiuchunguzi zilizoundwa na Rais kuhusiana na Usimamizi wa Madini ya dhahabu; na Azimio la Bunge la tarehe 14 Juni, 2017 la kuunga Mkono juhudi za Rais katika ulinzi wa rasilimali na maliasili za nchi kwa manufaa ya taifa. Serikali imefanyia kazi mapendekezo yaliyowasilishwa na Kamati kwa kuchukua hatua madhubuti za kulinda, kudhibiti na kusimamia uchimbaji na biashara ya Tanzanite ili kuongeza pato la taifa.

# SURA YA TISA

# MAFANIKIO

## Utangulizi

Sura hii inahusu mafanikio ya Bunge la Tanzania katika nyanja mbalimbali kutokana na utekelezaji wa majukumu yake ya ki-katiba ikiwa ni pamoja na kutunga Sheria na Kanuni za uendeshaji wa shughuli zake. Aidha, Bunge limefanikiwa kuboresha miundombinu ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa Wabunge, Watumishi na wadau mbalimbali. Baadhi ya mafanikio hayo ni:-

## Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo

Mchakato wa utungwaji wa Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa na kupitishwa na Bunge katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge la Tisa, mwaka 2009. Lengo la mfuko huo ni kuongeza kasi ya utatuzi wa kero za wananchi hasa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Uanzishwaji wa mfuko huo umeinua ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo, kukuza ajira na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ugawaji wa rasilimali kwenye ngazi ya Halmashauri.

## Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu

Huu ni utaratibu wa Wabunge kumuuliza Waziri Mkuu maswali ya papo kwa papo katika kutimiza jukumu la Bunge la kuisimamia Serikali. Utaratibu huo ulianza mwaka 2008 katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Tisa, kufuatia mabadiliko ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Utaratibu huu unafanana na Bunge la Uingereza ambalo hutumia dakika thelathini katika siku ya Jumatano kwa ajili ya Wabunge kumuuliza Waziri Mkuu maswali ya Papo kwa Papo. Hivyo, Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Novemba 2007, zilianzisha utaratibu wa Wabunge kumuuliza Waziri Mkuu maswali ya Papo kwa Papo wakati wa Mikutano ya Bunge na siku ya Alhamisi ilichaguliwa kwa ajili hiyo. Aidha, utaratibu huo ulianza rasmi katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge hilo la Tisa.

**Mabadiliko ya Mfumo na Mzunguko wa Bajeti**

Mabadiliko ya mfumo na mzunguko wa bajeti ya Serikali yalilenga kuwezesha bajeti kujadiliwa kuanzia Aprili hadi Juni badala ya Juni hadi Agosti na hivyo kuruhusu bajeti ya Serikali kuanza kutumika sambamba na mwaka mpya wa fedha ambao huanza tarehe 1 Julai ya kila mwaka, na bajeti za Wizara kujadiliwa kabla ya bajeti kuu kama ilivyokuwa awali ya kuanza kwa bajeti kuu kabla ya bajeti za Wizara. Mabadiliko hayo yanatoa fursa kwa Wabunge kujadili, kuchangia na kufanya maridhiano na Serikali kwenye maeneo ya kipaumbele. Ili kuwezesha utekelezaji wa mabadiliko hayo Kanuni za Bunge zilifanyiwa marekebisho mwaka 2013.

**Kamati ya Bajeti na Ofisi (Idara) ya Bajeti**

Kuanzishwa kwa Ofisi (Idara) ya Bajeti kulitokana na marekebisho ya Sheria ya Uendeshaji wa Bunge ya mwaka 2008, yaliyofanyika mwaka 2015 ili kutatua changamoto

katika masuala ya bajeti. Aidha, Sheria hiyo iliitambua na kuanisha majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na:- kujadili na kuchambua makadirio ya bajeti ya Serikali, mpango na miongozo ya bajeti ya Serikali, kufuatilia uwajibikaji wa Serikali katika utekelezaji wa bajeti na kulishauri Bunge. Aidha, Idara ya Bajeti ina jukumu la kuisaidia Kamati ya Bajeti ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Uboreshaji wa Miundombinu**



Kumekuwa na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali katika mazingira ya Bunge kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma. Miongoni mwa uboreshaji uliofanyika ni pamoja na:- kumbi za mikutano ya Bunge na Kamati, Ofisi za Watumishi, maeneo ya kutolea huduma mbalimbali, ujenzi wa kambarau (lifti) na njia za watu wenye ulemavu (ramp) na maegesho ya magari.

Uboreshaji mwingine uliofanyika ni usimikaji wa miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ambayo imewezesha matumizi ya simu za kisasa katika kila Ofisi, printa, kompyuta, skana, kompyuta mpakato, vishikwambi (tablets), mitambo ya kiusalama, mdaharishi (Internet Cafe), runinga katika Ofisi, mgahawa na maeneo mbalimbali ya mapumziko kwa ajili ya kufuatilia mijadala ya Bunge na waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao. Aidha, Ofisi ya Bunge imefanikiwa kusimika mitambo ya

kisasa ya uchapishaji inayotosheleza mahitaji yote muhimu ya uchapaji. Mitambo hiyo ina uwezo wa kuchapa kwa kasi, ubora na wingi wa machapisho na hivyo, kuongeza ufanisi na usalama wa nyaraka. Aidha Ofisi ya Bunge imefanikiwa kuongeza eneo lake sasa toka mita za mraba 42,000 hadi kufikia mita za mraba 120,000 mwaka 2024.


**Bunge Mtandao na Mifumo ya Kieletroniki**



Bunge liliingia katika matumizi ya mtandao katika uendeshaji wa Mikutano ya Bunge na vikao vya Kamati kwenye Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge la Kumi na Moja kwa kuanza kupunguza matumizi ya karatasi na kuanza kutumia vishikwambi (tablet). Bunge mtandao (e-parliament) pia liliwezesha shughuli za Bunge kuendelea hususani katika Mkutano wa Kumi na Tisa, wakati kukiwa na changamoto ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID 19) ambapo, kumbi zaidi ya moja zilitumika kuendesha kikao kwa wakati mmoja ili kuepuka msongamano.

Aidha, mifumo mingine ya kieletroniki iliyopo katika lango la TEHAMA (ICT Portal) la Bunge ni mifumo ya uendeshaji wa Bunge, Masijala, Maktaba, Barua pepe, Utunzaji wa Nyaraka, Tovuti ya Bunge (www.parliament.go.tz), Mahudhurio (biometric), Orodha na Anwani za Watumishi (staff directory).

**Studio ya Televisheni ya Bunge**



Uratibu wa shughuli za Bunge hujumuisha huduma na miundombinu ya urushaji wa matangazo kwa njia ya televisheni. Ofisi imefanikiwa kusimika mitambo ya studio ya televisheni ambayo hutumika kuandaa vipindi na kurusha matangazo kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Aidha, vyombo vingine vya habari vimekuwa vikirusha vipindi vinavyoandaliwa na studio ya Bunge kama vile "Jimbo lako".

**Miongozo ya Utoaji wa Huduma za Bunge**

Bunge limefanikiwa kuandaa Miongozo ya utoaji wa huduma mbalimbali kwa ajili ya Wabunge, Watumishi na Wadau wengine. Baadhi ya Miongozo iliyoandaliwa inahusu:- huduma za utafiti, sera ya Maktaba, sera ya TEHAMA, usimamizi wa vihatarishi, hoja binafsi bungeni, muswada binafsi, uchambuzi wa muswada wa sheria, uridhiaji wa mikataba ya kimataifa, usikilizaji wa maoni ya wadau, na ziara za Kamati za Bunge. Miongozo hiyo imesaidia jamii kuelewa mambo ya kuzingatia wakati wa kujihusisha na masuala ya Bunge. Aidha, Miongozo hiyo inapatikana katika Tovuti ya Bunge (www.parliament.go.tz).

**Kituo cha Afya**

Ofisi ya Bunge imeboresha utoaji wa huduma ya afya kwa kuanzisha Kituo cha Afya chenye Madaktari bingwa, vifaa tiba, maabara, vitanda, vitendanishi (reagents), na magari

mawili ya wagonjwa yenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuhudumia Wabunge, Watumishi wa Bunge na wadau wengine. Aidha, Kituo kinahudumia wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.



*Kituo cha Afya cha Bunge*

## MAREJELEO


Africa Journal Limited, (1981). **Africa Who's Who.** Kirkman House, London, England.

BTg. (1962). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Mkutano wa Pili, Kikao cha Kwanza, tarehe 5 Juni. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (2014). **Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali kuhusu Matokeo ya Ukaguzi Maalum wa CAG katika Akaunti ya Tegeta ESCROW**. JMT, Dar es Salaam.

BTz. (1964). **Taarifa Tasmi za Bunge** (Hansard). Mkutano wa Kumi na Tatu, tarehe 25 Aprili – 12 Mei. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1964). **Taarifa Tasmi za Bunge** (Hansard). Mkutano wa Kumi na Nne, tarehe 8 - 9 Septemba. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1970). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Kwanza, Mkutano wa Saba, tarehe 27 Juni – 11 Julai. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1975). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Nne, Mkutano wa Kwanza, tarehe 6 - 8 Novemba. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1978). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Mkutano wa Tisa, tarehe 21 - 22 Februari. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1986). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Tano, Mkutano wa Pili, tarehe 28 – 30 Januari. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (1988). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Tano, Mkutano wa Kumi, tarehe 12 Aprili. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1990). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Sita, Mkutano wa Kwanza, tarehe 6 - 10 Novemba. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1994). **Kanuni za Bunge.** Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1994). **Orodha ya Wabunge.** Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1995). **Kanuni za Bunge.** Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1995). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Sita, Mkutano wa Saba, tarehe 25 Aprili – 3 Mei. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1996). **Bunge News: The New Parliamentary Complex, Julai 1996**. AMREF, Dar es Salaam

BTz. (1996). **Kanuni za Bunge.** Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1997). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Saba, Mkutano wa Saba, tarehe 8 – 11 Aprili. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1998). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Saba, Mkutano wa Kumi na Tatu tarehe 4 Novemba. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.

BTz. (1999). **Who is Who in the Tanzania Parliament.** Ofisi ya Bunge, Dar es Salaam.

BTz. (2000). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Saba, Mkutano wa Kwanza, tarehe 14 - 20 Novemba. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2002). **Kanuni za Kudumu Bunge.** Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2003). **Kanuni za Kudumu Bunge.** Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2004). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Saba, Mkutano wa Kumi na Nne tarehe 12 Februari. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2005). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Nane, Mkutano wa Kumi na Tisa, tarehe 29 Julai. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2005). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Tisa, Mkutano wa Kwanza, tarehe 28 - 30 Desemba. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2006). **Orodha ya Wabunge.** Ofisi ya Bunge, Dodoma

BTz. (2007). **Kanuni za Kudumu Bunge.** Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2007). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Tisa, Mkutano wa Nane, tarehe 13 Novemba. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2008). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Tisa, Mkutano wa Tano, tarehe 01 Februari. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2008). **Orodha ya Wabunge.** Ofisi ya Bunge, Dodoma.
BTz. (2008). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Tisa, Mkutano wa Saba, tarehe 25 Agosti. Ofisi ya Bunge, Dodoma.
BTz. (2009). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Tisa, Mkutano wa Kumi na Sita, tarehe 31 Julai. Ofisi ya Bunge, Dodoma.
BTz. (2010). **Orodha ya Wabunge.** Toleo la Tano, Ofisi ya Bunge, Dodoma.
BTz. (2010). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Kumi, Mkutano wa Kwanza, tarehe 8 Novemba. Ofisi ya Bunge, Dodoma.
BTz. (2010). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Tisa, Mkutano wa Ishirini, tarehe 16 Julai. Ofisi ya Bunge, Dodoma.
BTz. (2013). **Kanuni za Kudumu Bunge: Toleo la Aprili.** Ofisi ya Bunge, Dodoma.
BTz. (2014). **Orodha ya Wabunge.** Toleo la Kumi na Tisa, Ofisi ya Bunge, Dodoma
BTz. (2015). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Kumi na Moja, Mkutano wa Kwanza, tarehe 20 Novemba. Ofisi ya Bunge, Dodoma.
BTz. (2015). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Kumi, Mkutano wa Saba, tarehe 6 Februari. Ofisi ya Bunge, Dodoma.
BTz. (2015). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Kumi, Mkutano wa Kumi na Tisa, tarehe 27 Machi. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2015). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Kumi, Mkutano wa Kumi na Tisa, tarehe 19 Mei. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2015). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Kumi, Mkutano wa Kumi na Tisa, tarehe 9 Julai. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2016). **Kanuni za Kudumu Bunge: Toleo la Januari.** Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2020). **Orodha ya Wabunge.** Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2020). **Kanuni za Kudumu Bunge**: Toleo la Juni. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2020). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Nane, tarehe 28 Januari. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2021). **Orodha ya Wabunge. Toleo la Pili,** Ofisi ya Bunge, Dodoma.

BTz. (2021). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Bunge la Kumi na Mbili, Mkutano wa Tatu, tarehe 22 Aprili. Ofisi ya Bunge, Dodoma.

Halimoja, Y. (1975). **Bunge la Tanzania.** The East African Literature Bureau, Dar es Salaam.

Halimoja, Y. (1981). **Tanzania inayojitawala.** Morco printers Limited, Dar es Salaam.

JMT, (1965). **Hotuba ya Rais Mwalimu Julius K. Nyerere**, tarehe 12 Oktoba. JMT, Dar es Salaam.

JMT, (1965). **Hotuba ya Rais Mwalimu Julius K. Nyerere, tarehe 8 Juni.** JMT, Dar es Salaam.

JMT, (1965). **Hotuba ya Rais Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya tarehe 14 Desemba.** JMT, Dar es Salaam.

JMT, (1985). **Hotuba ya Rais Ali Hassan Mwinyi ya tarehe 7 Novemba**. JMT, Dar es Salaam.

JMT, (1985). **Hotuba ya Rais Mwalimu Julius K. Nyerere, tarehe, 29 Julai**. JMT, Dar es Salaam.

JMT, (1996). **Taarifa ya Uchunguzi wa Kamati Teule ya Bunge Kuhusu Tuhuma za Rushwa dhidi ya Viongozi Watatu Waandamizi wa Serikali na Wawili wa CCM, ya Oktoba**. JMT, Dar es Salaam.

JMT, (2001). **Taarifa ya Kamati ya Serikali ya Kuchunguza Hoja ya Utaratibu wa Kuingiza Sukari Nchini, ya tarehe 17 Oktoba**. JMT, Dar es Salaam.

JMT, (2002). **Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura 296 ya Marejeo ya Sheria za Tanzania.** JMT, Dar es Salaam.

JMT, (2013). **Hotuba ya Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ya tarehe 7 Novemba**. JMT, Dar es Salaam.

JMT, (2015). **Hotuba ya Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ya tarehe 9 Julai, 2015**. JMT, Dodoma.

JMT. (1965). **Katiba ya Mpito** (*Interim Constitution*). Wakala wa Uchapishaji wa Serikali (*Government Publication Agency*), Dar es Salaam.

JMT. (1977). **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Toleo la 1995**. M.P.P, Dar es Salaam.

JMT. (1977). **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Toleo la 2005**. Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam.

Kashilillah T, (1997). **The Parliamentary Mace**; in Bunge News Vol.3, AMREF, Dar es Salaam.
LEGCO. (1956). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Mkutano wa tarehe 25 Aprili. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.
LEGCO. (1957). **Taarifa Rasmi za Bunge** (Hansard). Mkutano wa tarehe 16 Septemba. Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam.
Magotti J. (2007**) Simba wa Vita katika Historia ya Tanzania: Rashidi Mfaume Kawawa**, Matai and Company Limited, Dar es Salaam
Makaidi, E. J. (1984). **Kamusi ya Kumbukumbu za Tanzania: 1497 - 1982**. Sunrise Publishers, Dar es Salaam.
MFAEAC, (2020). **Permanent Representatives: H.E. Ambassador Erasto Andrew Mbwana Mang'enya**. https://www.tzembassy.go.tz. accessed on 21 Machi, 2020.
Msekwa P. (2000) **Bunge la Kwanza Katika Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa Tanzania: 1995 – 2000**, DUP (1996) LTD, Dar es Salaam.
Msekwa P. (2012) **The Story of the Tanzania Parliament**, Hanns Seidel Foundation: East Africa, Tanzania Office, Dar es Salaam
Msekwa, P. (2000). **Reflections on Tanzania's First Multi-Party Parliament: 1995 - 2000**. DUP (1996) LTD, Dar es Salaam.
Msekwa, P. (2003). **Parliamentary Privileges in Tanzania**, DUP (1996) LTD, Dar es Salaam.

Msekwa, P. (2003). **A handbook for New Members of Parliament**. Dar es Salaam University Press, Ltd, Dar es Salaam.

Msekwa, P. (2012). **Uongozi na Utawala wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere: Miaka 25 ya Utumishi wangu kwa Umma chini ya Uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.** Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. & Sengo, T. (2005). **History of Kiswahili Poetry AD. 1000 - 2000.** The Institute of Kiswahili Research, UDSM, Dar es Salaam

Mwananchi Publications Ltd, (2011). **Abdulkarim Karimjee, Spika wa Kwanza Tanganyika huru**. Toleo la Jumatatu tarehe 7 Novemba, 2011 https://www.mwananchi.co.tz, accessed on 30 Julai, 2019

Ofisi ya Bunge. (2011). **Miaka Hamsini ya Uhuru, Maendeleo ya Bunge, Mafanikio na Changamoto.** Ofisi ya Bunge, Dodoma.

Ofisi ya Rais. (2011). **Taarifa ya Miaka Hamsini ya Uhuru wa Tanzania Bara: 1961 – 2011**. Ofisi ya Rais, Dar es Salaam

Oonk, G. (2009). **The Karimjee Javanjee Merchant**, Princes of East Africa: 1800 – 2000. Amsterdam University Press, Amsterdam.

PMO, (2020), **Former Prime Minister's Profile**. https://www.pmo.go.tz/index.php/former-prime-ministers, imetizamwa tarehe 17 Machi, 2020.

Sitta, S. Slaa, W. & Cheyo, J. (2008), **A Parliament with Teeth**. Africa Research Institute, London.

Sylivester J, (2011). **Ubadilishaji Msimbo Bungeni na athari zake kwa Wasikilizaji**. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

BTg, (1955). **The Legislative Council (Powers and Privileges) Ordinance Cap. 359 of the Law of Tanganyika.** BTg, Dar es Salaam.

URT, (1970). **Address of the President Mwalimu Julius K. Nyerere to the National Assembly: Arusha Declaration Parliament, on 6th of July, 1970**. URT, Dar es Salaam.

URT, (1980). **Address of the President Mwalimu Julius K. Nyerere to the National Assembly, on the 22nd July, 1980,** URT, Dar es Salaam.

URT, (2000). **Election Act of 1985: 2000 version.** URT, Dar es Salaam.

URT, (2002). **The Public Service Act.** URT, Dar es Salaam.

URT, (2008). **The National Assembly (Administration) Act.** URT, Dar es Salaam

**KIAMBATISHO I: Jedwali la Wabunge Wanawake kuanzia 1954 – 1985**

| NA. | JINA | AINA YA UBUNGE | WADHIFA | CHANZO |
|---|---|---|---|---|
| **Baraza la Kutunga Sheria: 1950 - 1955** | | | | |
| 1. | Bibi Elifuraha Mkamangi Marealle | kuteuliwa | Mbunge | Hansard 1-3/9 /1955 |
| 2. | Bibi S. Keeka | Kanda ya kati | Mbunge | Hansard 1-3/9 /1955 |
| 3. | Bibi K.F. Walker | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 1-3/9 /1955 |
| **Baraza la Kutunga Sheria: 1955 - 1960** | | | | |
| 1. | Bi. Kasindi | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 25/04/1956 |
| 2. | Bibi K.F Walker | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 25/04/1956 |
| 3. | Bibi Keeka | Kanda ya kati | Mbunge | Hansard 25/04/1956 |
| 4. | Bibi Elifuraha Mkamangi Marealle | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 25/04/1956 |
| 5. | Bi. B. Akim | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 6/05/1958 |
| 6. | Bibi J. Davis | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 6/05/1958 |
| **Baraza la Taifa la Tanganyika: 1960 - 1965** | | | | |
| 1. | Mhe. Marion Lady Chesham | Iringa | Mbunge | Hansard 11/12/1961 - 17/2/1962 |
| 2. | Mhe. Babro C Johansen | Mwanza | Mbunge | Hansard 11/12/1961 - 17/2/1962 |
| 3. | Mhe. E. Markwada | Tanga Urban | Mbunge | Hansard 11/12/1961 - 17/2/1962 |
| 4. | Mhe. Titi Mohamed | Rufiji | Mbunge | Hansard 11/12/1961 - 17/2/1962 |
| 5. | Mhe. S. Mustafa | Arusha | Mbunge | Hansard 11/12/1961 - 17/2/1962 |
| 6. | Mhe. Mwami Thereza Ntare | Kasulu | Mbunge | Hansard 11/12/1961 - 17/2/1962 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7. | Mhe. Lucy S. Lameck | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 11/12/1961 - 17/2/1962 |
| 8. | Mhe. Cecilia Paes | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 11/12/1961 - 17/2/1962 |
| **Bunge la Kwanza la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: 1965 - 1970** | | | | |
| 1. | Mhe. Violet M. Baraka | Njombe Kusini | Mbunge | Hansard 13 – 30/6/ 1967 |
| 2. | Mhe. Fatuma Haji | Mjumbe Wa Taifa | Mbunge | Hansard 13 – 30/6/ 1967 |
| 3. | Mhe. Pili Khamisi | B.L.M. Zanzibar | Mbunge | Hansard 13 – 30/6/ 1967 |
| 4. | Mhe. Jokha Mohamed Selemani | Kuteuliwa Zanzibar | Mbunge | Hansard 13 – 30/6/ 1967 |
| **Bunge la Pili la JMT: 1970 - 1975** | | | | |
| 1. | Mhe. Lucy S. Lameck | Moshi | Waziri Mdogo wa Afya na Ustawi wa Jamii | Hansard 19 - 27 /1/ 1971 |
| 2. | Mhe. Mboni O. Cheka | Mjumbe wa Taifa | Mbunge | Hansard 19 - 27 /1/ 1971 |
| 3. | Mhe. Pili Khamis | B.L.M Zanzibar | Mbunge | Hansard 19 - 27 /1/ 1971 |
| 4. | Mhe. Mwinchum Vuai | B.L.M. Zanzibar | Mbunge | Hansard 19 - 27 /1/ 1971 |
| **Bunge la Tatu la JMT: 1975 - 1980** | | | | |
| 1. | Mhe. Julie C. Maning | Kuteuliwa | Waziri wa Sheria | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 2. | Mhe. Tabitha Siwale | Kuteuliwa | Waziri wa Ardhi Nyumba na | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Maendeleo ya Mijini | |
| 3. | Mhe. Anna Abdallah | Katibu wa Chama wa Mkoa | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 4. | Mhe. Tabu M. Ali | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 5. | Mhe. Mtumwa Boraafya | Kuteuliwa Zanzibar | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 6. | Mhe. Mboni O. Cheka | Mbunge wa Taifa | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 7. | Mhe. Margaret Choggo | Mbunge wa Taifa | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 8. | Mhe. Anna Kabati | Kuteuliwa | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 9. | Mhe. Anna Makinda | Mbunge wa Taifa | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 10. | Mhe. Patma Hamza Mjanakheri | B. L. M. Zanzibar | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 11. | Mhe. Anna A. Namilikwa | Mbunge wa Taifa Singida | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 12. | Mhe. Mwinchumu Vuai | Kuteuliwa - Zanzibar | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| 13. | Mhe. Mkuja Suleiman Khamis | Kuteuliwa Zanzibar | Mbunge | Hansard 30/6 – 04/7/1980 |
| **Bunge la Nne la JMT: 1980 - 1985** | | | | |
| 1. | Mhe. Tabitha Siwale | Mbunge wa Taifa | Waziri wa Elimu wa Taifa | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 2. | Mhe. Anna Abdalah | Kamishna wa Mkoa | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 3. | Mhe. Thereza Olban Ali | B.L.W Zanzibar | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4. | Mhe. Ashura Abeid Faraji | Kuteuliwa Zanzibar | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 5. | Mhe. Amina Saadi Feruzi | Mbunge | Mbunge wa Taifa | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 6. | Mhe. Mwanabaraka Marijani Hassan | B.L.W Zanzibar | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 7. | Mhe. Fatuma Said Hamad Jadi | Mbunge wa Taifa Pemba Kaskazini | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 8. | Mhe. Lucy S.Lamecky | Mbunge wa Taifa/ Kilimanjaro | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 9. | Mhe. Simai Pandu Makame | B.L.W Zanzibar | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 10. | Mhe. Zainab Omar Mohamed | B.L.W Zanzibar | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 11. | Mhe. Raya Khamis Mwinyi | B.L.W Zanzibar | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 12. | Mhe. Mwinchumu Vuai | Kuteuliwa Zanzibar | Mbunge | Hansard 16/6 - 22 /7/1981 |
| 13. | Mhe. Anna Makinda | Mbunge Wa Taifa | Waziri wa Nchi Ofisi Ya waziri Mkuu | Hansard 20/6/1984 |
| 14. | Mhe. Corona Busongo | Mbunge | Mbunge Wa Taifa | Hansard 20/6/1984 |
| 15. | Mhe. Mboni O. Cheka | Mbunge wa Taifa | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |
| 16. | Mhe. Zaituni Fadhili | Mbunge wa Taifa/ Ruvuma | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |
| 17. | Mhe. Kate Kamba | Masasi | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 18. | Mhe. Kijakazi S Kyelula | Mbunge wa Taifa/ Dar es Salaam | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |
| 19. | Mhe. Julie Manning | Kamishna wa Mkoa | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |
| 20. | Mhe. Sarah Mwenge | Dodoma Mjini | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |
| 21. | Mhe. Anna Namilikwa | Mbunge wa Taifa/ Singida | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |
| 22. | Mhe. Cynthia H. Ngoye | Mbunge wa Taifa/ Iringa | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |
| 23. | Mhe. Penieli ole Saibatu | Arumeru | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |
| 24. | Mhe. Martha Wejja | Ilala | Mbunge | Hansard 20/6/1984 |
| | | | | |

**Tanbihi:** Wabunge Wanawake waliopo kwenye Jedwali hili waliingia Bungeni kabla ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Toleo la mwaka 1984 kutaja namna ya kuongeza nafasi za uwakilishi wa Wabunge Wanawake.

**KIAMBATISHO II: Ufafanuzi wa baadhi ya Maneno yanayotumika kwenye Shughuli za Bunge**

| NA. | MANENO | TAFSIRI |
|---|---|---|
| 1. | Akidi | Ni idadi ya Wabunge inayoruhusu Kamati au Bunge kufanya maamuzi kuhusu jambo fulani. |
| 2. | Azimio | Ni tamko au uamuzi wa Bunge kuhusu hoja mahsusi. |
| 3. | Bendera | Ni Bendera rasmi ya Bunge ambayo ina rangi ya bluu katika umbo la mstatili na yenye umbo dogo la bendera ya Taifa ndani yake katika pembe juu ya upande wa kushoto na Siwa, chini kukiwa na utepe wenye maneno "Bunge la Tanzania". |
| 4. | Bunge | Ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 62 ya Katiba. |
| 5. | Chama | Ni Chama cha Siasa chenye uwakilishi Bungeni. |
| 6. | Gazeti | Ni Gazeti la Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama lilivyotafsiriwa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria. |
| 7. | Hoja | Ni pendekezo linalotolewa na Serikali, Kamati au Mbunge ili lipate uamuzi wa Bunge. |
| 8. | Kamati | Ni Kamati yoyote ya Bunge iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. |
| 9. | Kamati ya Bunge Zima | Ni Kikao cha Wabunge wote wanapokaa kama Kamati chini ya uongozi wa Mwenyekiti. |
| 10. | Kamati Maalum | Ni Kamati inayoundwa na Spika kwa ajili ya kushughulikia jambo mahsusi. |
| 11. | Kamati ya Matumizi | Ni kikao cha Wabunge wote wanapokaa kama Kamati kushughulikia Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Serikali. |
| 12. | Kamati ya Mipango | Ni kikao cha Wabunge wote kwa lengo kujadili mapendekezo ya mpango Serikali. |
| 13. | Kikao cha Bunge | Ni kikao cha Bunge cha siku moja. |

| | | |
|---|---|---|
| 14. | Madaraka ya Bunge | Ni nguvu ya kisheria kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba. |
| 15. | Maeneo ya Bunge | Ni maeneo tengwa kwa matumizi ya Bunge. |
| 16. | Maisha ya Bunge | Ni muda wa kisheria wa Bunge tangu kuitishwa baada ya uchaguzi mkuu hadi kuvunjwa na Rais. |
| 17. | Mkutano wa Bunge | Ni mfululizo wa vikao vya Bunge, kuanzia kikao cha kwanza hadi cha mwisho. |
| 18. | Mpambe wa Bunge | Ni mbeba siwa kutoka Kitengo cha Ulinzi na Usalama wa Bunge. |
| 19. | Mwenyekiti wa Kamati | Ni Mbunge aliyechaguliwa na Wajumbe wa Kamati kutoka miongoni mwao kuongoza shughuli za kamati. |
| 20. | Ombi | ni wasilisho mahsusi la Mbunge, bungeni. |
| 21. | Orodha ya Shughuli | Ni mpangilio wa Shughuli za Bunge katika kila kikao cha Bunge. |
| 22. | Randama | Ni kitabu kinachofafanua utekelezaji wa bajeti ya Serikali. |
| 23. | Shughuli za Serikali | Ni Shughuli zinazowasilishwa Bungeni na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |
| 24. | Taarifa Rasmi za Bunge | Ni kumbukumbu za majadiliano ya Bunge au Kamati. |

**Chanzo: Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020**